# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Oktoba 10, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580045

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper





UKURASA 13

## UN yakumbwa na ukata, hofu yatanda hatima wafanyakazi

UKURASA 25

# Dar yaongoza kwa wagonjwa wa akili

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**RAIA WA CHINA WAKIRI KOSA, WALIPA MAMILIONI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru raia wawili wa China Li Ling na Chen Guo...

**UKURASA WA 3**

**TRA YAPEWA SIKU 75 KUWASILISHA WALIPAKODI**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ameipa Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA...

**UKURASA WA 26**

**MVUA KUBWA ZAIDI MIKOA YA PWANI**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imetoa tahadhari ya mvua kubwa zaidi kuanzia jana mpaka keshokutwa kwenye...




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akionyesha kitambulisho, kabla ya kujiandikisha kwenye daftari la wapigakura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika kituo cha Shule ya Msingi Kilimani, jijini Dodoma jana. Kulia ni mwandikishaji wa kituo hicho, Asha Mussa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Uandikishaji wapigakura wasuasua kila mahali

UKURASA 3

# Waumini watwangana makonde kanisani

**MCHUNGAJI** adaiwa chanzo, atiwa korokoroni, polisi yaeleza mkanda mzima... *Endelea ukurasa wa 2*


**MICHEZO** **YANGA: TUTAWASHANGAZA CAF** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Raia wa China wakiri kosa, walipa fidia

**Na Beatrice Shayo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru raia wawili wa China Li Ling na Chen Guo, baada ya kukiri makosa yao na kulipa fidia ya Sh. milioni 70.

Mahakama hiyo pia imetaifisha gari aina ya Toyota Prado T 982 CDH na mashine mbili za washtakiwa hao na kuwa mali ya serikali.

Pia imemtaka mshtakiwa Chen Guo kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la kuishi nchini bila kibali.

Uamuzi huo ulitolewa baada ya upande wa mashtaka kuwafutia washtakiwa hao mashtaka ya uhujumu uchumi na kuwasomea mashtaka mawili ya kujihusisha na nyara za serikali na kuishi nchini bila kibali.

Washtakiwa wengine wanne waliokuwa katika kesi moja na raia hao wa China wamegoma kukiri mashtaka yao yanayowakabili hivyo kurudishwa rumande.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi alisema mshtakiwa Li Ling atatakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 45 na Chen Guo, atalipa Sh. milioni 25 na faini ya Sh. milioni moja au kwenda jela mwaka mmoja.

Shaidi alisema gari aina ya Toyota Prado na mashine mbili zinataifishwa na kuwa mali ya serikali.

Raia hao wametakiwa kuondoka nchini mara moja kwa kuwa sio raia wa Tanzania.

**MPEMBA NAYE AKIRI**

Mfanyabiashara Yusufu Ali maarufu Mpemba wa Magufuli na wenzake wanaokabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi likiwamo la kujihusisha na biashara ya meno ya tembo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wameandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kuomba kukiri mashtaka hayo.

Mbali ya Mpemba, washtakiwa wengine ni Charles Mrutu, mkazi wa Mlimba Morogoro, Benedict Kungwa, mkazi wa Mbagala Chamazi, Jumanne Chima, mkazi wa Mbezi, Ahmed Nyagongo, dereva na Pius Kulagwa.

Wakili wa Serikali, Elizabeth Mkunde alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kwamba washtakiwa wameshaandika barua hivyo na kuiomba mahakama iwape muda kwa ajili ya kuingia katika makubaliano.

Hakimu Simba aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 16, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne ya kujihusisha na biashara ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 785.6.

Inadaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari, 2014 na Oktoba, mwaka huu wakiwa Dar es Salaam, Tanga, Iringa na Mtwara, walijihusisha na mtandao wa ujangili kwa kukusanya na kuuza nyara za serikali ambazo ni vipande vya meno ya tembo 50 vyenye thamani ya Dola za Marekani 180,000 sawa na Sh. milioni 392.8 bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

# Dar kinara kwa magonjwa ya akili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIKOA mitano imetajwa kuwa na wagonjwa wengi wenye magonjwa ya akili, huku Mkoa wa Dar es Salaam ukiongoza kuwa na idadi kubwa.

Hali ya kimazingira ukiwamo ugumu wa maisha na matumizi ya vilevi, vimetajwa ni miongoni mwa viashiria vinavyochangia tatizo hilo kwa maeneo ya mijini kuliko vijijini.

Akizungumza na Nipashe jana, Daktari wa Afya ya Akili katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ububuyu, alisema takwimu zilizopo kwa miaka mitatu kuanzia 2016 hadi 2018 zinaonyesha magonjwa ya akili yameongezeka kutoka 301,000 hadi 356,000.

"Kwa mwaka 2016 kulikuwa na wagonjwa 301,000 inahusisha magonjwa ya akili, kifafa na matumizi ya kilevi," alisema wakati akizungumzia maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani leo.

Alieleza kuwa magonjwa ya kifafa kwa ujumla wake baadhi yametibiwa kwenye idara ya magonjwa ya akili na mengine nje ya idara ambapo yana takribani asilimia 50 ya wagonjwa wote.

"Sasa magonjwa haya matatu katika takwimu za Wizara ya Afya na Tamisemi zinaonyesha katika vituo vya afya takribani wagonjwa 356,000 kwa mwaka 2018, pia asilimia 50 ya magonjwa ni ya akili na nyingine ni kifafa," alisema na kuongeza:

"Hii ni kwa hospitali ya mkoa na vituo vya afya, hapa hatujahusisha takwimu kutoka hospitali kama Muhimbili na Mirembe na hospitali zingine kubwa."

Mikoa vinara

Dk. Ububuyu alisema mijini kuna wagonjwa wengi zaidi ambapo takwimu hizo zinaonyesha Dar es Salaam inaongoza kuwa na wagonjwa asilimia 20 bila kujumuisha Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Mkoa mwingine ni Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Mwanza, yote mitano ipo juu na hali hii hapo katika magonjwa ya akili peke yake hata magonjwa yasiyo ya kuambukiza hali ipo hivyo hivyo."

"Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza halafu

INAENDELEA UK.8



Mtuhumiwa wa kesi ya kupatikana na nyara za serikali "meno ya tembo" raia wa China, Li Ling, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. Mtuhumiwa huyo, ameandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kukiri mashtaka yanayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waumini watwangana makonde kanisani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAUMINI wa Kanisa la Assemblies of God (TAG) Swaswa Mnarani mjini hapa, wametwangana makonde baada ya mchungaji wa kanisa hilo, Msafiri Malendaa, kukamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuuza viwanja 10 vya kanisa hilo.

Tukio hili lilitokea Oktoba 6, mwaka huu, majira ya saa nne asubuhi ndani ya kanisa hilo.

Nipashe ilishuhudia mchungaji Malendaa akikamatwa na polisi wakati akiendesha ibada madhabahuni na kupandishwa kwenye gari la polisi namba PT 4300.

Tukio hilo lilisababisha waumini kutoka nje ya kanisa na kuanza kuvutana huku wengine wakimtuhumu mchungaji huyo kuwa ni mwizi, huku wengine wakimtetea hali iliyosababisha baadhi yao kuanza kupigana makonde.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja wa waumini hao, Lidya Mgowela, alisema anashangaa kuona katibu wa kanisa akipigana na muumini.

"Nimetoa sadaka yangu, nilivyomaliza nikaona watu wanaanza kupigana nikaogopa sana nimekuja kutubu halafu kuna mambo haya, nipo hapa nje naangalia kinachoendelea ila ni mbaya sana mimi sijui chochote, nimeumia tena kanisa lenyewe ni kiroho," alisema.

Naye Paul Mathew alisema Jiji la Dodoma lilibomoa kanisa hilo katika eneo la Swaswa Mnarani kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara na kulilipa kifuta jasho kanisa viwanja 10 katika eneo la Ilazo Extension ili viuzwe na lijengwe kanisa jipya.

Alifafanua kuwa Jiji lilitoa viwanja hivyo na kumpa mchungaji huyo ambaye ilidaiwa aliandika viwanja hivyo majina ya familia yake na ndugu, jamaa na marafiki ili iwe rahisi kuviuza.

"Tuliona ni sawa kwani alisema vikiandikwa jina la taasisi vitakuwa vigumu kuuzwa na kanisa lilipewa kiwanja kingine cha kujenga hivyo kama tungeviuza vile tungepata fedha za kuendelea na ujenzi.

"Lakini alipoviuza fedha hakuna na hatujui kinachoendelea ukimuuliza anakufukuza kanisani, hali ambayo imesababisha kutokea kwa ngumi hizo," alisema.

Akizungumzia mgogoro huo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema anaufahamu na baada ya barabara kupita katika kanisa hilo, Jiji walitoa viwanja vya hisani ili waweze kuviuza na kuendelea na ujenzi wa kanisa mahali pengine walipopangiwa.

"Maelezo ya mchungaji ni kwamba viwanja vile viandikwe kwa majina binafsi inawezekana hapa ndipo walipokosea, ili viweze kuuzika na fedha ziendelee na ujenzi kama kuna mgogoro wameutengeneza wao sisi kama serikali tulishamaliza kuwapa viwanja," alisema.

Hata hivyo, Katambi alionyesha kusikitishwa na kitendo cha waumini hao kupigana ndani ya ibada.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema jambo hilo bado wanaendelea kufuatilia.

Nipashe ilipomtafuta mchungaji Malendaa kuzungumzia tuhuma hizo, alisema kuwa viwanja hivyo vipo na wanatafuta wateja ili waviuze.

"Tatizo kuna baadhi ya waumini ni wakorofi wanaamini mimi nimeviuza bila kuwashirikisha," alisema.

## HABARI KITAIFA

# TRA yapewa siku 75 kuwasilisha walipakodi

**Na Benny Mwaipaja**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ameipa Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA miezi miwili na nusu kuandaa na kuwasilisha wizarani orodha ya walipakodi, idadi ya majengo na mabango yote yaliyoko katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kupata takwimu sahihi za idadi ya walipakodi.

Dk. Kijaji ametoa muda huo hadi ifikapo Desemba 31, mwaka huu.

Alitoa muda huo jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya kikazi katika Mamlaka hiyo, mkoa wa kikodi wa Temeke ili kukagua utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hayo kwa lengo la kubaini fursa na changamoto za masuala ya ukusanyaji kodi.

Alisema pamoja na mamlaka hiyo kufanya vizuri katika makusanyo ya mapato mwezi Septemba 2019 kwa kukusanya Sh. trilioni 1.78, kiasi hicho bado ni kidogo ikilinganishwa na mwamko wa wananchi uliopo hivi sasa wa kulipa kodi.

Aliitaka TRA kuwasilisha kwake takwimu ya ongezeko la walipa kodi lililotokana na ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali nchini, akisema lengo la Rais Dk. John Magufuli kugawa vitambulisho hivyo lilikuwa ni kuongeza wigo wa walipa kodi watakao kuwa wanafuzu kwa kuongeza mitaji yao, hivyo ni vyema kujua idadi yao na mahali walipo.

Kwa upande wa kodi ya majengo, Dk. Kijaji aliitaka TRA kuhakikisha inapata orodha ya nyumba zote nchini kwa kuorodhesha wamiliki wa nyumba hizo na mawasiliano yao na kisha kuandaa kanzidata itakayosaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi hiyo.

"Nataka pia mkague watumiaji wote wa mashine za utoaji risiti za kielektroniki (EFD) kwa wafanyabiashara wa Temeke ili kuhakikisha kila anayeuza anatoa risiti na anayenunua anadai risiti na kwa kufanya hivyo itasaidia kuongeza makusanyo ili taifa liendelee kujitegemea kimapato," alisisitiza Dk. Kijaji.

# Uandikishaji wapigakura wasuasua kila kona

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI uandikishaji wapigakura katika Daftari la Wapigakura ukiendelea kwa kusuasua katika sehemu mbalimbali nchini, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan amewataka Watanzania kujitokeza kwa wingi na kuchagua viongozi wenye maadili na watakaoendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano.

Uandikishaji wa wapigakura katika daftari hilo ni kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Hata hivyo, tofauti na vituo vingine wakati wananchi hutakiwa kuandika majina matatu bila kuulizwa kitambulisho, katika kituo alichoandikishwa Makamu wa Rais, mwandikishaji, alimtaka kuonyesha kitambulisho.

Hatua ya wananchi kujiandikisha bila kuonyesha kitambulisho imewafanya baadhi yao kujiuliza kama hakutatokea udanganyifu wakati wa kupiga kura.

Makamu wa Rais, alijiandikisha jana katika kituo cha Shule ya Msingi Kilimani, mjini Dodoma.

Samia alisema: "Tujitokeze kwa wingi Watanzania kujiandikisha na kwenye kupiga kura tuchague viongozi wanaotusimamia mambo yetu katika mitaa yetu, mimi nimetumia fursa hii kujiandikisha katika mtaa wa Salimin ili kuchagua viongozi wangu, kwa kuwa najua makazi yangu yapo Dodoma na hawa ndio watakaonisimamia mambo yangu katika mtaa wangu."

Aliwataka kuchagua viongozi watakaokuwa na maadili ya kuwatumikia Watanzania, ya kutunza rasilimali zao na kuiletea Tanzania maendeleo.

INAENDELEA UK. 8



Kamishna wa Opereshени na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, CP Liberatus Sabas, akizungumza na madereva wa bodaboda waliopo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, eneo la Mtipesa, mkoani Mtwara jana, wakati kamati ndogo ya vyombo vya ulinzi na usalama walipokagua vipenyo rasmi na visivyorasmi vinavyotumiwa na wahalifu kutoka nchi jirani ya Msumbiji. **PICHA: POLISI**

# Ushirikina kikwazo mapambano fistula

**Na Mary Geofrey**

IMANI za kishirikiana zimetajwa kuchangia tatizo la fistula kuendelea kuwatafuna wanawake wengi kutokana na kwenda kwa waganga wa kienyeji, hivyo kuchelewa kupata matibabu hospitali.

Mratibu wa Huduma ya Wanawake wenye Fistula katika Hospitali ya CCBRT, Theodorath Mullinga, alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam, wakati akipokea misaada iliyotolewa na Kanisa la Waadventista wa Sabato Tawi la Kinondoni katika kuadhimisha miaka 10 ya kwaya yao ya Gethsemane.

Alisema wanawake wengi wanachelewa kupata matibabu na badala yake hukimbilia kwa waganga wa kienyeji wakiamini huo si ugonjwa bali wamelogwa na watu wao wa karibu.

"Tunapoenda kuwachukua

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
05-10-2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 13-10-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Chang'ombe, gari hizo zenye namba za usajili:

   **T 636 DFA / T 887 DJB**
   **T212 BTE/T 574 BZB**
   **T653 DFA/T 900 BAZ**
   **T195 BTE/T837 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 27 |
| **Upana** | - | mita | 4.0 |
| **Kimo** | - | mita | 5.1 |

3. Njia itakayotumika: Dar es salaam Port hadi Chang'ombe kupitia Mandela road, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215454002



## NAFASI ZA MASOMO KOZI YA UUGUZI NA UKUNGA (NURSING AND MIDWIFERY)

**Chuo cha A3 Institute of Professional Studies.**
Kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi ya Ukunga na Uuguzi (Nursing and Midwifery)
Kwa ngazi ya Cheti (Certificate)

Muombaji awe amaehitimu kidato cha NNE (form iv) na kufaulu masomo matatu (3) ya sanyansi, Biology, Chemistry na Physics kwa alama D, Kiingereza na Hisabati ni sifa ya ziada.

Chuo kimesajiliwa na Wizara ya Afya na ustawi wa jamii, TNMC, na NACTE.

Chuo kina mazingira mazuri nayakuvutia pamoja na walimu wenye weledi, ujuzi na uzoefu.

***Ada zetu ni za kuridhisha na utalipa kwa awamu.***

Chuo ni cha kutwa,na nafasi za hosteli zinapatikana. Masomo yataanza tarehe 15 October 2019.

**Chuo kipo kibaha mpakani (mkoa wa Pwani).**
Pia kuna nafasi za masomo ya ualimu {Grade A,Diploma na chekechea] na uandishi wa habari{journalism}nafasi za masomo chekechea,msingi(English medium)sekondari kidato I – iv.

**Mawasiliano zaidi : 0655 573011 / 0718321095/ 0659573003 / info@wipahs.co.tz S.Lp 19711 Dar -es-salaam**

115454902

## HABARI KITAIFA

# Hakimu kuburuzwa mahakamani tuhuma za rushwa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga, inatarajia kumfikisha mahakamani Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Benjamini Mhangwa, kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 200,000.

Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Shinyanga, Husseni Mussa, alisema juzi kuwa Septemba, mwaka huu, hakimu huyo aliomba rushwa ya Sh. 300,000 kutoka kwa mzazi ambaye mtoto wake alibakwa, ili amsaidie kushinda kesi yake na kufanikiwa kukamatishwa na Sh. 200,000.

Alisema hakimu huyo alimfuata mzazi wa mtoto ambaye amebakwa na kumrubuni kuwa ametumwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kishapu, Wilberforce Luhwago, ili wamsaidie kupata ushindi kwenye kesi hiyo.

"Baada ya mzazi huyo kuombwa kiasi hicho cha fedha alitoa taarifa kwetu na tukamwekea mtego hakimu wa Sh. 200,000 na kufanikiwa kumkamata na fedha hizo kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007," alisema Mussa.

"Katika uchunguzi ambao tumeufanya, tumebaini kuwa fedha hizo za rushwa hazikuombwa na Hakimu Luhwago bali ziliombwa na hakimu huyo wa Mahakama ya Mwanzo tutakayemfikisha mahakamani," aliongeza.

Mussa alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kuendelea kutoa taarifa kwa taasisi hiyo juu ya vitendo vya rushwa ili wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria na kukomesha vitendo hivyo.



Rais John Pombe Magufuli akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine, akiwa katika ziara yake mkoani Rukwa juzi. Rais alisisitiza uendelezaji wa viwanda na kuyaongezea thamani mazao ikiwamo ya kuchakata pamba na kahawa na sio kuuza malighafi pekee baada ya kuvuna. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyepinga kufukuzwa kazi TRA kwa cheti cha kughushi ashindwa kesi

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), imesema uamuzi uliofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) dhidi ya mlalamikaji Salehe Hussein wa kufukuzwa kazi baada ya kukutwa na cheti cha kughushi cha kidato cha nne, ulikuwa sahihi.

Akisoma hukumu ya kesi hiyo Jumatatu jijini Dar es Salaam, Ofisa Mfawidhi Mkoa wa Dar es Salaam, Usekelege Mpulla, alisema TRA walifuata utaratibu wa kumwachisha kazi mlalamikaji (Hussein) aliyekuwa Ofisa wa Msaidizi wa kushughulikia ulinzi wa mipaka.

Kesi hiyo ilikuwa ikisimamiwa na wakili wa upande wa mlalamikaji Heriel Munisi na upande wa mlalamikiwa, Jacqueline Chunga.

Upande wa mlalamikiwa ulikuwa na mashahidi wawili, Ofisa Rasilimali Watu wa TRA, Sixmund Matembo na Ofisa Rasilimali Watu TRA kituo cha Zanzibar, Haula Issa.

Upande wa mlalamikaji ulisema hauna shahidi mwingine.

Mpulla alisema kuwa Chunga alieleza kuwa cheti kilichohakikiwa na kuonekana ni cha kughushi kilikuwa na namba P.0083-390 cha mwaka 1990 chenye jina la Salehe Hussein Salehe na kwamba kilikutwa kwenye jalada binafsi la mlalamikaji.

"Kabla ya kutoa amri za mwisho nawiwa kuvaa vazi la kuelimisha na kusema maneno mawili kuhusiana na kile nilichobainika kwenye shauri hili ambalo nalichukulia ni la kipekee," Mpulla alisema.

Alisema inasikitisha kuona mtu anaajiriwa bila vyeti vyake kuhakikiwa vyema hali inayosababisha kuwapo kwa vyeti vya kughushi kutokana na mbegu iliyopandwa na waajiri wenyewe.

"Ifahamike kwamba kwa wengi waaminio, hakuna kitu kinachodumu isipokuwa Mungu hivyo ukiukwaji wowote wa sheria, kanuni na taratibu hata kama mwanzo hautaonekana inakuwa ni mbegu ambayo haijalishi imekaa muda gani, siku moja inaweza kuota na kuleta matunda ambayo yeyote aliyepanda atavuna.

"Labda, nimeandika kwa namna ambayo inaweza kutafsiriwa kama vidonge vichungu ambavyo ni vigumu kumeza japokuwa vinatarajiwa kwamba somo kubwa kama nchi tumejifunza."

Alisema mbali na Tume kufikia hitimisho kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa, mlalamikiwa hawezi kukwepa lawama katika zoezi hilo pamoja na waajiri wengine nchini.

"Ninaona ni busara kuwakumbusha waajiri wote ikiwamo serikali kuzingatia sheria na miongozo katika mazoezi ya kuajiri watu," alisema.

Akielezea ushauri huo, Mpulla alisema kuachishwa kazi kwa mlalamikaji kulikuwa halali. Alimuru kuwa mgogoro pamoja na madai yote yametupiliwa mbali na kila upande ubebe gharama zake.

Pia alisema ndani ya wiki sita mlalamikaji kama atakuwa hajaridhishwa na hukumu iliyotolewa na Tume hiyo, anaweza kukata rufani ili kiu ya wengine wengi ambao waamini zoezi hilo halikuwa la haki na wengine kuamini lilifanyika kwa haki, wapate tafsiri yake.

"Mimi siyo Mungu nimetimiza wajibu wangu wa kutafsiri nilivyoona inafaa kwa yale mliyoyaleta kwangu, ninawashauri ndani ya wiki sita muende Mahakama Kuu ya Tanzania mkaangalie hukumu hii niliyoitoa na yenyewe iwe na ya kwake, na hata ikihukumiwa vinginevyo huko bado ninashauri muende Mahakama ya Rufani ambayo ndiyo yenye maamuzi ya mwisho," alisema.

Awali, akisoma ushahidi uliotolewa kwenye shauri hilo alisema shahidi wa kwanza katika kesi hiyo, alikiri kumtambua mlalamikaji tangu 1996 na kabla ya kuhamia kwenye mamlaka hiyo, alitokea Wizara ya Fedha.

Katika ushahidi wake, aliieleza Tume hiyo kuwa mlalamikaji alianza kazi rasmi mwaka 1997 na kufukuzwa mwezi Novemba mwaka 2018.

Shahidi wa pili, Issa alieleza kuwa anamjua malalamikaji kama mmoja wa waliokuwa waajiriwa TRA katika nafasi ya Ofisa wa Msaidizi aliyekuwa akishughulikia ulinzi wa mipaka.

CAPITAL RADIO
POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

HABARI KITAIFA

# Mil. 400/- kuboresha miundombinu Tanapa

**Na Lusungu Helela**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa ) limepangiwa kukusanya Sh. bilioni 400 kwa mwaka huu wa fedha zitakazotumiwa kuboresha miundombinu katika hifadhi nne mpya za taifa zilizopandishwa hivi karibuni katika Kanda ya Magharibi.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema hayo juzi mkoani hapa alipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Ugalla huku akiwataka wakazi wa mkoa huu wawe mstari wa mbele kiutalii.

Alisema Tanapa inachangia asilimia 15 pekee ya mapato yake kwenye mfuko wa serikali kuu na kiasi chote kinachobakia kitatumiwa kuboresha miundombinu katika hifadhi hizo.

Kutokana na mpango huo, Kanyasu amewataka wakazi wa Tabora na mikoa ya jirani wajiandae kuchangamkia fursa za utalii ili kunufaika baada ya mapori ya akiba ya Moyowosi, Kigosi na Ugalla kupandishwa hadhi na kuwa hifadhi za taifa.

Kuhusu mpango wa wizara katika ukanda huo, Kanyasu alisema wizara yake imepania kufungua kanda zote zisibaki nyuma katika masuala ya utalii badala ya kutegemea kanda ya kaskazini pekee.

"Tumeanza Kusini na sasa tupo kanda ya Magharibi. Lengo letu ni kuhakikisha kanda zote nchini zinafunguka kiutalii," alisema Kanyasu na kuongeza kuwa: "Jengeni hoteli nzuri kwa ajili ya watalii na wakulima limeni mazao pendwa kwa ajili ya watalii, hizi ndizo fursa zenyewe."

Amesema utalii ni biashara endelevu ambayo watalii wanapotembelea vivutio vilivyopo, wanahitaji usalama wa maisha yao na ukarimu.

"Utalii ni biashara isiyofilisika. Huwezi kufananisha na madini kwa vile mtalii anakuja kuzitumia fedha zake alizozihifadhi kwa muda mrefu, zikiisha anaondoka zake," alisisitiza.

Aidha, Kanyasu amewataka wazazi wawashauri vijana wao kusomea masuala ya utalii ikiwamo kozi ya kuongoza watalii badala ya kuanza kulalamika kuwa nafasi hizo zinachukuliwa na wageni kutoka kanda zingine ambako biashara ya utalii imepiga hatua.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magri, alisema kufunguliwa kwa ukanda huo kiutalii kunatuma ujumbe kwa wananchi wake kujipanga kikamilifu kuchangamkia fursa za uwekezaji wa miundombinu ya utalii kwa watu pamoja sekta binafsi ili kunufaika.

Aliongoza kuwa kwa vile Sikonge ina misitu ya hifadhi kwa asilimia 95, hivyo itawafanya wananchi wazidi kuhifadhi kutokana na kunufaika na maliasili zinazowazunguka.

# Waziri aagiza ukaguzi maeneo yaliyovamiwa

**Na Munir Shemweta,** MWANZA

HALMASHAURI zote nchini zimetakiwa kupitia upya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii kama vile makaburi, maeneo ya wazi, ujenzi wa taasisi za umma na masoko ili kujiridhisha kama bado yanafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa au yamevamiwa.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (pichani), alitoa agizo hilo jana wakati akikagua utekelezaji kupitia maeneo yaliyovamiwa katika wilaya za Ilemela na Nyamagana.

Mabula alikemea kitendo kinachofanywa na baadhi ya halmashauri nchini kutolipa fidia katika maeneo zinayoyatwaa hali inayosababisha kuzalisha migogoro isiyo ya lazima na uvamizi mpya katika maeneo hayo.

"Halmashauri zote nchini naziagiza kupitia upya maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za kijamii ili tujue maeneo hayo yamevamiwa kwa kiasi gani, tuwafanyie urasimishaji wananchi walipe kodi ya serikali. Kama eneo bado halijavamiwa basi tulilinde ili lisiendelee kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa," alisema.

Pia aliwataka wataalamu wa ardhi nchini kuacha kukaa ofisini na badala yake waende kwa wananchi ili kuepuka kuitia hasara serikali kwa kutoa taarifa zisizo na uhakika. Aliwatoa hofu wananchi wa mitaa ya Nyagungulu, Mwambani na Bukengwa yaliyoko kata ya Ilemela kuwa serikali itaendelea kutatua migogoro ya ardhi kwa kuzingatia haki, sheria na ubinadamu.

Mbunge wa Nyamagana, Stanslaus Mabula, mbali na kumpongeza Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuunda timu ya mawaziri kupitia maeneo yote yenye changamoto za ardhi, huku akiiomba Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuhakikisha ulipaji fidia kwa wananchi wenye migogoro ya ardhi unafanyika.

Naye Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Ziwa, Makwasa Biswalo, alisema ukaguzi maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za kijamii ulianza Septemba 30, mwaka huu na kumalizika Oktoba 4 kabla ya kuongezwa siku nne.

Hata hivyo, kamishna huyo msaidizi aliomba ushirikiano kutoka kwa wananchi na viongozi ili kukamilisha ukaguzi huo haraka na kwa ufanisi.

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

TANESCO

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UJENZI WA NJIA KUU YA KUSAFIRISHA UMEME YA MSONGO WA KILOVOLTI (kV) 132 TABORA - KATAVI

Oktoba 10, 2019, Mpanda - Katavi

Serikali kupitia Wizara ya Nishati na TANESCO imeanza rasmi utekelezaji wa ujenzi mradi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Tabora hadi Mpanda, Katavi umbali wa kilometa 381.

Ufikishaji wa gridi ya Taifa Mkoani Katavi utakwenda sambamba na uwekaji wa jiwe la msingi siku ya Ijumaa Oktoba 11, 2019 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kuashiria kuanza rasmi kwa utekelezaji wa mradi huu.

Gharama za mradi huu ni Shilingi Bilioni 135.3, fedha zote zinalipwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili.

Ujio wa gridi ya Taifa Mkoani Katavi utaenda utawezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika na unaotabirika kwenye Vijiji 191 vya Mkoa wa Katavi, hivyo kuongeza fursa ya wananchi kupata huduma ya umeme kwa gharama ya shilingi 27,000/= tu.

Hatua ya utekelezaji wa mradi huu inatokana na dhamira ya dhati ya Serikali kuondokana na umeme unaozalishwa kwa kutumia mafuta ambao umekuwa ukiigharimu Serikali.

Kwa miaka mingi Mkoa wa Katavi umekuwa ukitumia umeme unaozalishwa na mitambo inayotumia mafuta, matumizi hayo ya mafuta yamekuwa yakiigharimu Serikali takribani shilingi milioni 800 kwa mwezi, matarajio ni kuwa baada ya mradi kukamilika fedha hizi zitatumika katika uendelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

TANESCO inapenda kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Nishati kwa kuwezesha Mradi huu kuanza kutekelezwa na inawasihi Wananchi na Wadau wote wa maendeleo kuupokea ikiwa ni maandalizi ya ujio wa Gridi ya Taifa Mkoani Katavi.

IMETOLEWA NA: OFISI YA UHUSIANO
TANESCO MAKAO MAKUU

215454102

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Bravo kuwapumzisha wazee wa mahakama

**MAHAKAMA** ya Tanzania imesikia kilio cha muda mrefu, ambacho kimekuwa kikitolewa na baadhi ya watu wenye mashauri mahakamani dhidi ya wazee washauri wa mahakama.

Wazee hao wamekuwa wakilalamikiwa kuwa wanachangia kuchelewesha kumalizika kwa mashauri mahakamani.

Ni kweli kwamba ulikuwa uamuzi mzuri wa kuwa na wazee washauri katika mahakama zetu kwa kuwa walikuwa wanasaidia kutoa ushauri kwa majaji na mahakimu kwa kutumia uzoefu wao, busara na pia kuijua vizuri jamii wanayoishi nayo.

Kwa kuzingatia hayo, kwa muda mrefu walikuwa wakiwasaidia majaji na mahakimu kupata maoni na ushauri kabla ya wakati wa kusikiliza kesi na kuandika hukumu.

Hata hivyo, kutokana na mapungufu mbalimbali ya washauri hao ambayo yalisababisha malalamiko dhidi yao, mahakama imefanya uamuzi wa kutokuwatumia, isipokuwa katika baadhi ya kesi.

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amesema Mahakama inakusudia kupunguza kuwatumia wazee hao katika kuamua mashauri mahakamani.

Badala yake amesema itabaki ikiwatumia katika mashauri ambayo yataonekana yana ulazima wa kuwatumia.

Akizungumza wilayani Bunda mkoani Mara katika ziara ya kikazi kukagua shughuli za Mahakama, Jaji Kiongozi alisema wazee hao watatumiwa na Mahakama kwenye mashauri ambayo yatakuwa na ulazima wa kuwatumia, lakini yale ambayo siyo lazima, wataacha kutumiwa.

Jaji Kiongozi alisema baadhi ya wazee washauri wa Mahakama hujihusisha na vitendo vya rushwa na kuwatisha mwingine huwatisha mahakimu wanapokuwa wakitekeleza wajibu wao.

Alisema matumizi ya wazee washauri wa Mahakama wakati mwingine husababisha mashauri kuchelewa kumalizika kutokana na kuchelewa kwao kufika mahakamani na kusababisha mashauri kutokusikilizwa kwa wakati.

Sababu zilizotolewa na Jaji Kiongozi za kuacha kuwatumia wazee washauri ni za msingi kwa sababu bila kuchukuliwa uamuzi huo, kunaweza kuathiri shughuli za mahakama hasa kuchelewesha haki au kuwanyima haki watu wengine.

Inapofika mahali washauri hao wakajiingiza katika vitendo vya rushwa au kuwatisha mahakimu, ni dhahiri kwamba wanakuwa wamekosa sifa na uhalali wa kuishauri mahakama. Pia wadau wa mahakama na wenye kesi hawawezi kuwa na imani kwao tena.

Tunakubaliana na mahakama kwa kuchukua hatua hiyo kwa lengo la kurejesha imani ya umma kwa chombo hicho cha kutoa haki nchini.

Tunaona njia nzuri ya kuwawezesha majaji na mahakimu kupata ushauri mpana wakati wa kusikiliza mashauri, ni kufikiria uwezekano wa kuwatumia wataalamu hususan wa fani ya kesi husika.

Kwa mfano, kama kesi inahusu masuala ya ardhi, basi inaweza kuwatumia watu wenye utaalamu wa sekta hiyo, wakiwamo wastaafu. Hata hivyo jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa watu hao ni waadilifu, waaminifu na wenye weledi.


Tunashauri kuwa mahakama iendelee kuweka utaratibu mzuri wa kusikiliza malalamiko ya wananchi yanayoonekana kuathiri utoaji wa haki, na kuchukua uamuzi wa haraka baada ya kuyafanyia uchunguzi wa kina.

Tunaamini kuwa mahakama haitaishia kuwaondoa wazee washauri tu, bali watumishi wake wote ambao watabainika kujihusisha na vitendo vya ukosefu wa maadili.

Hilo likifanyika, mkakati wa chombo hicho wa kupunguza malalamiko ya rushwa dhidi yake litakuwa limefanikiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Bila ushirikiano sasa Afrika inajiua yenyewe

Na Raphaeli Kibiriti

**BIASHARA** miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), inatetereka na mambo si mazuri.

Ni masuala yanayoibuka kwenye mkutano wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), wakati wa kujadili ripoti ya Kamati ya Biashara na Uwekezaji ya EAC ya mwaka 2016.

Hapo inaelezwa kuwa thamani ya biashara miongoni mwa nchi wanachama kwa mwaka huo, ilishuka kutoka dola bilioni 3.2 mwaka 2015 hadi kufikia dola bilioni 2.6.

Moja ya sababu zinazotajwa kuchangia kushuka kwa biashara katika ripoti hiyo ni pamoja na kuendelea kuwapo kwa vikwazo visivyo vya kodi au 'none tariff barriers' (NTBs).

Aidha, kukosekana kwa mifumo inayodhibiti ufanyaji biashara na kingine ni mataifa wanachama kushindwa au kukataa kuridhia mikataba ya biashara baina yao bila sababu yoyote ya msingi.

Jambo hilo si jema kwa afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayokusudia kuwa na ushirikiano ili kufikia mtangamano.

Lakini tatizo hilo si kwa EAC pekee huenda ni Afrika nzima.

Masuala yanayohusu ushirikiano yamekuwa magumu kufikiwa kutokana na wanachama kufikiria kibinafsi zaidi.

Wakati mambo yanashindikana kuanzia biashara na maingiliano ya raia wa EAC na hata kwenye Umoja wa Afrika (AU), ni wakati wa kujikumbusha kuwa ili usikike na ushawishi wako kukubalika na wengine ni lazima uwe na nguvu. Nguvu hizo ni kiburi cha kiuchumi, umahiri wa teknolojia, uwezo wa kijeshi na mamlaka za kisiasa za kushawishi na kuyalazimisha mataifa mengine kukusikia na kukutii.

Ndiyo maana mataifa yenye msuli huo kama Marekani na China ambalo ni taifa la pili kwa uchumi mkubwa duniani yanathamini muungano, umoja na mtangamano.

Si hivyo hata Umoja wa Ulaya (EU) unasimama imara na kulinda muungano wake licha ya kuwapo na sekeseke kama vile Uingereza kujitoa. Umoja na ushirikiano ndiyo msingi mkubwa wa kuwa imara kiuchumi, teknolojia na hata kiushawishi.

Leo hii dunia inazitazama China, Marekani, India na EU kama madola yenye nguvu na ambayo yana ushawishi mkubwa mno (influence). Amerika inaposimamia jambo leo ni lazima dunia itasikiliza, aidha China inapoinuka kila taifa linasikiliza kufahamu China inasema nini.

Si hivyo tu hata India, Umoja wa Ulaya na pengine mataifa ya Amerika Kusini hasa Mexico.

Afrika isijidanganye kuwa itakuwa inaendeleza ubinafsi wa kila nchi kujifanyia inavyotaka na kukataa mtangamano na ushirikiano. Kama Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan hazitaweza kufanya biashara na kushirikiana zitawezaje kushirikiana na China, India na EU?

Kama inakuwa vigumu kuwa na umoja na ujirani ndani ya Afrika itawezekanaje kuwa na Dola la AU ambalo nalo linatakiwa kusimama kama China au India au EU kwenye kutetea mambo yake iwe kiuchumi au kisiasa?

Inabidi Afrika na pia EAC, kujikumbusha kila wakati kuwa umoja ndiyo silaha pekee ya ushindi.

Kama Marekani ina majimbo 52, Afrika nayo yenye nchi 53 inashindwaje kuwa na mtangamano kama ilivyo Marekani?

Kwanini mataifa ya Afrika yasiungane na kuwa na dola la AU ambalo ndilo litakalokuwa mwanzo wa mafanikio ya kila kitu ikiwa ni pamoja na kuondoa umaskini na uasi wa kisiasa?

Afrika Mashariki inahitaji sana kuungana na kufanya biashara na miradi ya maendeleo pamoja kwa kuunganisha nguvu, kama ilivyo China na India.

Ni wazi kuwa hakuna mafanikio kama Waafrika hawatajiunga na kuamua kufanya mambo kwa ushirika. Baadhi ya wabunge wa EALA wanasema nchi wanachama zimejawa na hofu 'isiyofahamika' ya kuogopa muungano au mtangamano.

Wanaona kuwa kuna woga uliojaa miongoni mwa wanachama wa EAC yenye nchi sita wanachama, kuwa ndio unaochangia kuua jumuiya kwa kuwa unasababisha malengo ya waasisi wa jumuiya kushindwa kufikiwa.

Ni lazima Afrika pamoja na EAC kutekeleza maamuzi wanayojiwekea wenyewe kwa ajili ya manufaa yao na watu wao kwa sababu bila mtangamano hakuna maendeleo.

Ni kitu gani kinachosababisha wanachama kuogopana na kushindwa hata kuridhia masuala na mikataba waliyokubaliana wenyewe kwa miongo kadhaa? Bila kuwa na umoja mambo yataendelea kuwa mabaya kwa Afrika na watu wake watabaki kuwa maskini, wagonjwa, wajinga na walio nyuma kimaendeleo kwa kuwa tu, viongozi wamekataa ushirikiano.

Kwa mfano, kama Tanzania haiwezi kufanya biashara na Uganda, itafanyaje uwekezaji na ushirikiano na mataifa mengine?

Ni lazima kujirekebisha na kuondoa tofauti hizi kwa kuwa China na Afrika na mataifa mengine ya Mashariki ya Mbali kama Indonesia, Malaysia na Korea yalikuwa kwenye kiwango kimoja cha kiuchumi na Afrika miaka ya 1960, lakini hao umoja na ushirikiano umewavusha, Afrika na EAC zinangoja nini?

Ni wakati wa kutekeleza hayo ambayo viongozi wa Afrika wameyaona na yamethibitisha kuwa umoja ni ushindi na ndiyo mafanikio popote duniani.

MAKALA MAALUM

## SIKU AFYA YA AKILI DUNIANI

# Namna udadisi wa azma ya mtu anayetaka kujiua unavyomwokoa

**Na Betuna Mwamboneke**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linakadiria kuwapo zaidi ya watu milioni moja wanaojikatisha uhai kila mwaka. Ni ngumu kujua kinachowafikisha hapo, lakini wao wanakuwa kwenye maumivu yanasogeza katika maamuzi hayo magumu.

Wanaotaka kujiua huwa hawaombi msaada au kusaidiwa, lakini haina maana kwamba, hawahitaji kusaidiwa. Pia, wanaojiua sio kwamba hawataki kuishi, bali wanatawaliwa na mawazo ya kutaka kuondoa maumivu, wapumzike na mateso yasiyovumilika.

Mtu anayejiua haoni njia mbadala ya kutatua tatizo alilo nalo, bali kifo tu. Wanatamani kuwapo njia nyingine mbali na kifo, lakini hawaoni. Wanafunikwa na ukungu wa msongo wa mawazo, kupoteza matumaini, kujiona hawana thamani na wanatengwa. Wanapata ugumu katika kufanikisha kukatisha maisha yao.

Ni ngumu kuelewa sababu zinazowafanya wajiue, lakini wao wanakuwa kwenye maumivu makali sana na hawaoni njia nyingine ya kutatua maumivu hayo.

**MITAZAMO YAO**

●Wengi wanaoongelea kujiua wanatishia tu, hawawezi kujiua. Mtu akidhamiria kujiua, anafanya kimya kimya.

Ukweli ni kwamba, kila mtu anayetaka kukatisha uhai wake, kuna viashiria atavionyesha. Daima usipuuze mtu anapokwambia atajiua, hata kama anaongea kwa utani.

●Yeyote anayejiua ni mgonjwa wa akili. Wengi tumekuwa tukifikiri hivyo, lakini ukweli ni kwamba, sio kila anayekatisha maisha yake ni mgonjwa wa akili. Wengine wana msongo wa mawazo na maumivu ya kihisia.

**VIASHIRIA VYAKE**

Asilimia kubwa ya wanaotaka kukatisha uhai wao huwa wanazungumzia suala hilo. Pia, wanaweza kuongea kwa utani.

Wanaandika sana vitu vinavyoashiria kutoweka kwao, kutafuta vitu vitavyowasaidia kutoweka kwao, kama vile sumu, kamba, silaha, visu, dawa za binadamu na mimea.

Hizo ni dalili mbaya sana na hasa kama mtu ana msongo wa mawazo au dalili za magonjwa ya akili, kuathirika kwa dawa ya kulevya na pombe.

Pia kama mtu huyo alikishwawahi kujaribu kujiua au kwenye familia kuna mtu aliyejiua, kwa maana ya kuwa na historia ya kujiua.

Kupoteza matumaini ni dalili mbaya sana ya mtu kukatisha uhai wake, kwa sababu mara



nyingi wanapoteza thamani kabisa ya kuishi, hawana matumaini tena ya ama kuendelea au kufanikisha matarajio yao. Mara nyingi hawaoni au hawajihisi wana cha kupoteza.

Watu wenye malengo ya kukatisha uhai, wanakuwa na mabadiliko katika ulaji chakula; kula kulikopitiliza au kutokula kabisa.

Pia, watu hao wanapoteza uwezo wa kufanya kazi zao za kila siku. Hiyo ni kwa sababu hawaoni maana tena ya kuwajibika na wanajisikia kuchoka, wakitawaliwa na huzuni.

Hisia zao zinabebwa na hulka ya kujichukia, kujiona ana hatia kwa matatizo yake, kujisikia aibu kwa jambo fulani, kujiona ni mzigo kwa wengine.

Mtu huyo anatamka maneno ya wosia baada ya kifo chake kifanyike nini, anakuwa anatembelea ndugu kwa lengo la kuwaaga, japo wengi katika tendo hilo wanaficha malengo yao. Akishajiua, ndio utasikia ndugu wakisema "kumbe alikuwa anatuaga."

Wengine huwa wanaaga kwa maneno kama 'hamtaonana tena' na wanapenda kukaa katika namna ya kujitenga.

Wapo wanaofanya mambo ya kuhatarisha maisha binafsi, kama vile kuendesha gari vibaya na kasi kubwa, kutumia vilevi kulikopitiliza na wapo wanaotumia dawa za kulevya au pombe mpaka hatua ya kufariki.

Lingine, mtu anapotawaliwa na msongo wa mawazo na kisha ghafla anatawaliwa na furaha, ni ishara ameshachukua maamuzi ya kujiua.

**UNAZUIAJE KUJUA?**

Jambo kuu la kufanya unapohisi mtu ana viashiria vya kutaka



Betuna Mwamboneke

kujua ni kuongea naye. Ni ngumu kuongelea hilo na mhusika na kama huna utaalamu. Ila kuna mambo machache yanaweza kurahisisha mazungumzo hayo.

Kwanza ni lazima uonyeshe unajali hisia zake na sio kumhukumu, huku ukimruhusu aeleze hisia zake. Namna nzuri ya kurahisisha mazungumzo ni kwa kutumia mfano huu: "Nimekuwa nikiona tofauti kwako hivi karibuni. Natamani kujua, nini kinakusumbua mpaka unakuwa hivyo?

"Kitu gani kimekutokea kinakufanya wewe kuwa hivi ulivyo?" Ninaweza kukusaidia kwa namna gani kama unaniruhusu? Siwezi kukuelewa yale unayoyapitia kwa sasa, lakini najali wewe kuniruhusu niweze kukusaidia."

**UNAVYOONGEA NAYE**

Muda wote, zungumza ukiwa unaonyesha unajali. Tenga muda wa kumsikiliza mawazo yake, daima utapata maeneo mengi ya kumsimamia kwenye hicho kitendo.

Pia usimhukumu kwa mawazo yake ya kujiua. Mwelewe kwa kile anachoona kitamsaidia zaidi. Mwongezee matumaini na lazima ulichukulie suala lake la kutaka kujiua kwa umuhimu wa juu zaidi.

Wakati unazungumza na mhusika huyo mwenye dhamira, usimhukumu kwa maamuzi yake, usionyeshe mshtuko wa taarifa hizo na daima jiweke wa kawaida.

Pia ni lazima kumhakikishia usiri wa kile mnachoongea, jambo litakalomsaidia kufunguka zaidi na unaweza kuwapatia mbadala wa suluhisho la matatizo aliyo nayo.

Muhimu ni kwamba, kama mtu amekuambia ana wazo la kujikatisha uhai, ni muhimu kujua hatari iliyoko kwa kudadisi mpango mkakati uliopo, kwa sababu mtu mwenye mipango anakuwa kwenye hatari zaidi.

Muulize kama kuna kitu chochote ameandaa kwa ajili ya kutekeleza azma yake, mfano kisu, kamba, sumu, vidonge ya dawa na silaha. Muulize muda aliyopanga kutekeleza, kwani itakusaidia kumpeleka kwa wataalamu wa saikolojia haraka iwezekanavyo.

Aidha, anashauriwa kutoa vitu vyote vinavyoweza kumsaidia kujikatisha uhai.

**HISIA ZAO**

Kwa uzoefu wa kazi yangu ya kutoa ushauri wa kisaikolojia, nimekutana na mikasa mingi ya ama waliojaribu kujiua na wenye mawazo ya kujiua.

Wamekuwa wakitoa kauli mbalimbali zinazotafsiri hisia zao, baadhi yake ni zifuatazo: Najiona mtupu sana, sioni cha kufanya kurekebisha makosa yangu; sidhani kama naweza kurekebisha haya, bora nife; thamani yangu haipo tena, sioni maana ya kuishi; mwili wangu umekufa ganzi, nikifa nitapumzika; matatizo yangu ni makubwa sana, hakuna atakayeweza kuyatatua; na zilikuwa hasira tu.

Msisitizo nauweka kwamba kumuuliza mtu kuhusu kujiua, iwapo umemhisi kunaokoa maisha. Wanaoujiua si kwamba hawajui thamani ya maisha.

***Soma zaidi kuhusu afya ya akili Uk. 14**

**● Mwandishi ni mtaalamu wa saikolojia katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.**

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Uandikishaji wapigakura wasuasua

INATOKA UK. 3

"Niwaombe sana ndugu zangu tukajiandikishe kwa wingi tuchague viongozi wetu ambao watatusaidia viongozi wa juu, ngazi ya chini kusukuma gurudumu la maendeleo kwa Watanzania."

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Binilith Mahenge, alisema mkoa huo kwa makadirio ya mwaka 2017 una watu milioni 2.3 na matarajio ni kuandikisha na kupiga kura watu 900,000.

"Tuna vituo 3,979 na Mkoa wa Dodoma katika zoezi hili jana (juzi) tumeandikia watu 156,334, wanaume 82,114 na wanawake 74,220," alisema.

Alisema kwa mwenendo huo inawezekana kuvuka malengo ya uandikishaji kwa kuwa kasi ya uhamasishaji imefanyika kubwa kwa wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhamasisha.

**UANDIKISHAJI MOROGORO**

Mkoa huo unatarajia kuandikisha idadi ya wapigakura 1,423,111, watu 203,553 wameshaandikishwa tangu uandikishaji ulipoanza juzi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya uchaguzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alisema kuwa mkoa huo una wakazi 2,537,955 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 na idadi inayotarajiwa kuandikishwa ni sawa na asilimia 56 ya wakazi wote, kati yao wanaume ni 684,671 na wanawake 738,440.

Alisema wenyeviti wa mitaa 327 wanatarajiwa kuchaguliwa, wenyeviti wa vijiji 671, wenyeviti wa vitongoji 3,380 pamoja na wajumbe wa halmashauri ya kijiji, kundi mchanganyiko na wajumbe kundi la wanawake ambao si chini ya theluthi moja ya wajumbe wote.

Pia alisema katika uchaguzi wa Mamlaka za Miji nafasi zitakazogombewa katika ngazi ya mtaa ni mwenyekiti wa mtaa na wajumbe watano, ambao kati yao wawili watakuwa wanawake na uchaguzi huo utahusisha mitaa 294 ya Manispaa ya Morogoro na mitaa 33 ya mji wa Ifakara, wilayani Kilombero.

Katika Mamlaka ya miji midogo nafasi zinazogombewa ni mwenyekiti wa kitongoji katika mji mdogo wa Mikumi, Kilosa pamoja na Gairo.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Sheila Lukuba, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwa muda uliopangwa ili waweze kupata haki yao ya kidemokrasia ya kuwachagua viongozi wanaowataka kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

**RC MTWARA ATOA ANGALI ZO**

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, Selemani Mzee, amesema ujiandikishaji katika daftari la mpigakura hauhusiani na utoaji wa kero za wananchi kwenye vituo vya kujiandikisha.

Alisema hakuna uhusiano wowote kati ya kujiandikisha na kutoa kero kwenye mitaa na kata.

Mzee alisema kuna baadhi ya wananchi au viongozi wanatumia fursa hiyo ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpigakura kutaka kuacha kujiandikisha kwa kisingizio cha uwepo wa kero kwenye maeneo.

Alisema kipindi hiki ni cha kujiandikisha katika daftari la mpigakura na sio kutumia fursa ya kueleza kero zilizopo kwenye mitaa.

**DAR BADO WASUASUA**

Katika jiji la Dar es Salaam kwa siku mbili mfululizo, bado wananchi wameendelea kusuasua kujiandikisha.

Sababu zilizoelezwa na baadhi ya viongozi wa mitaa mbalimbali ya jiji hilo ni mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha watu wengi kushindwa kujitokeza.

Katika maeneo mengi vituo vilionekana kuwa wazi huku wananchi wakijitokeza mmoja mmoja.

INAENDELEA UK. 26

# Ushirikina kikwazo mapambano fistula

INATOKA UK. 3

hawa wanawake maeneo wanakoishi, tunapata changamoto ya kuwapa elimu kuhusu ugonjwa huu. Tunaambia unasababishwa na nini ili waondokane na dhana ya kuamini wamelogwa. Wanapotuelewa ndipo wanakuja hospitali kutibiwa na wasipoelewa wanaahidi kuja na hawaji," alisema Mullinga.

Alisema changamoto nyingine wanayokabiliana nayo ni wanawake kubanwa na shughuli za kuhudumia familia na kilimo kunakowafanya washindwe kuwahi hospitalini kupata matibabu.

"Wanachelewa kuja hospitalini licha ya kuwa tunawagharamia kila kitu, kuanzia chakula, usafiri na matibabu na sababu kubwa kubanwa na shughuli za kilimo ndiyo maana wakati wa msimu wa kilimo na mavuno wagonjwa wanapungua wodini," alisema.

Wakati ambao si wa mavuno au kulimo wagonjwa wananaokuwa hospitalini wanafika 70, lakini wakati wa msimu huo wanakuwa kuanzia 25 hadi 35.

Kuhusu chanzo za magonjwa hayo, alisema kwa sehemu kubwa husababishwa na wanawake kuendelea kujifungulia kwa wakunga wa jadi hasa mikoa ya pembezoni kama Kigoma, Katavi, Kagera na Zanzibar, hivyo kukosa huduma muhimu za kitaalamu.

Alisema pia wagonjwa wengine ni watoto chini ya miaka 18 waliozaa katika umri mdogo ambao viungo havijakoo hivyo kupata matatizo wakati wa kujifungua.

Mullinga alisema pia wako wagonjwa ambao wanapata matundu mawili lakini matatizo yote yanatibiwa katika hospitali hiyo ndani ya siku 14.

Alitumia fursa hiyo kuishauri serikali kuwekeza kutoa elimu kuanzia ngazi ya shuleni ili kuijengea jamii uelewa kuwahi kupata matibabu ya tatizo hilo.

Mwalimu wa Kwaya ya Gethsemane, Stellah Mwalongoza, alisema wamekabidhi misaada yenye thamani ya Sh. milioni 2.5 kama sehemu ya kusaidia jamii yenye uhitaji.

"Leo (jana) tumekabidhi mafuta, dawa za meno na sabuni za kuogea ambazo zitawasaidia wagonjwa hawa ambao kwa sehemu kubwa wanahitaji faraja zaidi kutoka kwetu. Lakini tutashiriki nao ibada na kuwaburudisha kwa nyimbo nzuri tunazoimba kwaya yetu," alisema Mwalongoza.

Enabel

**Enabel – SAKIRP - Vacancy**

**Gender and microfinance specialist - Kigoma region**

Enabel – the Belgian Development Agency is recruiting a gender and microfinance specialist for its Sustainable Agriculture Kigoma Regional Project.

**Duty station:** Kigoma region – based at Kasulu Town with occasional travel to other districts

**Contract term:** I year extendable - competitive salary package.

**Profile:** minimum of degree in business studies, microfinance, agricultural economics, sociology or related area

**Experience:** minimum of one year hands-on in microfinance and promoting women economic inclusion. Computer literate and good reporting skills in English/ Kiswahili.

**Details vacancy at:**
**https://btctanzania.wordpress.com/**

**Submit your applications to:**
**recruitment.tza@enabel.be**

**Deadline: all applications should be submitted by 31 October 2019.**

**Only shortlisted candidates will be contacted.**

215455202

# Dar kinara kwa magonjwa ya akili

INATOKA UK. 2

mikoa mingine inafuata, Dar es Salaam ina asilimia 20, Kilimanjaro 9, na mingine asilimia 7 hadi 5. Mikoa yenye wagonjwa kidogo ni Katavi 0.1, Rukwa 4, Songwe pia ina asilimia chache ya wagonjwa," alisema.

Hata hivyo, alisema hali za kimazingira na vilevi ndizo zinazochangia zaidi kuliko viashiria vya kibaiolojia kwenye maeneo ya mijini kuliko vijijini.

"Kuna vihatarishi vinavyosababisha magonjwa ya akili ambapo kikubwa namba moja ni vinasaba, vitu vya kibaiolojia kuna kupata majeraha ambayo yanaathiri ubongo, baadhi ya magonjwa yanayopanda kichwani ikiwamo malaria, HIV."

"Pia matumizi ya vilevi kama pombe, bangi, sigara na vilevi vingine kwa kuwa vilevi kazi yake kubwa ni kushusha uwezo wa ubongo kufanya kazi na mambo yaliyokuwa yakitarajiwa," alisema.

Mtaalamu huyo alisema: "Utakuta vilevi vingi vinaweza kuwa vihatarishi, unaweza ukatumia bangi ukaumwa, pia hali ya kijamii yaani ya kiuchumi ikiwamo ugumu wa maisha yaani kuwa na hali ngumu kupita kiasi ambayo mtu hawezi kuimudu kama kufiwa mtu akashindwa kustahimilivu maumivu ya kupoteza kitu anachokipenda kama kazi, mwenza, rafiki au ndugu."

Alieleza wakati mwingine pia kuwapo katika mazingira ya ukatili, ajali kubwa kwa mfano ajali ya moto Morogoro kuna baadhi ya watu hawakuathirika na moto, lakini walishuhudia yale yaliyotokea kwa hiyo hao wanaweza kuathirika kiakili.

Kuhusu watoto wadogo, alisema kwa watoto wadogo kinachochangia kwa kiasi kikubwa kushinda sehemu nyingine zote ni vitendo vya ukatili wa aina zote.

"Kadhalika, kuugua magonjwa mengine kama saratani au ugonjwa mwingine wowote mkubwa unaweza kuwa kihatarishi cha kupata magonjwa hayo.

"Lakini kuishi na mtu anayetumia vilevi kupindukia, au matatizo ya akili ambayo yamekosa kabisa huduma inaweza kusababisha mtu kuwa kwenye mazingira magumu ambayo yanaweza kumpeleka kwenye vihatarishi," alisema.

Utafiti uliofanyika

Dk. Ububuyu alisema baadhi ya utafiti uliofanyika ukiwamo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ambao ulifanyika kujua ukubwa wa tatizo na Tanzania ilijumuishwa, na kuonyesha takribani asilimia moja ya watu wana matatizo makubwa ya magonjwa ya akili kupita kiasi.

HABARI KITAIFA

# Chanjo ya mifugo sasa lazima

Na Mary Geofrey

CHANJO kwa mifugo sasa ni lazima na siyo hiari, baada ya serikali kuboresha mwongozo wa matumizi na udhibiti wa dawa za majosho wa mwaka 2019 kwa lengo la kudhibiti magonjwa yatokayo na wanyama kwenda kwa binadamu.

Katika kutekeleza hilo, tayari serikali imeshanunua lita 11,000 za dawa za kudhibiti magonjwa yatokanayo na wanyama kwa lengo la kuongeza ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo.

Hayo yalielezwa jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akifungua mdahalo wa vyakula vya asili ya wanyama na mchango wake katika masuala ya afya ya umma na lishe katika kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani mwaka huu.

Katika mdahalo huo, uliohusisha wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba Muhimbili (Muhas), pia alizindua mikakati ya kitaifa ya kuzuia na kudhibiti magonjwa ya brusela na kimeta kwa binadamu na wanyama.

"Chanjo sasa ni lazima siyo hiari, kila mfugaji ana wajibu wa kutoa chanjo kwa mifugo yake ili kupunguza magonjwa na ambao hawatafanya hivyo, atawajibishwa kwa mujibu wa sheria na adhabu ni kutumikia kifungo, kulipa faini au yote mawili," Ulega alisema.

"Ina maana kama jamii itatumia nyama, mayai na maziwa kama inavyotakiwa, itakuwa na afya njema, hivyo kuipunguzia Wizara ya Afya mzigo wa bajeti wa Sh. bilioni 200 inayotengewa kwa mwaka kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba kwa ajili ya wagonjwa," Ulega alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani (FAO) nchini, Fred Kafeero, alisema wameendelea kujenga uwezo wa utayari wa kukabiliana na kuitikia milipuko ya magonjwa kwa kutumia utaratibu wa afya moja.

Alisema unawapatia watu protini ambayo ni sehemu muhimu katika chakula kwa sababu asilimia 50 ya idadi ya watu wanategemea wanyama moja kwa moja kama chanzo cha chakula chao na kiwango kingine kikubwa pia hutegemea hivyo ingawa siyo moja kwa moja.

"Uzalishaji wa tija kwa mazao ya mifugo ni suala muhimu linalohusu maisha ya watu. Kwa miaka mingi FAO imekuwa ikijihusisha na uimarishaji wa uwezo wa kitaifa wa kuzuia, kugundua na kudhibiti magonjwa ya wanyama nchini," Kafeero alisema.




Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Happiness Mgalula, akifungua mkutano wa jukwaa la wakurugenzi wa asasi za kiraia, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Matumizi ya nishati mbadala yahimizwa

Na Gwamaka Alipipi

WATANZANIA wametakiwa kutumia nishati mbadala katika maisha ya kila siku kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwani uharibifu wa mazingira unaofanywa na shughuli za kibinadamu husababisha serikali kutumia fedha nyingi kuzuia majanga.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa tatu uliohusu mabadiliko ya tabianchi ulioandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Kigoda cha Mwalimu Nyerere cha Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Simbachawene alisema Watanzania wanapaswa kuwekeza katika utunzaji wa mazingira kwa kutumia nishati mbadala kama gesi katika kupikia, matumizi ya magari rafiki kwa mazingira na kutokukata miti.

Alisema uchafuzi wa mazingira unaofanywa na binadamu huleta athari nyingi ikiwamo ongezeko la joto hali linayohatarisha maisha ya viumbe hai walioko baharini.

"Kwa sasa ongezeko la joto duniani limeongezeka kwa wastani wa nyuzi joto 1.5, wito wangu kwa Watanzania tutunze mazingira, vyanzo vya maji vitunzwe," alisema Simbachawene.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willium Olenasha, alisema matumizi ya utafiti unaotolewa na wataalamu unaisaidia serikali kutatua matatizo yanayoikuta jamii na si kweli kwamba huishia katika makabati.

Naye Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere cha Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Prof. Pius Yanda, alisema mkutano huo uliowakutanisha wanasayansi kutoka Afrika na Ulaya, umejikita katika kuainisha namna matokeo ya utafiti yanavyoweza kusaidia katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi katika fukwe za bahari.

"Wanasayansi kutoka nchi za ulaya wapo hapa ambapo wataweza kuwasilisha taarifa za kisera ambazo zitaweza kusaidia kutatua changamoto cha kutatua mabadiliko ya tabianchi katika fukwe za bahari," alisema Prof. Yanda.

## TTCL yafanya mapinduzi kwenye bidhaa zake

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation), limezindua maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Mteja huku likisisitiza kuleta mapinduzi makubwa kwenye utoaji huduma na ubunifu wa bidhaa zake.

Akizindua maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Balozi mteule Mohamed Mtonga, alisema shirika litaendelea kufanya mapinduzi makubwa eneo la utoaji huduma pamoja na ubunifu katika bidhaa zake ili kuhimili ushindani uliopo sokoni.

Alisema ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mwaka unaoishia Desemba 2018, ilibaini kuwa TTCL ni shirika la huduma za mawasiliano linalokua kwa kasi, huku likiongoza kwa idadi ya ongezeko la wateja na hata huduma ya T Pesa nayo ikitajwa miongoni mwa huduma zinazostawi kwa kasi kubwa.

"Hadi sasa, tumeweza kuwafikia asilimia mbili ya wateja wa huduma za simu nchini, yaani wateja zaidi ya milioni mbili huku huduma ya T Pesa ikifikisha wateja zaidi ya 400,000, mawakala 14,000 na miamala ya takribani Sh. bilioni tano," alisema.

Alisema katika kuwajali zaidi wateja wake kihuduma TTCL imezindua rasmi huduma ya TTCL 'App' na namba maalum ya 'WhatApp' ya huduma kwa wateja kuboresha zaidi huduma zake.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Waziri Kindamba, alisema wanawapatia wateja wao huduma mpya na mwaka huu itaenda sambamba na utoaji wa zawadi kemkem za kuonyesha shukrani kwa wateja wao.

"Mwaka huu 2019, tunawaletea huduma ya TTCL 'App' itakayowawezesha wateja wa TTCL kujiunga na vifurushi, kuongeza salio na kupata salio la akaunti yake kupitia simu za mkononi na 'tablets'."

# 'Watoto wenye matatizo moyo wapelekwe JKCI'

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI nchini wameshauriwa kuwapeleka watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) mapema iwezekanavyo baada ya kuwagundua na matatizo hayo ili waweze kupata matibabu kwa wakati.

Wito huo ulitolewa hivi karibuni na daktari bingwa wa magonjwa ya moyo kwa watoto JKCI, Naiz Majani, wakati akizungumzia kuhusu kambi ya matibabu ya magonjwa ya moyo ya kuzaliwa kwa watoto ambayo ni matundu na mishipa ya damu ya moyo iliyomalizika mwishoni mwa wiki katika taasisi hiyo.

Dk. Naiz ambaye ni msimamizi wa kambi za matibabu ya moyo zinazofanyika katika taasisi hiyo, alizitaja dalili za mtoto mwenye magonjwa ya moyo kuwa ni pamoja na kutokwa na jasho kwa wingi wakati wa kunyonya, kutoongezeka uzito, kupata nimonia, kikohozi cha mara kwa mara, kushindwa kucheza, kuvimba miguu na kubadilika rangi kwenye midomo na kucha kuwa rangi ya bluu.

"Ninawaomba madaktari wanapoona dalili kama hizi kwa mtoto wawalete katika taasisi yetu kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi zaidi kwani kuna baadhi ya matatizo ya moyo ya kuzaliwa nayo mtoto hatakiwi kuzidi umri wa miezi sita hadi mwaka mmoja bila ya kupata matibabu. Mtoto mwenye matatizo hayo akichelewa kupata matibabu akiwa na umri huo hawezi kufanyiwa upasuaji tena," alisisitiza Dk. Naiz.

"Katika kambi ya matibabu ya pamoja tuliyoyafanya na wenzetu wa Shirika la Mending Kids International lenye wataalamu wa afya kutoka nchini Italia na Marekani, watoto wanne walishindwa kufanyiwa upasuaji kutokana na umri wao kuwa mkubwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu hivyo wataendelea na matibabu ya kawaida," alisema Dk. Naiz.



Vijana wakiokota chupa za plastiki kwa ajili ya kwenda kuziuza ili wajipatie riziki, kwenye rundo la takataka zilizokusanywa na mvua katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upigaji fedha elimu bure wabainika

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga, inafanya uchunguzi wa Sh. milioni 195.7 ambazo hutolewa shuleni kwa ajili ya elimu bure, ambazo zimedaiwa kutumika kwenye matumizi mengine yasiyokusudiwa.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Husseni Mussa, wakati akitoa taarifa juu ya utendaji wake kazi kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Alisema kwa kipindi hicho cha miezi mitatu wamefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo 33 yenye thamani ya Sh. milioni 465, na kubaini kuwapo na dosari kwenye miradi hiyo, zikiwamo fedha za elimu bure Sh. milioni 195.7 kutumika tofauti na matumizi yaliyokusudiwa.

"Takukuru kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu, tumefanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 33 yenye thamani ya Sh. milioni 465, ambapo miradi ya maji Sh. milioni 55, barabara Sh. milioni 214.1, na elimu Sh. milioni 195.7 ambapo tumebaini kuna dosari," alisema Mussa.

"Kwa upande wa fedha za elimu bure tulifanya uchunguzi katika shule 30 kwa mkoa mzima wa Shinyanga, ili kujiridhisha kama kweli fedha hizo zinatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa ikiwamo kununua vifaa vya shule, na kubaini kiasi cha Sh. milioni 195.7 zimetumika kwa matumizi mengine," alieleza.

Aidha, alisema Takukuru bado inaendelea na uchunguzi juu kuwapo na dosari kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo 33, zikiwamo na fedha hizo za elimu bure, ambapo uchunguzi ukikamilika, wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Katika hatua nyingine, Mussa alitoa tahadhari kwa wagombea katika uchaguzi wa mwaka huu wa serikali za mitaa, kuwa makini kujiepusha na mienendo ya rushwa ili kuepukana na mkono wa dola, na kusema taasisi yake imejipanga vyema kukabiliana na vitendo hivyo.

# Kasike: Simamieni wafungwa kutatua uhaba makazi askari

**Na Mwandishi wetu,** SONGWE

KAMISHNA Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike, amewataka wakuu wa magereza Tanzania Bara kuhakikisha wanatekeleza ipasavyo agizo la Rais John Magufuli kuhusu ujenzi wa nyumba za makazi ya askari wa jeshi hilo nchini kwa kutumia nguvu kazi ya wafungwa waliopo magerezani.

Akizungumza mkoani Songwe baada ya kukagua miradi ya ufyatuaji wa matofali ya kuchoma na ujenzi wa nyumba za maofisa na askari katika Magereza ya Ileje, Mbozi, Ngwala na Kambi ya Mkwajuni, Kasike alisema ujenzi wa makazi ya askari unaoendelea katika vituo mbalimbali nchini ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli katika kutatua changamoto ya makazi kwa watumishi wa jeshi hilo. "Mkakati wa utatuaji wa changamoto ya uhaba wa nyumba za maofisa na askari lazima utiliwe mkazo na kupewa kipaumbele katika kuwatumia wafungwa waliopo magerezani katika suala la ujenzi sambamba na uzalishaji wa chakula cha kutosha ili kuipunguzia serikali gharama za kuwahudumia wahalifu wote walipo magerezani," alisema Kasike.

Katika hatua nyingine, Kasike aliupongeza uongozi wa Wilaya ya Songwe kwa kuanzisha ujenzi wa gereza jipya katika mji wa Mkwajuni ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Songwe.

Alisema uwapo wa gereza hilo katika Wilaya ya Songwe utasaidia katika kumaliza tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu kwenye Gereza la Wilaya ya Mbozi.

"Kutokuwapo kwa magereza ya wilaya kunasababisha msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza ya jirani, pamoja na kuchelewesha upatikanaji wa haki, hivyo nimpongeze sana Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samwel Opulukwa na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kwa kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa gereza. Kimsingi, utatatua tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Gereza la Mbozi," alisema.

Naye Opulukwa alishukuru ujio wa Kamishna Jenerali katika ziara yake ya kikazi katika Gereza la Ngwala pamoja na Kambi ya Mkwajuni ili kujionea hali halisi ya uendeshaji wa jeshi hilo, wilayani Songwe.

**HABARI ARUSHA**

# Suluhisho la ongezeko la watu Ngorongoro latajwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

BARAZA la Wafugaji Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha limesema suluhisho pekee la ongezeko la watu ndani ya Tarafa ya Ngorongoro iliyopo ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ni kuimarisha huduma za jamii ndani ya mamlaka hiyo ikiwamo kutoa ufadhili wa watoto wenyeji kujenga makazi ya kudumu nje ya eneo hilo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Edward Maura, jijini hapa wakati alipokutana na waandishi wa habari.

Alisema janga la ongezeko la watu na mifugo ni la nchi nzima kwa sasa na sio ndani ya NCAA pekee kama inavyodaiwa na baadhi ya watu.

Maura ambaye ni Diwani wa Kata ya Enokanoka, alisema kuondoa wafugaji ndani ya hifadhi hiyo sio suluhisho la kudumu la kuondoa changamoto zilizopo.

Alisema uamuzi huo utaua mifugo yote ya wafugaji na kuzuia eneo la mapito ya wanyama wanaotoka na kurudi kutoka Masai Mara nchini Kenya na kuja nchini na jamii hiyo itaishi katika umaskini mkubwa.

Pia alisema ili kupunguza idadi ya mifugo baraza linashauri maeneo yote ya hifadhi yaliyovamiwa yarudishwe pamoja na kuwaondoa wahamiaji.

Maura, alisema kuchukua kilometa za mraba 1,500 katika tarafa ya Loliondo na kuleta katika eneo la mamlaka ya hifadhi ni kuleta mgogoro na wafugaji bila sababu za msingi na pili ni kupunguza mapato kwa Halmashauri ya Ngorongoro.

Alisema awali NCAA ilikuwa na watu 8,000, lakini kwa sasa kuna zaidi ya 93,000 ikiwamo ongezeko la mifugo na watu na walimwomba Rais Dk. John Magufuli na serikali yake kukaa meza moja na baraza hilo kutatua changamoto zilizopo kwa maslahi ya pande zote.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafugaji, Shutuk Kitamwas, alisema elimu ni muhimu katika kutatua changamoto za ongezeko la watu na mifugo katika Tarafa ya Ngorongoro kutokana na uelewa mdogo wa jamii iliyopo katika tarafa hiyo.

Kitamwas aliutaka uongozi wa NCAA kuacha kutoa matamko yenye kuonyesha kuingilia kazi inayofanywa na Tume iliyoundwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala kuhusu mgogoro kati ya wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi.

Aliomba Tume hiyo kufanya kazi yake kwa umakini na uangalizi mkubwa bila kuharakishwa au kushurutishwa na mtu au kikundi chochote kwa maslahi ya pande zote.

"Nasema hivi sababu kuna dalili za baadhi ya viongozi kuingilia Tume hii kazi wakati haijamaliza kazi yake," alisema.

Katibu wa Baraza la Wafugaji, Johannes Tiamasi, alisema Rais Magufuli ni kiongozi mwenye kuwaletea maendeleo wananchi wote bila ya kubagua hivyo katika suala la wafugaji katika Tarafa ya Ngorongoro huenda akalichukua kwa uzito mkubwa kwa kujua kuwa wananchi wa eneo hilo ni wa hali ya chini na wanapaswa kusaidiwa.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti (kulia), akimsikiliza Diwani wa Kata ya Oljoro Namba 5, wilayani Simanjiro, Loishiye Lesakwi, katika mkutano ambao alikuwa akijibu maswali mbalimbali ya wananchi wa kata hiyo, jana.

# Gambo azindua uandikishaji wapigakura

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amezindua rasmi ujindikishaji wa wapigakura, uchaguzi wa serikali za mtaa na kuwataka wakuu wa wilaya zote katika mkoa huo kuhakikisha wanahamasisha wananchi kujiandikisha.

Akizindua uandikishaji huo jana katika Kata ya Muriet, jijini Arusha, baada ya kujiandikisha katika kituo cha Shule ya Msingi Kisimani, Gambo alisema uandikishaji umekosa mwitikio wa wananchi, hivyo wakuu wa wilaya wanapaswa kufanya mikutano ya hadhara ili kuhamasisha wananchi bila kubagua vyama vya siasa waweze kujitokeza kujiandikisha.

Aliwahakikishia wananchi hao ulinzi na usalama wakati wa kupiga kura na kuwataka wasimamizi wa vituo vya kujiandikishia kutowahoji wanatokea vyama gani vya siasa kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kosa na wanapaswa kuchukuliwa hatua.

Awali Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema kuwa mkoa huo unatarajia kuandikisha wapigakura wa serikali za mtaa wapatao 1,099,289 kutoka katika wilaya zote za mkoa wa Arusha, huku Jiji likitarajia kuandikisha wapigakura 328,000.

Alisema Mkoa wa Arusha una jumla ya vijiji 390, vitongoji 1505 na mitaa 154 katika Jiji la Arusha na katika Halmashauri ya Arusha kuna wapigakura 200,002, Karatu 144,000, Meru 100,000, Monduli 110,000, Longido 63,252 na Ngorongoro 148,815.

Kwa upande wake Msimamizi Mkuu wa uchaguzi katika Jiji la Arusha, Msena Binna alisema, wanatarajia kuandikisha wapigakura wapatao 328,605 katika vituo 154 katika jiji hilo, huku katika Kata ya Muriet, wakitarajia kuandikisha wapigakura 17,300.

Naye msimamizi msaidizi katika kituo cha uandikishaji cha Shule ya Msingi Kisimani Kata ya Muriet, Amani Ngatuli, alisema uandikishaji umekuwa na mwamko mdogo kutokana na idadi ndogo ya watu kujitokeza.

Aliongeza kuwa hadi kufikia jana mchana walikuwa wameandikisha wapigakura wapatao 48 pekee hatua ambayo ameomba hamasa iendelee kutolewa.

Uandikishaji unatarajia kufikia ukomo Oktoba 14, huku kampeni zikitarajia kuanza Oktoba 22, na uchaguzi wa serikali za mtaa ukitarajiwa kufanyika Novemba 14, mwaka huu.

# Mnyeti awashukia wanaowagawa wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amewaonya baadhi ya wanasiasa wilayani Simanjiro wanaowagawa wananchi kwenye makundi ya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa tiketi ya CCM ili wapate nafasi ya kuchaguliwa katika ubunge mwakani.

Alitoa onyo hilo juzi katika Kijiji cha Narakauo Kata ya Loiborsiret, akiwa kwenye siku ya kwanza ya ziara yake ya siku tano wilayani Simanjiro.

"Mwisho wa wanasiasa uchwara wa Wilaya ya Simanjiro wanaotumia nafasi ya makundi na kugawa wananchi ili wapite katikati yao na kupata ubunge imefika mwishoni," alisema Mnyeti.

Alisema anataka kuona Simanjiro mpya moja yenye wananchi wenye kutaka maendeleo na siyo kugawa na baadhi ya wanasiasa uchwara wanaogawa wananchi kwa maslahi yao ya kutaka kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Alisema yeye ni mjumbe wa kamati ya siasa ya mkoa ndiyo sababu wakafuta mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa ndani ya CCM wilayani Simanjiro na kuagiza uanze upya kwa lengo la kuondokana na ubabaishaji.

"Wananchi wa Wilaya ya Simanjiro hivi sasa wanataka maendeleo hawahitaji tena siasa uchwara zisizo na mwelekeo wenye manufaa kwao kwa kutumia nafasi ya uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema Mnyeti.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula, aliwataka wananchi wa eneo hilo kutowachagua viongozi wanaojihusisha na uuzaji wa ardhi ili kuepusha migogoro ya ardhi.

Mhandisi Chaula, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kutumia nafasi hiyo vizuri ya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwaondoa madalali wa kuuza ardhi na kuondokana na migogoro ya ardhi.

"Mkitumia makosa kwa kuchagua madalali wa ardhi baadaye msije ofisini kwangu kunisumbua kwani mtakuwa mmewachagua wenyewe na vijana wa sasa wanasema itakula kwenu," alisema Mhandisi Chaula.

## Takukuru yaonya wagombea kujitoa

**Na Paul William,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kilimanjaro, imesema itachukua hatua kali dhidi ya wagombea watakaojitoa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji baada ya kuchukua za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Uchaguzi huo wa vijiji, mitaa na vitongoji unatarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu nchini kote.

Taarifa ya Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Hole Makingu, iliyotolewa juzi ilisema watakaothubutu kujitoa kabla ya mchakato wa uchaguzi kukamilika, watachunguzwa kwa kuwa hiyo ni dalili mojawapo ya kuashiria vitendo vya rushwa.

Alisema wako baadhi ya wagombea ambao huchukua fomu kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, lakini hujitoa kabla ya mchakato wa uchaguzi baada ya kuahidiwa fedha au kuchukua fedha ili kumpa mshindani nafasi ya kushinda.

Makingu alisema kitendo hicho ni dalili kuwa mgombea huyo amepewa fedha za rushwa ili kujitoa kwa maslahi mapana ya mgombea wa pili na kudai kuwa kwa sasa Takukuru itapambana na wagombea watakaofanya hivyo. "Inakuwaje mtu anachukua fomu ya kugombea nafasi ya uongozi kupitia chama fulani halafu anakuja kujitoa kabla ya mchakato wa uchaguzi ili mwingine apite bila kupingwa. Kama hajapewa rushwa ni nini? Hatutakubali kuona kitendo hiki na tutapambana na wagombea hao," alisema Makingu.

Alisema matendo mengine yanayoweza kuhesabika kuwa ni makosa ya rushwa wakati wa uchaguzi ni mpigakura kushindwa kujiandikisha katika daftari la mpigakura kutokana na kuhongwa na hivyo kupoteza haki yake ya kushiriki kwenye uchaguzi.

Makingu alisema kuwa wapo baadhi ya wagombea wamekuwa wakitumia fedha kuandaa kundi au watu wa kufanya vurugu kwenye mikutano ya kampeni ili mgombea mwingine asipate fursa ya kujinadi kwa wapiga kura na wananchi kwa ujumla nao watachukulia hatua kwani ni njia moja wapo ya rushwa.

Aidha, Mkuu huyo wa Takukuru aliwataka wananchi kuwafichua wale wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi pamoja na kuwa tayari kutoa ushahidi katika kesi mbalimbali zinazochunguzwa na Takukuru ili kuunga mkono jitihada za mapambano dhidi ya rushwa nchini.

# Mkandarasi umeme akalia kuti kavu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPUNI ya Rural & Urban Engineering Services Ltd iliyopewa kazi ya kusambaza umeme katika vijiji 83 vya mkoa wa Kilimanjaro, sasa ni kama amekalia kuti kavu baada ya serikali kutangaza kuiwekea uangalizi maalum kwa siku 21.

Jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi ya Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Styden Rwebangila, alisema katika kipindi hicho cha uangalizi, mkandarasi huyo anatakiwa kufanya kazi zote zilizokuwa zimesimama ikiwamo kusimika nguzo, kuvuta nyaya na kuunganisha umeme kwa wananchi.

Alitangaza juzi uamuzi huo baada ya kamati hiyo kufanya kikao cha pamoja na mkandarasi ambako alipewa fursa ya kujieleza ni kwa nini ameshindwa kutekeleza kwa kiwango cha kuridhisha mradi huo kwa mujibu wa mkataba. "Kwa mwenendo huu, tumeona hatuwezi kufika kama tulivyodhamiria, yaani kukamilisha mradi ifikapo Desemba 31, mwaka huu. Sasa tumemweleza huu ni mradi wa kipaumbele wa serikali, hivyo aupe umuhimu unaostahili maana inaonekana yeye hajaupa kipaumbele," alisema.

Rwebangila alisema kasi ya mkandarasi huyo katika kutekeleza mradi huo ni ndogo na amefikia asilimia 44 tu ya utekelezaji badala ya asilimia 62 aliyopaswa kuwa amefikia.

Alisema baada ya kuzungumza na watendaji mbalimbali wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) ambao ndio wanamsimamia mkandarasi huyo, walibaini changamoto kadhaa ikiwamo kutokuwapo kwa wafanyakazi katika maeneo ya kazi, hususani meneja na msimamizi, jambo ambalo limekuwa likiwapa Tanesco wakati mgumu katika usimamizi.

Mhandisi Rwebangila alisema kamati yake haikuridhishwa na mpango kazi uliowasilishwa na mkandarasi, hivyo inampa siku saba akae na watendaji wa Tanesco wanaomsimamia ili wabainishe vipaumbele na kuwasilisha tena ndani ya muda huo.

Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka REA, Mhandisi Jones Olotu, ameeleza kampuni hiyo ni miongoni mwa makandarasi ambao hawafanyi vizuri katika utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu ya REA (REA III) nchini.

Alisema kuwa hadi sasa mkandarasi huyo ameunganisha umeme vijiji 16 tu kati ya 77 ambavyo mradi wa REA III awamu ya kwanza umelenga kuvifikia. Mkandarasi huyo anadaiwa kukwamisha utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli, kwa kushindwa kuunganisha umeme katika vijiji 68, kati ya 83 vilivyomo katika mkataba wake, huku muda wa mkataba huo ukikaribia kufikia ukomo Desemba, mwaka huu.



Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Kilimanjaro (Shivyawata), Hellen Mbando (aliyevaa miwani nyeusi), akiteta jambo na wanaharakati wanawake wakati wa uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja wa kutetea wanawake na wasichana dhidi ya ukatili wa kijinsia mkoani humo jana. **PICHA: GODFREY**

# DC aingilia kati uandikishaji wapigakura

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

MKUU wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, amemtaka msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo la Rombo, David Rubibira, kuondoa ukakasi kuhusu mkanganyiko wa uandikishaji wa wapigakura watakaoshiriki uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Hatua hiyo ya Hokororo, inatokana na dhana potofu waliyo nayo baadhi ya wananchi wa vijijini kwamba uandikishaji uliofanyika Julai, mwaka huu, wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ni kwa ajili ya uchaguzi huo.

"Nitoe angalizo kwamba ni lazima tuhakikishe wananchi wanapata elimu ya kutosha ili wahamasike kwenda kujiandikisha kupiga kura kwa sababu ziku zimebaki chache. Baadhi wanaamini kazi iliyofanyika Julai ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ambalo ni kwa ajili ya uchaguzi wa dola (uchaguzi mkuu) ndilo linalotumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema Hokororo juzi.

Uandikishaji wapigakura ambao watashiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, ulianza rasmi juzi na unatarajiwa kufikia ukomo Oktoba 14.

Alisema ili kumaliza ukakasi huo, kuna haja kwa viongozi wote kutimiza wajibu wao ili kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika katika hali ya utangamano mkubwa na kutimiza lengo la serikali la kuongeza usimamizi wa mamlaka za serikali za mitaa.

Kutokana na ukakasi huo, Rubibira alitoa ufafanuzi kuhusu uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa wagombea, akisema Kanuni ya 17 (1) na ya (2) zinaelekeza mgombea atachukua fomu siku 29 kabla ya uchaguzi na kurejesha ndani ya muda wa siku saba, tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu.

Agosti 23, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, alitoa tangazo la uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 kwamba utafanyika Novemba 24, wakati akitoa maelekezo yake kwa wakuu wa mikoa na wadau mbalimbali wa uchaguzi huo.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, kanuni za uchaguzi zimeeleza wazi kwamba upigaji kura utaanza saa 2.00 asubuhi na kuhitimishwa saa 12.00 jioni.

Waziri Jafo alisema viongozi watakoma uongozi wao, siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea.

Aliweka bayana kwamba waangalizi wa uchaguzi watauhusiwa baada ya kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Tamisemi na maombi yatatakiwa kupata kibali kwa Katibu Mkuu ndani ya siku 21, baada ya tangazo la uchaguzi kutoka.

ama
ALHAMISI OKTOBA 10, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Nyanya zinaboresha mbegu za kinababa

Ukurasa 14



Kichaa cha mbwa kinavyobaki janga la jamii mahali kote iliko

Ukurasa 15



Ukurasa 14


Mtaalamu: Ukiwa hivi, basi una tatizo



RIPOTI MAALUM HAZINA MAJI

# Dhana 'takwimu' ilivyokamata kelele, vilio vya watumia maji

Ukurasa 18



Nyanya zilizokaangwa. **PICHA: MTANDAO.**

# Nyanya zinaboresha mbegu za kinababa

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU wa afya, wamezama maabara na kuibuka na majibu kwamba wanaume wanaotumia nyanya zilizoandaliwa vyema jikoni, wana nafasi ya kuboresha mbegu zao za uzazi.

Timu ya wataalamu bingwa wanaohusika na masuala ya mbegu za uzazi wamesema kuwa, hiyo inaendana na haja ya kinababa wenye matatizo ya uzazi kuvaa chupi zisizobana.

Katika majaribio yaliyochukua wiki 12 (miezi mitatu), yalionyesha mafanikio kwa wanaume, kama ilivyo kwa watumiaji dawa.

Dk. Liz Williams, bingwa wa afya ya lishe kutoka Chuo Kikuu cha Sheffield, Uingereza aliyeongoza utafiti huo, anaeleza katika Jarida la Lishe la Ulaya kwamba, ili wanaume waimarishe uzazi wao wanapaswa kupunguza pombe na kuboresha lishe.

Mkurugenzi wa Huduma za Kliniki katika Chuo Kikuu cha Liverpool, Andrew Drakeley, anaongeza lingine la haja ya watu kupunguza msongo wa mawazo na kukutana kimwili, huzuni na walezi wao mara nyingi, hali inayosaidia uwezekano wa kupatikana mimba, kwa wahitaji.

Huko nyuma, utafiti ulifanyika na kuhimiza nafasi ya lishe zenye Vitamini E na madini ya zinki, kwamba zinasaidia uwezekano wa mimba kushika, japo hivi sasa kuna mjadala mwingine wa kitaaluma umeibuka.

• **Kwa mujibu wa majarida.**

## SIKU YA AFYA YA AKILI DUNIANI

# Mtaalamu: Ukiwa hivi, basi una tatizo

**Na Sabato Kasika**

MATATIZO ya afya ya akili ni changamoto inayowakumba watu wa rika tofauti, kuanzia vijana hadi watu wazima. Sababu kubwa ni kwenda kinyume na mtazamo na matendo sahihi.

Afya ya akili, kitaalamu ina uhusiano na ustawi wa mwili, kwamba inaufuatilia mwili kwa karibu, hata unapopata tatizo, akili inakuwa makini kuuhami kupitia mifumo yake.

Wakati mtu ana shida ya afya ya akili, inamaanisha hana nafasi ya mwamko sahihi ya kutetea mwili kwa madhara au unapokuwa hatarini. Hapo, kitaalamu kuna sababu nyingi zinazoigusa afya ya akili.

Leo dunia inaadhimisha Siku ya Afya ya Akili. Mtaalamu wa akili na jamii kutoka taasisi ya kijamii iitwayo, Psychosocial Health and Entrepreneurship Development Skills (PHEDES), John Ambrose, alipozungumza na Nipashe ana mengi ya kujuza.

Ambrose anasema, suala la afya ya akili ni muhimu na lina mtazamo, fikra na matendo ya kipekee. Mtu akitenda kinyume na mpangilio rasmi uliopo, huyo anatafsiriwa kuwa na tatizo la afya ya akili.

**Umri**

Anasema, kila umri una mtazamo, fikra na matendo yake na vyote vikienda kinyume na usahihi uliopo, jibu ni kwamba kuna tatizo la afya ya akili, ambalo ni muhimu likafanyiwa kazi liishe.

"Takwimu za dunia zinaonyesha, tatizo la afya ya akili linafanya vijana wa umri wa kati ya miaka 15 hadi 29 kupoteza maisha, kwamba kila baada ya sekunde 40 kuna mtu hufariki duniani kwa kujinyonga," anasema Ambrose.

Anaeleza vijana katika umri wa balehe wana mengi ya hatari, hivyo ni muhimu wakapewa elimu maalum inayohusu makuzi na afya ya akili, ili iwaweke sawa mbali na madhara yanayowazunguka.

Mtaalamu huyo, anafafanua kuwa ni umri ambao hata kijana akichapwa na mzazi wake, kwa sababu ya kufanya vibaya masomoni, anaamua kujiua.



Mtaalamu wa afya ya akili, John Ambrose, akizungumza katika ofisi za Nipashe. **PICHA: SABATO KASIKA.**

> **"Unaweza kukuta wengi wao wanafungwa kwa sababu ya kutokuwa wastahimilivu katika kutafuta maisha. Hii yote inatokana na mtazamo ambao ni hasi na kimsingi unatokana na tatizo la afya ya akili," anasema.**

"Hilo ni tatizo la afya ya akili, kutokana na mtazamo wake kwenda kinyume na kutawaliwa na mihemko ambayo ni hatari kwa maisha yake, hivyo ni muhimu kuelimishwa jinsi ya kuishinda hali hiyo," anasema.

Katika hulka hiyo, analitaja lingine la umri wa miaka 29 hadi 40, ambalo linachangamkia maisha hata kwa kuiba au kuomba rushwa, lengo likiwa ni kufanikiwa haraka.

Anasema, kichocheo cha hali hiyo ni afya mbaya ya akili. Anasema, kuna haja ya kuwasaidia vijana wa umri huo kuacha dhuluma na tamaa za maisha na wazingatie maadili kazini watimize ndoto zao kwa haki.

"Unaweza kukuta wengi wao wanafungwa kwa sababu ya kutokuwa wastahimilivu katika kutafuta maisha. Hii yote inatokana na mtazamo ambao ni hasi na kimsingi unatokana na tatizo la afya ya akili," anasema.

Anasema, pia afya ya akili inaingia katika ndoa; kuoa au kuolewa, elimu na kazini. Katika hilo, wapo wanaokosea kuchagua wachumba, wanaootoa ngono waahiriwe au kufanikiwa mtihani.

"Unapoona mtu anakwenda kinyume ili kutimiza lengo lake, basi ujue hilo linatokana na mtazamo wake wa kwenda kinyume ambao msingi wake unatokana na tatizo la afya ya akili," anasema.

Ambrose anasema, hilo pia liko kwa watu wazima, ambao mtazamo wao husababisha wasifikie malengo kwa kutofanya maamuzi sahihi kuanzia nyumbani hadi kazini na kujikuta wanakwama.

Mtaalamu huyo anasema, asasi yake ya Phedes inafanya kazi ya kuelimisha saikolojia katika maeneo mbalimbali nchini, kuanzia kwa mtu binafsi na ofisi, lengo ni kuwasaidia Watanzania kuepuka tatizo la afya ya akili.

"Pale tunapoona tatizo linahusu madaktari, tunawashauri wahusika kwenda hospitalini kupata huduma zaidi, lakini kama ni suala saikolojia, basi tunatoa elimu na tumesaidia watu wengi tu.

Anaeleza, suala la afya ya akili, kimsingi ni ukamilifu wa hisia, saikolojia na uhusiano wa jamii ikihusisha mtazamo wa mtu, fikra, matendo na tabia yake vinakuwa sawa.

"Sisi tunataka watu wajitambue na watambue wajibu wao ili wawajibike na kutekeleza majukumu yao ipasavyo, kwa maana ya kutokuwa na matatizo kwenye afya ya akili," anasema.

Anataja afya ya akili ni nyenzo muhimu inayomkalilisha mwanadamu dhidi ya maradhi ya ubongo na ustawi wake kijumla, unaotegemewa kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja.

Ambrose anataja ujumbe wa maadhimisho ya mwaka huu yanayofanyika leo ni 'Zuia Ukatili, Zuia Kujinyonga' ikiadhishwa maeneo mtambuka kupitia Siku ya Afya ya Akili Duniani, ambayo ni kila siku kama ya leo.

Mtaalamu huyo anataja ulingo mwingine wa maradhi hayo kwamba: "Mtu anapotumia dawa za kulevya hadi kufikia kutojitambua na kufanya mambo yasiyofaa kwenye jamii, basi ujue kuwa hilo nalo ni tatizo la afya ya akili. Wahusika wanatakiwa kusaidiwa kisaikolojia."

AFYA

Na Yasmine Protace

UKICHELEWA NI KIFO...

# Kichaa cha mbwa kinavyobaki janga la jamii mahali kote iliko

- Mbwa anayezurura hatari iliyojificha
- Unapokuwa na jeraha kaa mbali naye
- Kila miaka 87 nchini; tiba yake ni tishio
- Nusu hadi theluthi ya watoto wagonjwa



Mbwa wanaozurura ovyo mitaani ni hatari kwa kichaa cha mbwa. **PICHA: MTANDAO.**

KILA mwaka inapofika, tarehe 28 ya mwezi Septemba ni maadhimisho ya 'Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani na kaulimbiu ya mwaka huu ni: "Kichaa cha Mbwa: Chanja ili kukitokomeza."

Huo ni ugonjwa ulioathiri maeneo mbalimbali duniani, hususan Bara la Asia na Afrika. Chanzo chake kinatajwa ni virusi kutoka jamii inayoitwa 'lyssa' ambavyo hukaa katika mate ya wanyama jamii ya mbwa walioathirika; mbwa, paka, mbweha na fisi wanaangukia kundi hilo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema kuwa maambukizi pale anapoumwa na mnyama aliyeathirika, huingia kupitia jeraha analopata.

Ummy anataja takwimu zilizopo kwamba, zinakadiria kiwango cha maambukizi ya kichaa cha mbwa duniani kinafikia vifo 59,000 kila mwaka, kati yake asilimia 36 ya athari hiyo inaangukia barani Afrika.

Pia, kuna makadirio mengine ya takwimu kimataifa kwamba, wastani wa kati ya asilimia 30 nusu ya waathirika wa kichaa cha mbwa ni watoto wenye umri chini ya miaka 15.

"Ugonjwa wa kichaa cha mbwa hauna tiba. Pamoja na kusababisha vifo, ugonjwa huo unaleta athari kubwa kiuchumi, kwani gharama ya chanjo kwa binadamu ni kubwa," anasema Ummy.

Anafafanua: "Takriban Sh. 150,000 kwa mgonjwa kwa Bara la Afrika, ambayo ni sawa na asilimia sita ya mapato ya taifa katika bara hilo."

Waziri anarejea historia ya nchini Tanzania (tangu zama za Tanganyika), kwamba ugonjwa wa kichaa cha mbwa uliripotiwa kwa mara ya kwanza kati ya miaka ya 1932/33 na matukio yake yamedumu hadi sasa, ikiwa ni wastani wa miaka 87.

**HALI ILIVYO.**

Mwaka huu 2019, kuanzia mwezi Januari hadi Agosti mwaka huu, kuna jumla watu 16,290 walioripotiwa kuumwa na mbwa na vifo vinane viliripotiwa kutokana na kichaa cha mbwa.

Ummy anasema, tatizo la kichaa cha mbwa ni kubwa zaidi ya takwimu hizo, kwani hazijumuishi vifo vinavyotokea nyumbani na waathirika wasiofika katika vituo vya kutoa huduma za afya.

Utafiti uliofanyika mwaka 2002 nchini Tanzania ulibainisha kulikuwapo takriban vifo 499 kwa mwaka, kutokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Anasema, tafiti zimeonyesha waathirika wakuu wa ugonjwa huo ni watoto chini ya miaka 15, kwa sababu ndio wanaokuwa karibu zaidi na mbwa anayefugwa, pia wanapenda kuchokoza mbwa wasiofahamu.

"(Virusi vyake) kichaa cha mbwa kinapoingia katika jeraha hushambulia neva (mishipa) za fahamu kutoka katika eneo la jeraha, kuelekea katika uti wa mgongo na hatimaye kuathiri ubongo," anasema.

Anaongeza kwamba, dalili za ugonjwa kichaa cha mbwa huanza kuonekana baada ya kuathirika kwa mfumo wa kati wa fahamu na baadaye ubongo.

Hapo ndipo mgonjwa anatawaliwa na dalili za kuwashwa sehemu ya jeraha, homa, kuumwa kichwa, maumivu ya mwili, kuogopa maji na mwanga, kutokwa na mate mengi mfululizo, kuweweseka (kushtuka mara kwa mara na kuogopa), kupooza na hatimaye kupoteza maisha.

Ummy anasema, kuna wakati watu huhusisha dalili hizo na imani za kishirikina, haloi inayowafanya wasiende katika vituo vya kutoa huduma za afya na wanaishia kutibiwa kienyeji hadi kupoteza maisha wakiwa majumbani.

**MLIPUKO & KAMPENI**

Anasema, Aprili mwaka jana, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ilipata mlipuko wa ugonjwa huo na kusababisha vifo vya watu sita walioumwa na mbwa na kati yao, wanne walichelewa kwenda kupata chanjo ya kuzuia maradhi hayo na wakapaoteza maisha.

Waziri anaeleza udhibiti wake, tatizo hilo Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) na Shirika la Chakula Duniani (FAO), walishirikiana na serikali kupitia Dawati la Uratibu wa Afya Moja, ikatoa chanjo 33,700 kwa ajili ya kampeni ya kuchanja mbwa.

Kampeni ilifanyika tarehe 29 Aprili hadi 3 Mei, 2018, ambapo mbwa 15,314 na paka 1,057 walipatiwa chanjo katika wilaya hiyo.

Sambamba na hilo, elimu ya afya, ilitolewa kuhusu utoaji huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na mbwa na umuhimu wa kuwahi kupata chanjo.

Aidha, anasema mwaka huu ulitokea mlipuko mwingine katika Halmashauri za Wilaya za Ulanga na Malinyi ambao watu 292 waliumwa na mbwa na kati yao, wanne walipoteza maisha.

Katika kudhibiti mlipuko huu, kupitia Dawati la Afya Moja, Wizara ya Mifugo ilipata chanjo 16,000 kwa ajili ya kuchanja mbwa. Zoezi la kuchanja mbwa lilitekelezwa Mwezi Aprili hadi Mei, 2019.

Aidha, elimu ya kujikinga dhidi ya kichaa cha mbwa ilitolewa kwa shule za msingi na viongozi wa kata, ili kujikinga na kichaa cha mbwa.

Namna ya kujitibu, ni hatua ya kwanza muhimu ni kuosha jeraha kwa dakika 10 au zaidi kwa maji mengi yanayotiririka na sabuni na baada ya hapo kidonda kisifungwe.

Hatua inayofuata, inaelezwa ni kwa mgonjwa kupelekwa haraka katika kituo cha kutoa huduma za afya, ili kupata chanjo ya kichaa cha mbwa kwa kupatiwa dozi kamili.

Anafafanua kwamba, hadi sasa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inafafanua kwamba imekwishatolewa maagizo kwa mikoa na halmashauri kuhakikisha chanjo hizo zinakuwapo katika vituo vya huduma za afya, kwa wananchi wahitaji.

Ummy anasema, wanyama jamii ya mbwa na paka, daima wasiruhusiwe kulamba vidonda vya binadamu, kwani mate yao yana hatari ya kuambukiza, kwa waathirika.

**HATUA MUHIMU**

Rai yake ni kwa wamiliki kuzuia maradhi hayo mara moja kila mwaka na kupatiwa cheti cha chanjo na mbwa wadhibuitiwe na wasiachwe kuzurura ovyo, kwani wanapozurura, inakuwa rahisi kwamba kupata maambukizi kutoka kwa wanyama wenzao wanaoumwa.

Agizo la waziri linaenda mbali, kutaka watoto wapewe elimu stahiki na wakatazwe kuchokoza mbwa wasiowajua njiani, kama vile tabia ya kuwavuta mkia, masikio uya hata masihara ya kuwapandia mgongoni.

Ummy anasema katika utekelezaji mikakati ya pamoja kwa sekta zote zinazohusika kudhibiti ugonjwa huu, wizara yenye dhamana na afya nchini, inashirikiana na WHO, shirika la OIE na asasi zisizo za kiserikali kupitia uratibu wa dawati liitwalo 'Afya Moja' kuandaa

mkakati wa kitaifa wa kudhibiti kichaa cha mbwa wenye lengo kuu la kutokomeza ugonjwa huo nchini ifikapo mwaka 2030.

Ummy anasema, mkakati unasisitiza ushirikiano wa sekta mtambuka kitaifa kudhibiti kichaa cha mbwa, ikijumuisha hatua kama kuwachanja mbwa, kuhakikisha chanjo ya binadamu inapatikana katika vituo vya huduma za afya na elimu kwa umma inayozingatia dhana ya kujikinga.

MAZINGIRA

NEEMA WORLD VISION...

# Furaha kupata bomba waliochangia maji na wanyama visima kata jirani

- Mfadhili: Vuta nyumbani, mtunzaji wewe
- Mama kuamka alfajiri, binti mimba 'stop'
- Zahanati kupumua wagonjwa wa kuhara



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akikinga ndoo ya maji ya mkazi wa Kata ya Iyenze, katika uzinduzi wa mradi wa maji uliojengwa na World Vision Tanzania. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, Kahama**

SERIKALI imekuwa ikipambana kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na binafsi katika kuwapelekea wananchi walio pembezoni mwa miji huduma ya majisafi na salama.

Katika utekelezaji, inachimba visima virefu na vifupi ikiwa na kuwajengea maghati ya maji, yanayotumiwa na wananchi kujikimu dhidi ya adha ya kukosa maji, ili kama namna ya kupisha visima vya kienyeji au madimbwi ambavyo sio salama kiafya.

Wananchi nao wamekuwa wakijitahidi kuchimba visima kwenye maeneo yanayopatikana maji kirahisi, lakini mwisho wake visima hivyo vimekuwa vikikauka kutokana na shughuli za kibinadamu.

Kutokana na baadhi ya vijiji na kata kuwa na changamoto ya majisafi na salama, wananchi wake wamekuwa wakitumia maji yaliyotuama madimbwini, wakichangia na mifugo, hata kuwasababishia ongezeko la magonjwa ya kuambukiza, kama ya kuhara.

> “Hatutaki kurudi nyuma kutumia maji tena na wanyama wetu ambao tunawafuga. Tuutunze mradi wetu kama dhahabu usije ukaharibika na kuanza tena kinamama kutembea umbali mrefu kutafuta maji na ikiwezekana wekeni tozo za kisheria, ili ikitokea tatizo tuweze kukarabati,” anasema Macha.

Hata asilimia kubwa ya maradhi yanayoripotiwa katika zahanati vijijini na vituo vya kata, mengi yanayoongoza ni yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

**WADAU WANENA**

Kutokana na changamoto hizo, Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania, wilayani hapa mkoani limejenga mradi wa maji wa kutumia umeme wa jua unaotoa zaidi ya lita 5,350 za maji, kwa matarajio ya kuwahudumia wananchi zaidi ya 30,000 katika kijiji na kata ya Iyenze ndani ya Halmashauri, iliyoko katika mji wa Kahama.

John Massenza, ni Meneja wa Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania, Kanda ya Ziwa, anasema wamechimba kisima katika kijiji na kata ya Iyenze, ambako kitawahudumia wananchi hao maelfu.

Anasema, lengo la mradi pia ni kuwahudumia watoto zaidi ya 10,000 ambao kwa asilimia kubwa, ndio walikuwa wakitaabika na maradhi yatokanayo ya matumizi ya maji machafu na itasaidia kuhudumia kituo cha afya na taasisi za elimu.

Masenza anasema, mradi huo wa kutumia umeme umegaharimu Sh. milioni 150 na unawagusa kinamama kwa kuwanusuru kuamka alfajiri kwenda kata jirani kutafuta huduma ya maji.

Unalindwaje? Meneja huyo anasema, ili mradi usife ni vyema serikali ya kijiji ikaanzisha utaratibu wa kisheria ya wananchi kuchangia japo gharama au tozo kupitia ndoo za maji wanazochota na ikitokea tatizo, wanawajibika kurekebisha.

Masenza anafafanua kuwa, miradi mingi inakufa baada ya wahisani kuikabidhi kwa wananchi na chanzo kikuu kinatokana na usimamizi mbovu wa mradi.

Kwa mujibu wa Masenza, lengo la mradi ni kuhakikisha maji yanafika sokoni au magulioni na taasisi za elimu.

**MRATIBU MRADI**

Mratibu wa mradi, Machibya Mwalla, anasema kila mwananchi anatakiwa kuvuta maji nyumbani kwake, kwani lita za maji zinazopatikana ni nyingi sana, kulinganisha kiasi cha wakazi hao.

Mbali na hiyo, ansema maji hayo yatapatikana muda wote na matarajio ya sasa ni kuyapeleka katika Kituo cha Afya cha Iyenze na shule za msingi na sekondari zilizopo katika kijiji na kata ya Iyenze.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akizungumza na wananchi wa kata ya Kilango na Iyenze, kabla ya kukagua na kufungua mradi wa maji wa World Vision.

Anasema, mradi kwa sasa uko chini ya serikali ya kijiji na matarajio ni kuona kila mwananchi ananufaika nao, huku akisisitiza haya ya kila mmoja kuwa mlinzi wa mradi, kunusuru wasio na nia njema wakaiba mfumo wa umeme wa jua na miundombinu mimgineyo.

**WATUMIA MAJI**

Monica Jefta, ni mkazi wa kijiji cha Iyenze, anayesema walikuwa wanatembea umbali mrefu kutafuta huduma ya majisafi na salama kwa zaidi ya kilomita 20 kwenda kwenye kata za jirani kutafuta maji.

Anaeleza uzoefu wa walikotoka, waliamka alfajiri wakiwaacha waume na watoto majumbani, kwenda maji na wakati mwingine walilazimika kutumia maji ya mashimoni na madimbwi, wakichangia na mifugo yao ambayo, hali anayosema ilihatarisha afya zao.

“Ndoa zetu ziliingiwa na mashaka pale tulipokuwa tukiamka alfajiri na kwenda vijiji vya kata ya jirani kwenda kutafuta huduma ya maji na wakati mwingine wenzetu waliingiwa na wasiwasi na kutishia kutuacha na tukiacha kutafuta maji hakuna kupika wala kupakua,” anasema Monica.

Pia anasema kuwa, kuna wakati walilazimia kuwaachisha shule watoto na kutoendelea na masoko kwa siku moja ili kwenda kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, jambo lililokuwa linamnyima mtoto kusoma kwa kipindi ambacho ndani ya maji yanakuwa yamekwisha.

Samson Mabula, anasema kitendo cha wake zao kuamka alfajiri kwenda kutafuta huduma ya maji kilikuwa kinawatia wasiwasi mkubwa juu ya usalama wao na kuhofiwa, kusalitiwa kwenye ndoa huku wengine wakidiriki kuvunja miji yao.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Mayala Jagadi, anasema walikuwa wanashambuliwa na maradhi yanayotokana na kutumia maji ambayo sio safi na salama kutokana na kutumia maji ya mitaroni na madimbwi yanayotumiwa na mifugo. Mayala, anasema kukosekana kwa maji pia kulisababisha kijiji chao kuwa na ongezeko la mimba kwa wanafunzi na watoto wao, walitumia kufanya matendo hayo wanapokwenda kutafuta huduma ya maji kwa zaidi ya kilomita 20.

**DC KAHAMA**

Anamringi Macha, ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, anayesema kupatikana kwa huduma ya maji karibu, kutasaidia ongezeko la uzalishaji na shughuli za kijamii, kutokana na wakati waiotumia wanajamii wake na hasa kinamama, walielekea kutafuta maji.

Mkuu wa Wilaya anaeleza matazamio kwamba, afya za wananchi zitaimarika, tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyumba na kuongeza maji ambayo kwa sasa yanatumika yamepimwa na kuthibitishwa hayana madhara na yanafaa kutumiwa.

Pia anasema sambamba na hilo, afya za watoto waliodhoofika na wengine kudumaa kutokana na kushambuliwa na magonjwa mengi zitaimarika.

Anarejea kauli ya viongozi wa World Vision, kwamba hivi sasa kila mmoja anapaswa kutunza mradi usiharibike, jambo linaloweza kuwahatarisha warejee kutumia maji ya visima vya kenyeji, kama walikotokea awali.

Pia anaunga mkono wanakijiji na kata ya Iyenze, kuchangia gharama za matumizi ya maji, ili wahisani World vision Tanzania inapoondoka, mradi ujiendeshe na kuondokana na dhana ya pindi utakapoharibika watarekebishiwa.

“Hatutaki kurudi nyuma kutumia maji tena na wanyama wetu ambao tunawafuga. Tuutunze mradi wetu kama dhahabu usije ukaharibika na kuanza tena kinamama kutembea umbali mrefu kutafuta maji na ikiwezekana wekeni tozo za kisheria, ili ikitokea tatizo tuweze kukarabati,” anasema Macha.

Mkuu wa Wilaya anasema, serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wa maendeleo, wataendelea kutoa huduma ya majisafi na salama katika maeneo yote vijijini na kata ambazo zina changamoto za huduma hizo.

Hivi karibu, serikali ilianzisha huduma ya maji vijijini, ambazo watajihusisha na upelekeaji maji katika vijiji vyote vyenye changamoto ya ukosefu wa majisafi na salama na kusaidia kupunguza adha kwa wananchi wanaochangia maji na wanyama.

• ***Soma ripoti maalum Uk. 18.***

## Kupanda na kushuka umri binadamu kulivyo




Bibi wa Kifaransa, Jeanne Calment, aliyefikisha umri mkubwa ulioweka rekodi duniani, miaka 122. **PICHA: MTANDAO.**

UMRI na uhai wa binadamu kuishi katika kipindi cha historia ya karne mbili zilizopita, kumekuwa na mabadiliko makubwa kila wakati ikichukua sura yake.

Kurejea historia ya nyuma, katika mwaka 1840 umri wa watu kuishi ulikuwa wastani wa miaka 40 tu. Lakini, maboresho katika huduma za kimaisha yameleta mapinduzi makubwa.

Hapo kunaelezwa vitu na mambo kama vile upatikanaji wa lishe bora, uhakika wa afya, makazi na huduma za majitaka, yanaelezwa kuwa nafasi kubwa ya kuleta mageuzi makubwa katika uhai wa mwanadamu.

Ni jambo lililofanyika hadi kufikia mwaka 1900, uhai wao kwa jumla ukafikia umri wa miaka 60 na kadri siku zilivyoendelea, ukiondoa miaka dunia ilivyokumbwa na athari za vita, kuna mageuzi makubwa yameshuhudiwa.

Jambo hilo, mafanikio yake yalitokana na maboresho ya kinga kiafya inayowafanya watu wafanikiwe kiafya. Kuanzia miaka ya 1970 kunaelezwa kuwapo maendeleo katika maboresho dhidi ya matatizo ya maradhi ya kupooza na shida ya ugonjwa wa moyo.

“Kwa kuanza karne ya 21, umri wa kuishi imefikia miaka 80 kwa kinamama na miaka 75 kwa kinababa,” inaeleza taarifa ya kitafiti na kila baada ya miaka minne kuna maendeleo zaidi.

Hata hivyo, kufika mwaka 3011 kunaelezwa kuwapo mabadiliko ya umri wa kuishi kwa mwanadamu kuanza kupungua.

Kuna mfano wa marejeo, mwaka 2015 unaelezwa kuwa wa kipekee, katika mazingira ya Ulaya hususan nchini Uingereza, kunakoelezwa kuwapo ongezeko la vifo na chanzo kikubwa kinachoangukia kutoka maradhi ya homa.

Kwa mujibu wa ubashiri wa kitaaluma, ni kwamba hadi baada ya miaka 12 ijayo, hali itarejea na umri wa kuishi utaanza tena kuongezeka maradufu.

Rekodi rasmi inaeleza kwamba, binadamu aliyeishi katika umri mkubwa zaidi ni mama wa Kifaransa, Jeanne Calment, aliyefikisha umri wa miaka 122 na alishafariki zaidi ya miaka 20 iliyopita.

Jarida la kitafiti la kiafya, linaeleza upande wa pili wa kuwapo wanaopinga nadharia ya kuongezeka na kugota umri wa kuishi, akiwamo mtaaluma wa Kimarekani, David Sinclair, katika kitabu chake kiitwacho 'Umri wa Kuishi' anayesema chembehai za mwanadamu zinaweza kuongezewa umri wa kuishi.

Nchini Japan, kunatajwa katika siku za karibuni, umri wa kuishi kwa wananchi wake umeongezeka kwa kasi zaidi kulingana na kwingineko duniani.

Mtaalamu wa afya nchini Uingereza, Edward Morgan, anasema kuna mazingira mengi tata yanayochangia mabadiliko hayo yanayohusiana na umri wao kuishi na kunahitajika uchunguzi wa kina kuyapatia majibu.

Asasi ya Afya ya Umma ya Uingereza, ilishachapisha ripoti yake mwaka jana, ikitaja sababu za ziada kuhusu hilo, inayojumuisha mageuzi katika suala la afya ndani ya miongo kadhaa iliyopita.

Katika ufafanuzi wake, kunaelezwa kwamba kuna aina ya mazingira, kama vile vifo vinapungua katika upande mmoja, eneo la pili linachukua nafasi yake kukitajwa maradhi kama vile ya moyo, kansa na kupooza.

Ripoti ya Afya ya Umma nchini Uingereza, imefanyia kazi kitu kilichofanywa awali na mtaaluma wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Profesa Michael Marmot, anayesema kuwapo ushahidi unaofafanua kwamba jamii masikini ndio wanaoathirika zaidi katika majanga hayo ya kiafya.

Mtazamo wa mtaaluma huyo ni kwamba, pasipo kuwapo uangalizi bora, pia usimamizi mzuri kisera, kunaongeza kiwango cha madhara kwa jamii.

RIPOTI MAALUM HAZINA MAJI

# Dhana 'takwimu' ilivyokamata kelele, vilio vya watumia maji

- Wataalamu: Wadai gharama, ilikotoka hawajui
- Udhibiti matumizi wengi bado 'mbumbumbu'
- Imebeba siri ya ugomvi wakulima vs wafugaji
- Imekamata utalii, viwanda, miji, madaraja

**Na Frank Monyo**

MIAKA miwili iliyopita baada ya mume wangu kufariki, maisha yalikuwa magumu sana, maana mzigo wote wa familia ulikuwa juu ya yangu.

"Kilichokuwa kinaniumiza hasa ni bili ya maji. Nilikuwa nalipa Sh. 50,000 hadi Sh. 65,000 kwa mwezi, bado na mahitaji mengine," anasema Flora Mbega, mkazi wa Kimara, jijini Dar es Salaam, mwenye familia ya watu watano.

Flora, mchuuzi katika wa Soko la Mabibo, Dar es Salaam, anaeleza amekuwa akigombana na wasoma mita, hadi kufikisha malalamiko kwa Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) Kimara na makao makuu, kuhusu bili kubwa ya maji.

Anasema alijiuliza kulikoni familia ndogo ina matumizi makubwa ya maji, ingawa upande mwingine anakiri hakuwa na uelewa wa takwimu zake.

Baada ya sintofahamu ya muda mrefu, anasimulia ugunduzi wake: "Ilinibidi nifanye uchunguzi baada ya kushauriwa na Dawasa, ndipo nikagundua msichana wangu wa kazi pamoja na watoto walikuwa hawana 'discipiline' (nidhamu) na maji.

"Walikuwa wakiosha vyombo bombani, nguo wanafulia hapo hapo na wanaacha bomba linamwaga maji na walikuwa wanagawa maji kwa majirani."

Anaeleza hatua aliyochukua, ni kuwakanya watoto wanaobaki nyumbani dhidi ya tabia inayomhujumu na akanunua tangi la kuhifadhi maji la lita 10,000, akifafanua: "Pia nilipiga marufuku kufulia nguo bombani na nikawajengea sehemu maalum ya kufanya shughuli hizo."

"Kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na takwimu za matumizi ya maji katika ngazi ya familia, ili kuweza kulipia gharama za maji kulingana na matumizi yako," anaeleza.

Sura ya pili ya kilio cha bili, ipo kwa Joseph Shauri, mkazi wa Tabata, Dar es Salaam, anayelalamika kuwapo wasoma mita wasio waaminifu.



Mfanyakazi wa Dawasa, akihakiki mita ya mteja wakati wa kuwatambua, kuwasikiliza na kutatua kero zao, jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: FRANK MONYO**

> **"Nilikuwa naishi kwenye nyumba ya kupanga Tabata, tulikuwa wapangaji kama wanane, kila mwezi bili ilikuwa inapanda. Kwa kawaida tulikuwa tunalipa Sh. 15,000 kwa mwezi, lakini ikafika hadi Sh. 49,000 na wakati mwingine inafika hadi Sh. 50,000.**

"Nilikuwa naishi kwenye nyumba ya kupanga Tabata, tulikuwa wapangaji kama wanane, kila mwezi bili ilikuwa inapanda. Kwa kawaida tulikuwa tunalipa Sh. 15,000 kwa mwezi, lakini ikafika hadi Sh. 49,000 na wakati mwingine inafika hadi Sh. 50,000.

"Baada ya kusumbuana sana, wapangaji tuliamua kufuatilia jambo hili na kugundua kijana aliyekuwa anasoma mita alikuwa anaichezea," anasema Sauri.

Mkasa mwingine wenye wajihi huo, unamhusu

Maneno Salum, mhudumu katika nyumba ya kulala wageni (jina tunalo) iliyopo katikati ya Jiji la Dar es Salaam, anayeangukia kilio cha uelewa duni wa wateja kuhusu kiwango cha matumizi yao.

Anasema, kuna baadhi ya wateja wanakosa ustaarabu na kutumia vibaya maji wanapokabidhiwa chumba hata kuna wakati anakuta mabomba hayajafungwa, hivyo anapaisha sauti kwa Dawasa kutoa elimu.

"Hapa kwetu tunatumia maji ya bomba (Dawasa) na tuna matangi ya lita 40,000 ambayo tunayajaza. Hizi tangi unazoziona, maji yanakaa wiki moja au mbili kama kukiwa na shida ya maji, si unajua kuna kufua mashuka pia," anasema.

**Dawasa wafunguka**

Mtumishi wa Dawasa, msoma mita za maji ambaye hakutaka kutaja jina lake, anakiri wingi wa malalamiko ya bili za maji, akitaja sababu kuu ni wateja wengi hawajui uhalisia wa matumizi yao.

"Binafsi ninapoenda kusoma mita za maji au kuwakatia huduma ya maji wadaiwa sugu kwa kushindwa kulipa. Huwa nawapa darasa kidogo, kuwa maji kwa sasa ni mengi hata mgao wa maji umepungua.

"Baadhi ya maeneo sasa kama utakuwa unafurahia tu kutumia maji bila 'care' (uangalifu) utaleta usumbufu tu wakati wa kulipa,"anasema na kuongeza:

"Nawaambia (anawauliza) wanajua wanatumia maji kiasi gani kwa mwezi, itawasaidia kupunguza gharama?," Anasema.

Meneja Mawasiliano wa Dawasa, Everlasting Lyaro, anaungana kukiri malalamiko ya bili kubwa za maji tofauti na matumizi halisi.

Anasema, Dawasa ina utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya maji, kwani wengi wanalalamikia bili, pasipo kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

"Utakuta wengine matumizi yao yapo kwenye bustani ya mbogamboga, mifugo na wengine utakuta wanauza maji kabisa, bila ya kujua shughuli hizo huleta gharama kubwa," anasema Lyaro, akibainisha utafiti wao uliowapa mwanga kuhusu shida kubwa iliyojificha kwa wasaidizi wa kazi wanaobaki majumbani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, anasema zamani kulikuwapo na matumizi mazuri ya maji, kwa sababu ya changamoto ya upatikanaji majisafi na salama, tofauti na ilivyo sasa.

Anarejea mwaka 2015, upatikanaji maji jijini Dar es Salaam ulikuwa asilimia 68 na kuwapo maunganisho 123,000. Anaendelea kufafanua:

"Dawasco kipindi hicho kabla ya kuunganishwa na Dawasa, ilikuwa inakusanya kiasi cha Sh. bilioni 3.2 kwa mwezi. Leo tunapoongea hali ya upatikanaji maji jijini imepanda hadi asilimia 85 na maunganisho ya maji yameongezeka

INAENDELEA UK.19

RIPOTI MAALUM HAZINA MAJI

# Dhana 'takwimu' ilivyokamata kelele, vilio vya watumia maji

INATOKA UK.18

kutoka 123,000 hadi kufika 326, 000."

**Bonde Wami/Ruvu**

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, Hamza Sadick, anasema takwimu za rasilimali maji za muda mrefu ni muhimu kumwondolea umaskini mwananchi, sambamba na kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030.

Sadick anasema, mamlaka za maji kote nchini, haziwezi kufanya shughuli zake bila ya takwimu zinazoipa dira na mwongozo wa ugawaji maji na utekelezaji miradi yake.

"Kama mamlaka za maji zinatumia takwimu za rasilimali za maji katika kugawa maji kwa watumiaji, kwanini watumiaji wasiwe na takwimu za maji wanayotumia majumbani au kwenye maeneo mengine?" Anahoji.

"Hii itasaidia pia katika utunzaji wa vyanzo vya maji kwani ukijua kutumia maji kwa uangalifu vyanzo vya maji vitabaki salama," anafafanua.

Anasema takwimu hizo zinasaidia kupunguza umaskini, kuinua kipato, kukuza uchumi na kuipa serikali dira ya utekelezaji miradi kama kilimo, mifugo, utalii, usafirishaji na ujenzi wa madaraja, ikisaidia kutathmini kipindi na kiwango mito inafurika maji na madhara yake

Anasema, nchini kuna vituo vya kukusanya takwimu za uhai wa mito na maji, kazi inayofanyika mara mbili kwa siku; asubuhi saa tatu na alasiri saa tisa alasiri, kwa njia ya kisasa na kizamani, wakitumia vifaa maalum vilivyoweka mtoni.

"Katika upanuzi wa barabara kutoka Kimara (Dar es Salaam) kwenda Kibaha... ukipita pembeni mwa barabara kuna madaraja. Ili ujue, unatakiwa kujenga daraja lenye ukubwa kiasi gani, lazima ujue wingi wa maji yanayopita kwenye daraja hilo kipindi cha kiangazi au masika.

"Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mto Rufiji, takwimu zake zimeanza kuchukuliwa miaka 60 iliyopita na ndio maana serikali imeamua kuweka fedha nyingi ikiwa na uhakika wa maji ya kutosha kuzalisha umeme.

Anaongeza kwamba, katika maamuzi ya kuhamishia mji mkuu Dodoma, yalifanyika baada ya kupata takwimu zinazojitosheleza kuhusu maji ardhini, hatua inayotumika katika miradi kama kilimo na ufugaji.

**Uanzishaji viwanda**

Sadick anasema, mtu hawezi kuanzisha kiwanda pasipo kufahamu kiasi cha upatikanaji maji na matumizi yake, kwani hakuna kiwanda duniani kisichotegemea maji katika shughuli zake za uzalishaji.

Anasema, kwa maana hiyo serikali, wadau wa maendeleo pamoja na wawekezaji hawana budi kutumia takwimu za rasilimali za maji endelevu katika kutekeleza azma ya serikali ya kuwa Tanzania ya viwanda.



Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, Hamza Sadick (wa kwanza kulia), alipotembelea mtambo wa maji wa Ruvu Chini.

"Wafugaji wengi kutoka Mwanza na Arusha wanakimbilia Morogoro na mifugo yao kwa ajili ya kufuata hali ya hewa nzuri kwa mifugo na malisho," anasema.

"Hivi vitu lazima viende sambamba, serikali kwa sasa imetenga mkoa wa Pwani, kuwa ni eneo la viwanda hivyo ni wazi viwanda vingi vitajengwa kule na lazima vitumie maji. Swali ni je, maji tunayo ya kutosha kwa mahitaji ya viwanda?" Anahoji.

Ofisa wa Maji Bonde la Wami-Ruvu, Simon Ngonyani, anasema wadau wa maendeleo na serikali wanapaswa kuunga mkono utunzaji maji.

Anataja changamoto kubwa kwa bodi yao ni ongezeko la viwanda katika ukanda wa bonde, hivyo inaazaa haja ya kuwapo jitihada kuhakikisha vyanzo vinalindwa kutunza maji, akitaja hofu ya hatari ya maji kuwa kidogo baadaye, sababu ni kuongezeka watumiaji.

"Tujiulize maswali haya; maji yapo wapi? Swali la pili; je, kwa haya maji yaliopo ni endelevu...yataendelea kuwapo na kutosheleza mahitaji?" Anahoji na kuendelea:

"Swali la tatu; je, maji yaliyopo yana ubora? Tukipata majibu ya haya maswali tutaona tunatakiwa kuchukua jitihada za makusudi katika kuongeza nguvu katika utunzaji wa vyanzo vya maji."

**Mvua na mto**

Sadick, ambaye ni mtaalamu wa rasilimali maji (Hydrogeologist), anasema nchini nyingi ukanda wa tropiki zinategemea mvua kujaza mito na visima na anafafanua: "lakini maji yaende chini ya ardhi, ili visima viwe na maji ya kutosha na chemchemu zitoe maji."

Kwa mujibu wa Sadick, takwimu za mvua zinaonyesha jua kali linaweza kukausha maji ya ardhini, hivyo ni lazima kuwapo takwimu za mahitaji kama uvukizo (evaporation), mgandamizo wa hewa, (humidity), kasi ya upepo na ukali wa jua.

Pia anakumbusha asili yake kwamba, maji ni mazingira, wingi na ubora wake unasaidia kuamua matumizi, hivyo anarejea umuhimu wa takwimu ili kuamua mahitaji ya binadamu, kilimo, viwanda na viumbe hai.

Anasema mito yote nchini hufanyiwa tathmini ya kunusuru, kwa kuchukua vipimo vinavyotoa majibu ya uhai wa mto husika, tathmini mojawapo ni viumbe vilivyomo.

"Kuna baadhi ya mito unaweza kupima uhai wake na kukuta baadhi ya viumbe hai havipo hapo utagundua kuwa oksijeni kwenye maji ni ndogo, kwa mfano aina fulani ya samaki hawapo au mimea fulani haipo," anasema.

"Wenzetu wa hali ya hewa (TMA) kazi yao ni kutabiri, lakini sisi kwenye maji kazi yetu ni kufanya hesabu mito yetu itachukua maji ya kiasi gani kwa mvua itakayoonyesha, kwani tunafahamu uwezo wa udongo jinsi ya maji yanavyofyonzwa," anasema.

**Maji ardhini**

"Tunachimba visima sehemu nyingi, lakini tunajua tuna maji kiasi gani chini ya ardhi" anasema na kuongeza: "Lazima tujue tuna maji kiasi gani chini ya ardhi pamoja na aina ya miamba kwa maana hiyo kuna visima vya uchunguzi vipo sehemu mbalimbali."

Anatoa mfano takwimu zilizokusanywa zaidi ya miaka 40 katika eneo la Mzakwe, Makutupora ambako ni chanzo cha maji kwa jijini Dodoma, zimesaidia serikali kuhamia mkoani humo, licha ya kuwapo ukame.

Sadick anasema, tathmini ya serikali iligundua miaka ijayo maji yaliyoko hayatakidhi matumizi na ikabuni chanzo kingine katika Mto Bubu, eneo la Falkwa Usandawe, kujenga bwawa litakalokinga Mto Bubu, kusambaza maji Dodoma.

**Wakulima & Wafugaji**

Mtaalamu Sadick anasema, takwimu za maji zinasaidia kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji na anatoa mfano kilichotokea mkoani Morogoro, mzizi mkuu ni maji.

"Wafugaji wengi kutoka Mwanza na Arusha wanakimbilia Morogoro na mifugo yao kwa ajili ya kufuata hali ya hewa nzuri kwa mifugo na malisho," anasema.

Mfugaji kutoka jamii ya Kimasai eneo la Ngerengere mkoani Morogoro, Matayo Dakelo, anasema wakati wa kiangazi wanategemea maji ya mito, mabwawa na visima kunywesha mifugo yao, anakokueleza hayana magonjwa.

Anasema suala la wafugaji kupata taarifa za maji na mvua kwa mwaka au mwezi, ni changamoto katika maeneo yao, kwani wengi hawana elimu hiyo.

"Maji ambayo yanatembea hayana maradhi, ndio maana tunapenda kunywesha mifugo katika mito, lakini kama serikali imetukataza,

INAENDELEA UK.20



Mfugaji wa wilayani Kilosa, akipitisha ng'ombe wake mtoni, baada ya kuwanywesha maji. Picha ndogo ni mfugaji, Matayo Dakelo, kutoka Kilosa.

RIPOTI MAALUM HAZINA MAJI

# Dhana 'takwimu' ilivyokamata kelele, vilio vya watumia maji

INATOKA UK.19

basi itusaidie kujenga mabwawa kwa ajili ya kunywesha mifugo yetu na kama wakiweka gharama ndogo tutalipia, ikiwa kubwa hatutaiweza," anasema Dakelo.

**TMA je?**

Septemba 4 mwaka huu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitoa ripoti ya utabiri wa mwelekeo wa mvua za vuli, kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2019.

TMA inaeleza athari zitakazoweza kutokea kwa sababu ya mvua nyingi inajumuisha magonjwa ya mlipuko na uhaba wa majisafi na salama.

Mkurugenzi wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, anasema katika kipindi hicho kunakuwapo upungufu wa malisho, mvua zinakuwa za wastani au kidogo na kusababisha migogoro ya wakulima na wafugaji. Sadick anasisitiza wakulima na wafugaji kupata takwimu sahihi na za muda mrefu, kuondoa migogoro hiyo.

**DC Kilosa**

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoyi, analaumu wananchi wake hawazingatii sheria za maji, kwani wengi wanachepusha na kusababisha maafa kupitia mafuriko wakati wa mvua.

"Sisi Kilosa, udongo wetu ni laini, kwa hiyo wananchi wanavyochepusha maji bila utaratibu wa kujali mamlaka zinazosimamia wanasababisha athari.

Katika maoni yake, Salehe Selemani, mkazi wa Kitongoji cha Behewa wilayani Kilosa, ana sababu zingine, akisema katika kata yao kuna miradi mingi ambayo wajenzi wanatumia mchanga kutoka mto Mkondoa kwa njia ya isiyo sahihi na kusabaisha mto kuhamisha mkondo wake.

"Sasa ni mwezi wa 10 tunaenda mwezi wa 12, tunaanza kupokea maji (mafuriko) kutoka kwa wenzetu Bara (mikoa jirani). Sasa kwa hali hii tusipochukua tahadhari mapema itatuletea shida katika maeneo yetu," anasema.

**Waziri Mbarawa**

Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, katika hotuba iliyopita ya bajeti bungeni, anasema Azimio la Mwaka 2010 la Umoja wa Mataifa (UN), linatamka maji na usafi wa mazingira, ni haki ya msingi ya binadamu.

Pia anasema malengo yake endelevu ya UN ya mwaka 2015 hadi 2030, yanasisitiza upatikanaji majisafi na salama na usafi wa mazingira kwa wote.

Waziri anasema, Taarifa ya Maendeleo ya Maji Duniani ya Umoja wa Mataifa, inaonyesha zaidi ya watu bilioni mbili duniani wanaishi kwenye uhaba mkubwa wa maji, huku watu na shughuli za kiuchumi, ukame na mafuriko vyote vyaogezeka, kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Anasema, zaidi ya watu bilioni 2.1 duniani hawapati majisafi na salama na kati yao, watu milioni 844 hawapati maji safi ya kunywa.

Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2016, inahusu zaidi ya watu milioni 340 wanakosa huduma ya maji ya kunywa na wengine zaidi ya milioni 547 waliko katika mazigira machafu, hivyo kuna hitaji la maboresho.

Profesa Mbarawa anasema, maji nchini yanategemea mvua za vipindi viwili, masika na vuli na katika maeneo mengi yanapata wastani wa milimita 900 hadi 2000 kwa mwaka, wakati maeneo makame nchini yana milimita 400 hadi 550.

Anataja kwenye mvua nyingi, Nyanda za Juu Kusini na Milima ya Usambara, kuna wastani wa milimita 2,200 hadi 2,500 kwa mwaka.

Waziri anakadiria matumizi ya maji kwa mwaka ni mita za ujazo bilioni 126, yakigawanyika maji juu ya ardhi mita za ujazo bilioni 105 na chini ya ardhi, mita za ujazo bilioni 21.

"Hifadhi hiyo ya maji inaonyesha kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,300, ukilinganisha na wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa," anasema.

Anarejea historia, kiasi cha maji kwa mtu kila mwaka kinaendelea kupungua kutoka mita za ujazo 7,862 mwaka 1962 nchi ilipokuwa na watu milioni 10.6 hadi kufikia mita za ujazo 2,300 mwaka 2018, nchi ikiwa na watu milioni 54.

Waziri anasema, maji yanayohitajika majumbani kumwagilia, viwandani na mazingira, ni mita za ujazo bilioni 40 kwa mwaka, kati ya mita za ujazo bilioni 126 zilizopo kwa mwaka.

Vilevile, makadirio yanaonyesha maji yataongezeka kufikia wastani mita za ujazo bilioni 57 kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

Pofesa Mkumbo

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo, anasema kuanzia mwaka 2032, Dar es Salaam itahitaji maji lita bilioni moja kwa siku.

"Tunataka kuongeza uwezo wa Mto Ruvu, ndio maana tunataka kujenga bwawa linaloitwa Kidunda, liwe linasaidia kuongeza kasi katika Mto Ruvu, wakati wa kiangazi linafunguliwa maji yanaingia Mto Ruvu. Hiyo ndio mipango kwa Jiji la Dar es Salaam," anasema Profesa Mkumbo.

"Lakini mwaka 2030 hadi 2035, lazima serikali tufikirie kutumia maji ya bahari ila ukitumia maji ya bahari kwa sasa hivi lazima gharama ya maji ipande Dar es Salaam kutoka Sh. 1, 600 kwa lita hadi Sh. 12, 000," anasema.

Anasema, ili kulinda vyanzo mabondeni, serikali ilitunga sheria ya ada ya kutumia maji kwa wenye viwanda maeneo ya bondeni, ingawa haikutekelezwa kutokana na changamoto mbalimbali.

Profesa Mkumbo anasema, baada ya mazungumzo inatarajiwa viwanda vilivyopo kama ukanda wa Ziwa Victoria na vya Dar es Salaam vitalipia Bonde la Wami/Ruvu.

Mwakilishi wa wamiliki viwanda, Hussein Suphian, anaunga mkono malipo, kwani kwa viwanda vyote duniani, maji ni rasilimali muhimu katika uzalishaji.

**Ubora wa Maji**

Waziri Mbarawa, anasema serikali itahakiki ufuatiliaji wa ubora wa maji yanayosambazwa katika Halmashauri, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, taasisi na vyanzo vya maji vinavyomilikiwa na watu binafsi.

Jumatatu wiki hii akiwa mkoani Rukwa, Rais John Magufuli, alichukua hatua kali za kinidhamu na kisheria, dhidi ya hujuma zinazofanyika katika vyanzo vya maji mkoani humo, akimwagiza Profesa Mbarawa kubaki baada ya ziara kufuatilia utekelezaji.

Anasema, takwimu za maji hadi Aprili mwaka huu, kuna sampuli 4,165 zilizokusanywa na kufanyiwa uchunguzi na matokeo asilimia 91 zilikidhi viwango na zilizobaki zilikuwa na vimelea vya wadudu na madini.

**Victoria/ Tanganyika**

Hivi sasa serikali inatekeleza mradi wa maji katika Ziwa Tanganyika utakaohudumia wakazi wa maeneo pembezoni mwa ziwa na hadi mwezi Aprili, Waziri anaeleza mtaalamu mshauri ameshawasilisha taarifa ya upembuzi yakinifu kuhusu athari za kimazingira na kijamii.

Ni mradi unaotekelezwa katika mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi na utahusisha vijiji 73 vya wilaya za Kigoma, Uvinza, Nkasi, Kalambo, Mpimbwe na Mpanda.

Pia anasema serikali imepanga mradi wa maji Ziwa Victoria, utakaohudumia wakazi wa pembezoni mwa ziwa na mtaalamu mshauri anaendelea na sanifu katika vijiji vitakavyonufaika.

"Usanifu utakapokamilika, ujenzi wa mradi utaanza na utanufaisha jumla ya vijiji 301 vilivyopo pembezoni mwa Ziwa Victoria katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Simiyu," anasema.

**Jijini Dodoma**

Profesa Mbarawa anasema, serikali inatekeleza mradi wa maji katika mji mpya wa serikali eneo la Ihumwa, ambao umegawanyika katika awamu mbili.

Awamu ya kwanza, inagharimu Sh. bilioni 3.6 iliyohusisha kupima maji ardhini; ujenzi wa tangi la kukusanya maji ujazo wa lita 200,000; tangi la lita milioni moja; na kuchimba visima saba.

Mengine anataja ni ulazaji bomba kuu la kilomita 4.5 kutoka maji yanapokusanywa hadi kunakohifadhiwa; kununua pampu na kujenga pa kuhifadhi mitambo; kufunga transfoma na kupeleka umeme visimani.

Anasema, mkakati wa muda mrefu wa kupata maji ya uhakika Dodoma mjini, unahusu ujenzi wa bwawa la Farkwa, wilayani Chemba, litakalokuwa chanzo kikuu ikitarajiwa kuongeza maji kwa ujazo lita milioni 120 kwa siku, kwa ajili ya wakazi zaidi ya milioni moja.

**RC Pwani**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, anasema wakati Dar es Salaam inategemea maji ya Ruvu Juu na Chini, Dawasa ipo kwenye mchakato wa kutumia maji ya Rufiji kama chanzo chake kingine.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Luhemeja, anathibitisha kwamba kamati imeshaundwa kushughulikia hilo akifafanua: "Tumetumia fursa ya bwawa la Rufiji linalojengwa na sisi tutajenga mtambo mkubwa wa maji kutoka Rufiji... Tumeshawasiliana na wadau wetu Tanesco ambao ndio wenye bwawa."

Pia anasema wameshafanya mawasiliano na mkandarasi rasilimali wa bwawa na wakala wa barabara Tanzania (Tanroads) kuhusu ujenzi wa mtambo wa maji.

"Mwakani tutawasilisha hoja Bodi ya Dawasa kwa ajili ya kupata kibali, kisha upembuzi yakinifu ufanyike na kazi ianze, mtambo utajengwa kwa gharama ya takribani Sh. bilioni 200 ambazo ni fedha za ndani. Mradi utaanza Julai mwakani na utatumia miaka mitatu kukamilika," anasema.

• ***Mwandishi anapatikana kwa simu: (+255) 0658 141286; barua pepe: fmonyo7@gmail.com***



# Maagizo mazito kwa mamlaka za maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, ameziagiza mamlaka zote za maji nchini kutenga fedha kutoka kwenye mapato yake ya ndani kwa ajili ya miradi ya maji, ili kupanua huduma za upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Prof. Mkumbo alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya, huku akiwataka wafanye kazi kwa bidii kuhakikisha wanatoa huduma inayokidhi mahitaji ya wananchi.

Alisema utaratibu huo pia utasaidia mamlaka hizo kukabiliana na uhaba wa maji ambao unaweza kutokea kwenye maeneo yao.

"Naziagiza mamlaka zote za maji kuanzia sasa zianze kutenga fedha kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya miradi mipya ya maji itakayokuwa inaanzishwa kwenye maeneo yao," alisema Pro. Mkumbo. Alisema katika utekelezaji wa agizo hilo, mamlaka hizo zinapaswa kufungua akaunti maalum kwa ajili ya kuhifadhi fedha hizo na pia kutumiwa na wadau katika kuchangia miradi ya maji ambayo itasaidia kuboresha huduma kwa wananchi. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Ndele Mengo, alisema kwa sasa mamlaka yake inatumia zaidi ya shilingi bilioni tatu kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani kutekeleza mradi wa maji katika mji mdogo wa Mbalizi.

Alisema mradi huo wa kupeleka maji katika mji mdogo wa Mbalizi ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa wakati wa ziara yake mkoani Mbeya kwa ajili ya kuwapatia maji wananchi wa mji huo. Mengo alisema mpaka sasa mradi huo umekamilika kwa asilimia 53 na kwamba baada ya miezi miwili kuanzia sasa mradi huo utakuwa umekamilika kwa asilimia 100 na wananchi wataanza kupata maji.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya, Dk. Lwitiko Mwakalukwa, alisema uwezo wa vyanzo vya maji vinavyohudumia wakazi wa Jiji la Mbeya unazidi kupungua.

Alisema kwa sasa mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Mbeya ni lita za ujazo 60,000 kwa siku, lakini uzalishaji wa maji kwa kutumia vyanzo vilivyopo ni lita za ujazo kati ya 40,000 na 48,000 kwa siku kiwango ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji ya wananchi kwa asilimia 100.

Dk. Mwakalukwa alishauri kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Kiwira kwa kutumia vyanzo vya ndani ili kuongeza uwezo wa mamlaka kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Mbeya.

# Agizo la Chalamila latekelezwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SIKU moja baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuliagiza Jeshi la Polisi kumkamata mkandarasi aliyejenga daraja la mto Simba linalounganisha Kata za Tembela, Mwasanga na Mwakibete lilliovunjika na kuua watu watano, utekelezaji wake umeanza mara moja.

Chalamila alitoa maagizo ya mkandarasi kukamatwa juzi alipotembea kuangalia namna daraja hilo lilivyovunjika na kusababisha madhara baada ya kubaini lilijengwa chini ya kiwango. Katika maelezo yake Chalamila alisisitiza daraja hilo halikujengwa kwenye viwango vinavyotakiwa ndio maana lilibomoka na kusababisha maafa.

"Haiwezekani mvua ya kwanza tena ya saa tatu hadi nne ibomoe daraja kubwa namna hii, lazima kuna uzembe mahali sasa naliagiza Jeshi la Polisi kumtafuta mkandarasi aliyejenga daraja hili atueleze kwa nini limebomoka," alisema Chalamila.

Aidha, Chalamila alitoa pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu zao kufuatia maafa hayo na kwamba serikali itatoa rambirambi ya Sh. 500,000 kwa kila familia kama mkono wa pole.

Kufuatia maagizo hayo ya Mkuu wa Mkoa, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa, Ulrich Matei, aliwaambia waandishi wa habari kuwa mkandarasi huyo aliyefahamika kwa jina la Elishadai amepatikana na kwamba muda wowote ataripoti polisi.

Alisema tangu maagizo hayo yatolewa na Mkuu wa Mkoa, kwa kushirikiana walifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha mkandarasi huyo anapatikana.

Diwani wa Tembela, Anderson Ngao, alisema kata yake imepoteza watu wanne katika ajali hiyo.

Alisema licha ya kupoteza ndugu na jamaa lakini pia shughuli za uzalishaji mali zimesimama baada ya mawasiliano ya daraja kukatika kwani wafanyabiashara wanashindwa kusafirisha bidhaa na mazao yao kutoka eneo moja hadi lingine.




Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), Mkoa wa kihuduma Kibaha, wakiendelea na ukarabati wa bomba la inchi tatu lililoharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo ya Vitendo, Kata ya Misugusugu wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani jana. Bomba hilo linahudumia takribani kaya 50. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji sasa waomba vifaa vya kinga

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WACHIMBAJI wadogo wa madini katika Mji wa Mkwajuni, Halmashauri ya Wilaya Songwe wameiomba serikali kusaidia upatikanaji wa vifaa kinga ambavyo vitawasaidia kuwakinga dhidi ya athari zinazotokea kwenye shughuli za uchimbaji dhahabu.

Walitoa ombi hilo juzi, walipozungumza na Nipashe ambapo walidai wanafanya kazi kwenye mazingira magumu na hatari kwa afya yao kwa sababu vifaa vya uchimbaji wanavyovitumia ni hatari.

Walisema licha ya kuwa wanatambua matumizi ya zana holela kwenye shughuli za uchimbaji dhahabu yana madhara, hivyo wameshindwa kumudu gharama za kununulia mashine za kisasa kwa ajili ya uchimbaji.

Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo wa madini Mkoa wa Songwe, Emmanuel Kamaka, alisema matumizi ya zebaki katika shughuli za uchimbaji madini ni hatari kwa afya zao, hivyo uwapo wa vifaa kinga utasaidia kupunguza madhara yanayopatikana.

"Tunaomba serikali itusaidia vifaa kinga katika shughuli zetu za uchimbaji kama itashindwa kutununulia basi watusaidie kutafuta wakala ambaye atakuja hapa mkwajuni kutuuzia tupo tayari," alisema Kamaka.

Mbali na kuiomba serikali kuwanunulia vifaa tiba, pia alieleza kufurahishwa na mafunzo ya afya na usalama kwenye maeneo yao ya migodi ambayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha).

Alisema mafunzo hayo yamewasaidia kujifunza masuala mbalimbali ya kujilinda na kukabiliana na athari zinazotokea wakati wa shughuli za uchimbaji wa dhahabu.

Alisema wachimbaji hao hawajawahi kupata mafunzo yoyote ya usalama na afya katika migodi yao, hivyo aliipongeza Osha kwa kuandaa utaratibu huo na kuwaomba kuwatembelea mara kwa mara kutoa elimu hiyo ambayo ina manufaa kwao.

Mwanaidi Sembo alieleza wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu hususani wanawake wanavyokabiliwa na changamoto ya vifaa.

Alisema vifaa vinavyotumika kwenye shughuli za uchimbaji kama kole na sululu sio rafiki kwao na kuiomba serikali kuandaa utaratibu mwingine wa namna ya kuwapatia vifaa vizuri ambavyo vitarahisisha shughuli za uchimbaji. Meneja Afya Osha, Jerome Materu, katika mafunzo hayo alitoa tahadhari kwa wachimbaji hao kuachana na matumizi ya zebaki kwani ni hatari kwa afya zao.

Materu alisema vitu hivyo vinasababisha madhara makubwa kwenye mwili wa binadamu ikiwamo vilema vya miguu na mikono, hivyo kushindwa kutembelea na kurithisha kizazi chake. "Matumizi ya zebaki ni hatari kwa afya, hivyo nawasihi wachimbaji mwachane na vitu hivyo tafuteni teknolojia nyingine ya kupata madini hata kama ni bei ghali, lakini bora kununua ili kuokoa maisha yako na kizazi chako," alisema Materu.



## HABARI DODOMA

# Serikali kukabiliana magonjwa yasiyoambukiza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, amesema zaidi ya theluthi moja ya vifo vinavyotokea hospitali vinatokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Kufuatia hali hiyo, serikali inatarajia kuja na mpango mkakati wa kudhibiti magonjwa yasiyoambukizwa ifikapo Novemba mwaka huu utakaokuwa shirikishi kwa jamii ili kukabiliana na tatizo hilo.

Dk. Chaula alitoa kauli hiyo juzi wakati akizindua ripoti ya mpango mkakati wa nne wa sekta ya afya nchini katika mkutano wa 20 wa wataalamu wa sekta hiyo, jijini hapa.

Alisema magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya afya na yamekuwa yakiigharimu serikali fedha nyingi kutibu wananchi.

Alibainisha kuwa kuna umuhimu wa jamii kuhakikisha wanafuata ulaji wa vyakula vinavyofaa ili kupunguza magonjwa yasiyoambukizwa.

"Kutokana na magonjwa haya kutibiwa kwa gharama kubwa na hivyo kuigharimu serikali, tutakuja na mpango wa kudhibiti hilo na mpango wetu huu utaanza Novemba mwaka huu," alisema.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuwapo mafanikio kwenye sekta ya afya bado kuna haja ya wadau na watendaji wa Wizara ya Afya na Tamisemi kushirikiana ili kufikia malengo.

Alisema serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa katika kuboresha sekta ya afya na kusisitiza haja ya wadau na watendaji kushiriki ili juhudi hizo ziweze kuleta matokeo chanya katika sekta hiyo.

Akitoa maelezo ya tathmini ya Mpango huo, Dk. Catherine Joackim, alisema asilimia 36 ya vifo vilivyotokea hospitalini kwa mwaka 2018, vimetokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, huku vifo sita kati ya 10 vinavyotokana na magonjwa ya kuambukiza.

Alisema mwaka 2015-2018 kumewapo na mafanikio makubwa katika suala la matumizi ya njia za kisasa za mpango wa uzazi, chanjo wa wajawazito, huduma za kujifungua na baada ya kujifungua ambao umeonyesha katika kila mkoa na mafanikio zaidi yako katika mikoa iliyoko katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

"Inaonyesha kuna mafanikio katika mikoa yote kwa kuwapo na ongezeko kubwa kwa wajawazito kuhudhuria kliniki kabla na baada ya kujifungua ambayo imeongezeka kutoka asilimia 37 hadi kufikia asilimia 61, waliojifungua kwenye vituo vya afya wameongezeka kutoka asilimia 65 hadi kufikia asilimia 77 na wale waliokwenda kliniki siku mbili baada ya kujifungua imeongezeka kutoka asilimia 42 hadi asilimia 66," alisema.

Alieleza tathmini hiyo inabainisha kuwa pamoja na kupungua kwa vifo vya watoto, lakini bado idadi ya vifo vya watoto wachanga wanaokufa chini ya mwezi mmoja ni kubwa mijini hususani katika Jiji la Dar es Salaam.

"Kwa upande wa chanjo kwa watoto wachanga inaonyesha kufanya vizuri, watoto tisa kati ya 10 wamepata chanjo," alisema.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Ntuli Kapologwe, alisema katika mkutano huo wataangalia huduma gani zinatakiwa kuboreshwa pamoja na kuangalia namna ya kuboresha huduma za mama na mtoto.

Pia alisema wataangalia mwelekeo wa kupunguza vifo vya mama na mtoto, magonjwa yasiyoambukiza pamoja na kufanya mapitio ya nini kifanyike pamoja na maandalizi ya mkakati mwingine wa tano.

Dk. Kapologwe alisema serikali imefanikisha ujenzi wa vituo vya kutolea huduma 486, vituo vya afya 320, zahanati 76 na hospitali za wilaya 67.



Wakazi wa Mtaa wa Surugai, Kata ya Ipagala, mkoani Dodoma wakiangalia gari lililotumbukia kwenye mfereji wa maji kutokana na kufeli breki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Azaki zatakiwa kupitia malengo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

ASASI za Kiraia (AZAKI) zimetakiwa kufanya mapitio ya malengo yao ili yaendane na ya serikali iliyopo madarakani.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Happiness Mgalula kwa wakurugenzi 80 wa azaki katika mkutano wa kujadili uhusiano baina ya serikali na asasi za kiraia kuhusu maendeleo ya nchi.

Mgalula alizitaka asasi zote zenye mapenzi mema na serikali kufanya mapitio ya kina ya malengo, shughuli na matumizi yake, ili yaendane na vipaumbele vya serikali. Alisema ni vyema asasi hizo zikasikiliza na kuelewa mwelekeo wa serikali ya awamu ya tano katika vita ya kiuchumi badala ya kusikiliza maelekezo ya mashirika ya nje yasiyokuwa na mapenzi mema na Tanzania.

"Nchi ipo kwenye vita ya kiuchumi, hivyo watu binafsi na taasisi mbalimbali zinapaswa kuelewa amri ya serikali iliyopo madarakani," alisema.

Alieleza kuwa asasi hizo ni sehemu muhimu ya ushindi na zinapaswa kupigana upande wa serikali na kuitikia amri ya Amiri Jeshi Mkuu mmoja na kama wataitikia amri ya jeshi la nje watasababisha kupigwa.

Naye Dk. Ajali Nguyahambi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), akitoa mada katika kikao hicho kuhusu ubia wa maendeleo, alisema ili ubia ufanikiwe uelewa mpana ufanyike wa mipangilio ya kitaifa na changamoto za kisera.

# Vyama vitatu vya ushirika kuanzishwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini, inatarajia kuanzisha vyama vitatu vya ushirika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ili kusaidia wakulima wa zao la pamba.

Mikoa ambayo itakuwa na vyama hivyo ni pamoja na Geita (GCU), Shinyanga (KAKUA) na Simiyu (SIMKU).

Hayo yalibainishwa na Kaimu Mrajisi wa Tume hiyo, Edmund Masawe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa vyama vya ushirika nchini.

Alisema vyama hivyo awali vilionekana kulegalega kwa sababu mbalimbali, lakini hivi sasa serikali ya awamu ya tano inasisitiza suala la viwanda hivyo wamejipanga kuhakikisha vyama hivyo vinachukua jukumu la kufanya kazi hiyo kwa ufanisi na kuwainua wakulima wa zao hilo.

Alieleza kuwa lengo lao ni kuona vyama vyote vinakuwa na mwamko wa kufanyakazi za uchambuaji, ubanguaji na uchakataji wa mazao mbalimbali ili kusaidia wakulima kuwa na mwelekeo katika uuzaji wa mazao yao.

Alifafanua kuwa kwa upande wa Geita chama hicho cha ushirika wataungana na Chato ili kuwa na ushirika mmoja na kupanua wigo wa ufanyaji kazi zake.

"Mwakani tumejipanga vyama hivi vianze kazi ya kuchambua pamba tunahitaji kuona zoezi hilo linafanyika kiufasaha tofauti na ilivyo sasa," alisema Masawe.

Alisema imefika wakati sasa jamii inapaswa kujua umuhimu wa vyama vya ushirika na kujua nini vinafanya ili kuleta maendeleo kwa jamii.

Hata hivyo, alisema kuna vyama vingi vya ushirika ambavyo vinafanya kazi vizuri kama vile cha Kagera na Kilimanjaro ambavyo vinatumika kwa ajili ya kuchambulia kahawa na kwamba kutokana na mikakati waliojiwekea watahakikisha vyama vyote vinafanya kazi kama ilivyoelekezwa.

"Tunatakiwa tutoe elimu kwa jamii kuhusu nini maana ya ushirika tukifanya hivyo naamini wananchi watalewa suala hilo," alisema Masawe.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Tume hiyo, Ntambi Bunyazu, alisema wana kila sababu ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu vyama vya ushirika kwa sababu wengi wanaona haina umuhimu.

Alisema moja ya changamoto wanazokutana nazo ni pamoja na kutokuwapo na uelewa kwa wananchi kuhusiana na vyama hivyo.





# Mvua na upepo mkali vyaharibu nyumba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NYUMBA 15 za wananchi wa kijiji cha Kikungwi Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, zimeharibiwa vibaya na upepo mkali ulioambatana na mvua zinazoendelea kunyesha na kuwaacha baadhi ya wananchi kukosa makazi

Upepo huo uliovuma juzi mchana pia umeharibu miundombinu ya umeme, kukatika na kung'oka kwa miti na baadhi ya mazao mashambani kuharibika.

Kutokana na maafa hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayuob Mohamed Mahamoud, aliwatembelea waathirika na kuwataka kuwa na moyo wa subira na uvumilivu wakati serikali ikiendelea na taratibu za kufanya tathmini ili kujua namna gani ya kuwasaidia.

Alisema kwa hatua ya awali, serikali itahakikisha inawapatia msaada wa makazi na chakula hadi pale makazi yao ya kudumu yatakaporejea katika hali ya kawaida.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati, Hamida Khamis Mussa, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuwa na tahadhari na kutokaa chini ya miti katika kipindi hiki cha mvua na upepo mkali ili kuepukana na maafa yanayoweza kujitokeza.

Baadhi ya wananchi waliokumbwa na maafa hayo walisema wameshtushwa na hali hiyo ambayo walidai hawajawahi kuiona kwa kipindi kirefu huku wakisema wanamshukuru Mungu kwa kutokutokea vifo.

Waliiomba serikali kuwasaidia kwa hasara walioipata sambamba na kuipongeza serikali ya mkoa na wilaya kwa kufika mapema baada ya kupata taarifa hiyo.

Sheha wa Kikungwi, Mohammed Haji Ushahidi, alisema uongozi wa shehia hiyo utaharakisha tathmini kwa kushirikiana na maofisa wa mkoa na wilaya ili kuziwasilisha serikalini.

Upepo huo uliovuma kwa muda wa dakika 15 katika kijiji cha Kikungwi umeharibu takriban maeneo manne ya shehia hiyo.



Wakazi wa eneo la Ngwaru Kanisani wilayani Muheza, wakiangalia nyumba zilizozingirwa na maji ya mafuriko katika eneo la daraja la Ngwaru jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Balozi Iddi awapa CCM somo zito

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali imepiga hatua kubwa katika kutekeleza dhana ya utawala bora ikiwamo kuundwa kwa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi (Zaeca), Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Suleiman alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya ripoti ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kusema mafanikio hayo yamesaidia viongozi na watumishi wa umma kuwa na nidhamu kazini.

Alisema hiyo ni mara ya tatu kwa tume pamoja na mamlaka ya kuzuwia rushwa kuwasilisha taarifa mbele ya Baraza la Wawakilishi na kujadiliwa.

Pia alisema taarifa za taasisi hizo awali huwasilishwa ripoti yake mbele ya Rais na baadaye katika Baraza la Wawakilishi.

"Tumepiga hatua kubwa katika kutekeleza dhana ya utawala bora. taasisi zinazoshughulikia rushwa na uhujumu wa uchumi pamoja na maadili, zote zimewasilisha ripoti zao kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein." Alisema.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa umma wakiwamo wateuliwa wa Rais na watendaji wa mashirika na taasisi za serikali kujitayarisha kuwasilisha fomu za maadili ya viongozi na kutangaza mali zao.

Alisema fomu hizo kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi ni lazima na zinatakiwa zijazwe kabla ya kumalizika kwa Desemba, mwaka huu.

Suleiman alisema kwa mujibu wa ripoti ya Tume ya Maadili ya Viongozi katika mwaka 2018/9 fomu zilizowasilishwa ni 1,702 sawa na asilimia 103, huku viongozi waliowasilisha kwa wakati ni 1,672.

Alisema ripoti hiyo imebainisha kwamba wako viongozi wa serikali bado hawajarejesha fomu hizo kwa wakati na hilo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

"Tunawataka wale viongozi 26 walioshindwa kuwasilisha fomu za maadili sasa wawe wa mwanzo kurejesha fomu hizo kwa wakati kabla ya Desemba 31, mwaka huu," alisema.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeundwa chini ya Sheria Na.4 ya mwaka 2015, huku ikipewa majukumu ya kusimamia taarifa na kazi za kujaza fomu za tamko la mali na madeni kwa viongozi wa serikali wakiwamo walioteuliwa na Rais na watendaji wa taasisi za umma.

# SMZ kununua pilipili hoho kwa wakulima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema kuanzia sasa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) litachukua jukumu la kununua zao la pilipili hoho kutoka kwa wakulima.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, wakati akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu mikakati ya serikali ya kuimarisha mazao ya viungo nchini.

Hafidh alisema mazao ya viungo soko lake lipo la uhakika na kazi kubwa iliyopo sasa ni wakulima kuongeza bidii ya kuzalisha mazao hayo ikiwamo pilipili hoho.

Aliyataja mazao ya viungo ambayo soko lake ni la uhakika hivi sasa kuwa ni pamoja na pilipili manga, vanila na hiliki.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumepata soko la uhakika la kuuza bidhaa zinazotokana na viungo ikiwamo pilipili manga, pilipili hoho na vanilla," alisema.

Kutokana na uhakika wa soko kwa mazao hayo, Hafidh aliwataka Wawakilishi kuwahamasisha wakulima vijijini kuongeza kasi ya uzalishaji.

Alisema tayari mradi wa kuzalisha pilipili kichaa huko Panga Tupu Mkoa wa Kaskazini Unguja umeanza kuleta mafanikio baada ya wakulima kuotesha ekari 15 za aina hiyo ya pilipili.

"Soko kubwa la mazao ya viungo lipo katika nchi za Bahari ya Hindi pamoja na Arabuni na sasa limepanuka hadi China," alisema.

# Ushauri serikali kuomba fedha kudhibiti tabianchi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KUTOKANA na athari za mazingira nchini, serikali imetakiwa kutumia fursa ya mfuko kupambana na mabadiliko ya tabianchi (GCF) ulioanzishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) ambao kila mwaka umekuwa ukitenda wastani wa dola za kimarekani bilioni 10 hadi 50 kwa ajili ya nchi zinazoendelea.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Shirika linalohusika na Mazingira na Kupamba na Umaskini (FEMAPO), Mathias Lyamunda, wakati akiwasilisha taarifa ya Mfuko wa GCF kwenye kongamano la uwezeshaji wa jinsia wenye malengo katika kushiriki kwenye mabadiliko ya tabianchi.

Kongamano hilo lililoshirikisha asasi na taasisi za kiserikali liliandaliwa na shirika linalojishughulisha na kumuinua mwanamke na kusimamia masuala ya mazingira (Wated) lililofanyika mjini Morogoro, lililenga kutoa chachu kwa serikali na asasi hizo kutumia fursa za mfuko huo ili kupata fedha zitakazosaidia kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Lyamunda alisema GCF una fursa kubwa ya fedha za kusaidia mabadiliko ya tabianchi, huku ukiweka kipaumbele kwa wanawake ambao ndio wameguswa na kuathiriwa na mabadiliko hayo ikiwamo kwenye nyanja za kilimo, maji na nishati.

Mwanamazingira nguli na mtetezi wa wanawake ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu, Fatma Toufiq, alisema Tanzania kuna athari za mabadiliko ya tabianchi, lakini mpaka sasa hakuna wanaotambua kuwapo kwa athari hizo.

Alisema wanawake mpaka sasa ndio wamekuwa watumiaji wakubwa wa nishati kama kuni na mkaa ambao unachangia mabadiliko hayo na kuitaka serikali kuweka kipaumbele cha kutoa elimu juu ya matumizi mbadala ikiwamo gesi asilia na majiko banifu ili kupunguza athari hizo.

Alisema iwapo fedha zitapatikana kutoka GCF, zitasaidia asasi zinazojihusisha na mazingira kwa kushirikisha wanawake kutambua athari za mabadiliko ya tabianchi na kujua matumizi ya njia mbadala ya nishati.

Ofisa mazingira mwandamizi na mratibu wa mabadiliko ya tabianchi toka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Fredrick Mulinda, alisema kuwapo kwa GCF kunatoa fursa nyingine kwa serikali na asasi kuomba fedha hizo kwa ajili ya kasi ya kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira.



Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Simon Karikari, akijibu na kutatua maswali ya wateja wa Tigo katika kituo cha kisasa cha huduma kwa wateja, jijini Dar es Salaam jana, kama sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waajiri waelekezwa umuhimu mafunzo watumishi umma

**Na Mwandishi Wetu,** MEATU

SERIKALI imewataka waajiri nchini kuweka kipaumbele katika programu za mafunzo kwa watumishi wa umma ili kuwajengea uwezo kiutendaji kwa kuzingatia kanuni za maadili ya kiutendaji.

Wito huo ulitolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, wakati wa kikao kazi chake na watumishi wa umma wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, mkoani Simiyu.

"Waajiri hakikisheni mnatoa mafunzo kwa watumishi wenu ili kuendana na kasi ya sayansi na teknolojia pamoja na kuendana na kasi ya serikali," Mwanjelwa alisisitiza. Mwanjelwa alitoa wito huo baada ya kubaini kuwapo kwa uelewa mdogo wa masuala ya kiutumishi kwa baadhi ya watumishi wa umma wilayani humo.

"Nimegundua bado kuna ombwe la uelewa mdogo wa miiko ya kazi miongoni mwa watumishi wa umma unaosababisha kufanya kazi kwa mazoea, hivyo mafunzo yatawasaidia kuboresha utendaji kazi wao." Mwanjelwa.

Aidha, Mwanjelwa ameitaka Tume ya Utumishi wa Umma kuwa na utaratibu wa kujiridhisha kama waajiri wanawapeleka watumishi kupata mafunzo katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania ili wawe na ufanisi kiutendaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Fabian Manoza, alimshukuru Mwanjelwa kwa kufanya ziara wilayani hapo na kuahidi kutekeleza maagizo yote aliyoyatoa.

Mwanjelwa amehitimisha ziara yake ya kikazi mkoani Simiyu iliyolenga kuhimiza uwajibikaji kwa watendaji na watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na kusikiliza kero za watumishi hao na kuzitatua.

## Vita dhidi ya utapiamlo, udumavu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MAOFISA wa lishe idara mbalimbali mkoani Kagera, wanaendelea na shughuli za kupunguza viwango vya utapiamlo na udumavu unaopanda na kushuka. Kutokana na hali hiyo, wameainisha mipango ya upataji wa mahitaji shuleni. Lengo ni kuhakikisha hali ya udumavu katika mkoa huo inaondolewa na kuwa na taarifa nzuri ya lishe kwa watoto ambao bado wanahitaji makuzi bora.

Hayo yalielezwa katika uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji katika kikao cha kamati ya lishe cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/20 katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, ambapo Idara ya Elimu Msingi imeonekana kufanya vizuri katika suala la lishe.

Akitoa taarifa hiyo, Mkuu wa Idara ya Elimu Shule za Msingi, Gregory Fabian, alisema halmashauri hiyo ina jumla ya shule 151 kati ya hizo shule 141 za serikali na shule 10 za binafsi.

Alisema kati ya shule hizo, shule 33 zimeanzisha bustani za mboga na matunda na nyingine 139 zimepanda miti ya matunda kama embe, mipera na machungwa.

## Maonyesho Siku ya Chakula

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, amewataka wananchi kisiwani Pemba kufika katika maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani, ili kujifunza mambo yatakayowasaidia katika shughuli zao za ujasiriamali.

Maonyesho hayo yatafanyika Chamanangwe Wilaya ya Wete Mkoa wa Kusini Pemba kuanzia leo hadi Oktoba 16, mwaka huu, ambayo ndicho kilele cha Siku ya Chakula Duniani.

Akizungumza na waandishi wa habari, waziri huyo alisema wajasiriamali na wananchi kwa ujumla hupata uwelewa zaidi kwenye maonyesho kwa ajili ya kuimarisha shughuli zao za ujasiriamali, kutokana na kujifunza kwa vitendo, hivyo ni vyema kufika kwa wingi katika viwanja vya maonyesho.

"Kwa kweli maonyesho yanasaidia sana kukuza vipaji vya wajasiriamali na tumeona ni njia muhimu ya kufundisha, kwani hujifunza kwa vitendo," alisema waziri huyo.

Alieleza kuwa maonyesho yaliyofanyika mwaka jana kisiwani Pemba, yameleta matokeo chanya kwa wajasiriamali, kwani wamekuwa wakitumia mbinu walizofundishwa, jambo ambalo limesaidia kuimarika kwa uzalishaji katika shughuli zao za kilimo.

"Wajasiriamali wetu wamefanya mageuzi makubwa baada ya kupata elimu kwenye maonyesho ya mwaka jana, hivyo na mwaka huu tunatarajia wajifunze zaidi na mambo mapya," alisema.

## FBI yamtambua muuaji katili zaidi Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

SHIRIKA la Upelelezi la Marekani (FBI), limethibitisha kuwa mfungwa muuaji, Samuel Little, amekiri kuwaua watu 93 miongo minne iliyopita hivyo kuwa mhalifu hatari zaidi katika historia ya nchi hiyo.

Polisi imemhusisha Little na mauaji ya watu 79 katika matukio 50 ya uhalifu wa aina hiyo kutoka mwaka 1970 hadi 2005 kufikia sasa.

"Little tangu mwaka 2012 amekuwa akitumikia kifungo cha maisha gerezani baada ya kupatikana na kosa la mauaji ya wanawake watatu weusi ambao baadhi yao walikuwa makahaba na watumiaji wa dawa za kulevya," maofisa walisema.

Bondia huyo wa zamani alikuwa akiwapiga ngumi waathiriwa wake kabla ya kuwanyonga, kumaanisha mara nyingi hakuna ushahidi wa "kuthibitisha" kuwa mtu aliuawa kikatili.

Shirika hilo lilisema baadhi ya vifo hivyo havikuchunguzwa na FBI na vingine vilidhaniwa kutokana na ajali au sababu zingine na kwamba miili mingine haikuwahi kupatikana.

Katika taarifa yake ya siku ya Jumatatu, FBI ilisema wachunguzi wake wanaamini ushahidi wake "wote ni wa kweli".

"Kwa miaka mingi, Samuel Little aliamini hatawahi kujulikana kwa sababu hakuna mtu aliwatafuta waathiriwa," mchambuzi wa masuala ya uhalifu wa FBI, Christie Palazzolo alisema katika taarifa hiyo.

"Japo tayari ni mfungwa, FBI inaamini ni muhimu kuwatafutia haki waathiriwa wa karibu kila kesi."

Maofisa wa usalama bado wanachunguza visa 43 vya mauaji aliyokiri kutekeleza.

Maofisa sasa wametoa habari zaidi kwa umma kuhusu visa vitano vya mauaji yaliotekelezwa katika miji ya Kentucky, Florida, Louisiana, Nevada na Arkansas ili kusaidia utambuzi wa waathiriwa ambao hawajathibitishwa.

Shirika hilo awali lilisambaza michoro ya waathiriwa wa mauaji ya Little, ambayo alichora akiwa gerezani katika juhudi za kuwatambua waathiriwa zaidi.

Pia walichapisha kanda fupi za video wakati wakimhoji hasa sehemu aliyoelezea kwa kina jinsi alivyotekeleza mauaji hayo.

Katika moja ya matukio matano yaliyochunguzwa, FBI inaomba ushirikiano wa umma kumtambua mwanamke mwenye asili ya Kiafrika kwa jina Marianne au Mary Ann aliyeishi Miami na Florida, mwanzoni mwa miaka ya 70.

Little alielezea jinsi alivyomuua mwanamke huyo wa miaka 19, karibu na shamba la miwa na kisha mwili wake kuuburuta na kuutupa katika shamba hilo.

**BBC**

# UN yakabiliwa ukata kuwalipa wafanyakazi

**GENEVA, Uswisi**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amesema umoja huo unakabiliwa na 'mzozo mbaya zaidi wa fedha' kwa karibu muongo mmoja kwa sababu nchi wanachama 64 kati ya 193 hazijalipa michango yao ya kila mwaka.

Akizungumza na waandishi habari, Msemaji wa Umoja wa Mataifa, Stephane Dujarric, alisema kuwa, Katibu huyo wa UN, ameziandikia barua nchi zote wanachama kuwajulisha kuwa umoja huo uko katika hatari ya kuimaliza akiba yake ifikapo mwishoni mwa mwezi huu.

Guterres amezitaja nchi hizo kuwa ni pamoja na Marekani ambayo ndiyo mchangiaji mkubwa wa Umoja wa Mataifa.

Alitaja nchi nyingine ambazo hazijalipa ada ya mwaka ni pamoja na Brazil, Iran, Israel, Mexico, Korea Kusini, Saudi Arabia, Uruguay, Venezuela na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC).

Dujarric alisema iwapo fedha hizo hazitatolewa, umoja huo utashindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi wake na wanaotoa huduma.

Dujarric alisema hadi jana, nchi 129 zimelipa Dola bilioni 1.9 kama ada zao kwa mwaka 2019.

"Mwanachama aliyelipa fedha zote hivi karibuni ni Syria ambayo ndiyo inafikisha idadi ya nchi 129. Hadi sasa nchi wanachama wamelipa Dola bilioni 1.99 kuelekea katika tathmini ya bajeti ya kawaida ya mwaka 2019. Kiasi ambacho bado hakijalipwa mwaka huu ni Dola bilioni 1.3,'" alifafanua Dujarric.

Alisema hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Septemba, nchi wanachama zilikuwa zimelipa asilimia 70 ya fedha ya jumla ya bajeti ikilinganishwa na asilimia 78 katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita.

Katibu Mkuu huyo wa UN, alisisitiza kwamba mzunguko wa fedha ni tatizo ambalo limekuwa likijirudia na Umoja wa Mataifa hauna budi kwa sasa kuhakikisha matumizi yake yanaendana na kiwango cha fedha kilichopo, hali inayodhoofisha mamlaka na majukumu yake kwa watu wanaowahudumia.

Dujarric alisema kwa sababu umoja huo unaweza ukakosa fedha za kuwalipa wafanyakazi wake ifikapo mwishoni mwa Novemba, Guterres ameomba hatua za haraka zichukuliwe ikiwamo kupunguza safari za kikazi, kuahirisha manunuzi ya bidhaa na huduma, kusitisha shughuli zilizopangwa nje ya muda rasmi wa kazi na kwamba mikutano inaweza kuahirishwa au huduma zikabadilishwa.

Hata hivyo, kulingana na kalenda ya bajeti ya serikali ya Marekani, nchi hiyo kwa kawaida huwa inalipa mchango wake Oktoba.

Umoja wa Mataifa umesema unaidai Marekani Dola milioni 674 kwa mwaka 2019 na Dola milioni 381 kwa ajili ya bajeti za kawaida zilizopita.

Marekani pia haijatoa malipo ya bajeti tofauti kwa ajili ya shughuli za kulinda amani za Umoja wa Mataifa.

***DW***




Ikulu ya White House imetangaza kusimamisha ushirikiano na kile ilichokitaja kuwa uchunguzi unaofanywa kinyume cha sheria unaotekelezwa na wabunge wa chama cha Democratic ili kumng'atua mamlakani Rais Donald Trump. **PICHA: AFP**

# Tanzania, Kenya zaongoza idadi ya mabilionea EAC

**PORT LOUIS, Mauritius**

KENYA na Tanzania zinaongoza kwa idadi ya watu matajiri katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kulingana na ripoti ya utafiti ya mwaka 2019.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo kuhusu utajiri barani Afrika iliochapishwa Septemba na Benki ya AfrAsia, Kenya inaongoza ikiwa na mabilionea 356, ikifuatiwa na Tanzania ambayo ina mabilionea 99.

Uganda imeshika nafasi ya tatu yenyewe ikiwa na matajiri 67, huku Rwanda ikifunga orodha hiyo kwa kuwa na mabilionea 30.

Ripoti hiyo ilisema matajiri hao wana utajiri wa dola bilioni 10, na kwamba Tanzania ina tajiri mmoja wa dola bilioni moja.

Kwa Bara la Afrika, ripoti hiyo ilisema Afrika Kusini inaongoza kwa matajiri, ikiwa na mabilionea 2,169, Misri 932 na Nigeria wapo 531.

Hata hivyo, ripoti hiyo haitaji hata bilionea mmoja mbali na mali anayomiliki.

Katika miji mikuu, mji wa Nairobi unaongoza ukiwa na utajiri wa dola bilioni 49 mbele ya mji wa Dar es Salaam ambao umeorodheshwa kuwa wa 11 na una utajiri wa dola bilioni 24.

Mji Mkuu wa Uganda, Kampala una utajiri wa dola bilioni 16, huku Addis Ababa ikiwa na utajiri wa dola bilioni 14.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mabilionea wa Afrika ni asilimia 16 pekee ya idadi ya mabilionea wote duniani, huku Afrika ikiwa na asilimia moja pekee ya utajiri wote duniani.

Utajiri unaomilikiwa na bara hilo ni dola trilioni 2.2 kwa jumla ambapo asilimia 42 ya utajiri huo unamilikiwa na watu wenye utajiri wa kiwango cha juu au HNWIs.

Kwa ujumla mtu mwenye mapato ya kiwango cha kadri anayeishi Afrika ana mali inayogharimu dola 1,900.

Ripoti hiyo ilisema kuna matajiri 140,000 wanaoishi barani Afrika kila mmoja wao akiwa na mali yenye thamani ya dola milioni 10.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kuna takriban mamilionea 6,900 wanaoishi Afrika kila mmoja akiwa na mali yenye thamani ya dola milioni 10 ama zaidi na mabilionea 23 kila mmoja wao akiwa na mali yenye thamani ya dola bilioni moja.

***BBC***

# TMA yatahadharisha mvua kubwa

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imetoa tahadhari ya mvua kubwa zaidi kuanzia jana mpaka keshokutwa kwenye baadhi ya maeneo katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro na Zanzibar.

Tahadhari hiyo imetolewa ikionyesha kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo kwa mvua kubwa sambamba na mawimbi makubwa kwa siku tatu mfululizo.

Akizungumza jana, Meneja wa Huduma za Utabiri wa TMA, Samuel Mbuya, alisema tahadhari hiyo inaihusu mikoa ya Lindi na Mtwara.

"Kutokana na hali hiyo madhara tunayoyategemea ni pamoja na baadhi ya makazi kuzungukwa na maji, pia itaathiri usafiri kutokana na mawimbi na upepo, lakini pia usafiri wa nchi kavu utaathirika kutokana na miundombinu kuharibika," alisema Mbuya.

Aidha, alisema mamlaka husika pamoja na wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari kutokana na mvua hizo kubwa.

Mvua hizo zimetanguliwa na mvua zinazoendelea kunyesha kwenye baadhi ya mikoa ukiwamo mkoa wa Dar es Salaam.

Katika hatua nyingine, TMA kesho inatarajia kutoa utabiri wa mvua za vuli kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka.

Mikoa hiyo ni ya Kanda ya Kati, Nyanda za Juu Kusini na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dodoma.

Wananchi wameshauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA hasa katika kipindi hiki cha mvua.

.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya DCB, Godfrey Ndalahwa (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa akaunti maalum ya elimu ijulikanayo kama DCB Skonga, ikilenga kuwahamasisha wateja kuweka akiba kwa ajili ya elimu ya watoto wao. Wengine (kutoka kushoto) ni Balozi wa akaunti hiyo, Zamaradi Mketema, Mkurugenzi wa Biashara James Nhaluko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajipanga ongezeko la watu Dar

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI inajipanga kukabiliana na ongezeko la watu katika Jiji la Dar es Salaam ili liendane na mipango miji na ujenzi wa miundombinu.

Hatua hiyo inatokana na takwimu zinazoonyesha kuwa ifikapo 2030 jiji hilo litakuwa na zaidi ya watu milioni 10.

Akifungua kongamano la Siku ya Miji Endelevu Tanzania, lililoandaliwa kwa ushirikiano wa Ubalozi wa Ufaransa na Tasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini (Repoa), Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu, alisema ni lazima jitihada za kuwa na miundombinu na mipango miji sahihi zikafanyika sasa.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), George Simbachawene, alisema inahitaji maandalizi ya mifumo ya miundombinu na uwezo wa kuhimili kupokea watu wengi. "Bado Jiji la Dar es Salaama halijaweza kuhimili idadi kubwa ya watu, kwa sasa ikitokea mvua inakuwa ni changamoto kubwa, mifumo ya maji ya miundombinu hairuhusu shughuli za binadamu kufanyika, mvua kidogo maji yanajaa kila mahali," alisema.

Pia alisema ni lazima miji ikapangwa mapema ili kuhimili uwezo wa watu unaotakiwa na kwamba wadau mbalimbali wanapaswa kujadili namna ya kutatua na serikali kuongeza miradi itakayosababisha shughuli za kibinadamu ziweze kuendelea bila kusababisha majanga.

"Tuna miradi kwenye miji yetu inayoendelea yote hii ni kupangilia miji yetu, tuwe na mikakati ya miji mikubwa na midogo ili tuweze kupambana na ukuaji wa miji," alisema.

Naye Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema nchi hiyo imedhamiria kuchangia maendeleo ya miji endelevu barani Afrika na kwamba itakuwa kwenye kaulimbiu ya mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika na Ufaransa utakaofanyika Juni 4 hadi 6, mwaka 2020.

"Mkutano huo unalenga kutoa suluhisho na fursa za kuendeleza miji endelevu barani Afrika kwa kutoa nafasi kwa viongozi na wataalamu, utakuwa mkutano wa pekee utakaowaleta pamoja sekta binafsi, jumuiya ya wafanyabiashara na mashirika yasiyo ya kiserikali," alisema Balozi Clavier.

Alisema nchi za Afrika zinaongoza kwa matumizi ya nishati jadilifu ikiongozwa na Rwanda, na kwamba suala la kupambana na mabadiliko ya tabia nchi limebebwa kama jambo muhimu kwenye miradi yote inayotekelezwa na Ufaransa.

Alisema kwa mwaka 2018 jumla ya Euro bilioni moja zilielekezwa kwenye miradi mbalimbali na nchi hiyo imeweka mpango wa kuendeleza miji.

Naye Naibu Waziri wa Tamisemi, Mwita Waitara, alisema wanashirikiana na mamlaka mbalimbali kuhakikisha miji inapangwa kikamilifu katika uendelevu wake.

Alisema uwepo wa miji iliyopangiliwa vizuri na endelevu kutasaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato, ikiwamo kuwa makini kwenye utoaji wa vibali vya ujenzi na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Naye Mkurugenzi wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema ukishakuwa na mji unaokua kwa kasi kuliko miundombinu watu hawatapata huduma nzuri na wataingia katika uharibifu wa mazingira kutokana na kukosa rasilimali.

Alisema mafuriko ya mwaka 2018 yalisababisha hasara ya Sh. bilioni 230 hadi 500 kwa watu kupotea mali zao na uharibifu wa miundombinu na chanzo ni kukosa mipango thabiti na ongezeko la watu mijini ambao huamua kuvamia maeneo ya ardhi na kuishi.

## Apson Mwang'onda kuzikwa Jumamosi

**Na Mary Geofrey**

MWILI wa Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS), Apson Mwang'onda, unatarajiwa kuzikwa Jumamosi, huko kijijini kwao Vwawa, wilayani Mbozi mkoani Songwe.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na mtoto wake wa kwanza, Tomson Mwang'onda, mwili wa kiongozi huyo, utawasili leo saa 8:45 mchana kwa ndege kutoka Pretoria nchini Afrika ya Kusini.

Alisema mwili utalala nyumbani kwake Mbezi Beach jijini Dar es Salaam na Ijumaa watafanya ibada katika Kanisa la Mtakatifu Petro, Oysterbay, Kinondoni na shughuli za kuuaga.

Mwang'onda alifariki dunia Jumatatu. Alistaafu kuiongoza Idara ya Usalama wa Taifa Agosti 21, mwaka 2006 kwa mujibu wa sheria.

## Uandikishaji wapigakura

INATOKA UK. 8

Katika vituo vya Kata ya Msimbazi kwenye mitaa ya Mtambani Idrisa na Mwinyi Mkuu, wananchi walikuwa wanajitokeza mmoja mmoja.

Kadhalika katika Kata ya Magomeni, mitaa ya Makuti A, Sunna, Dossi na Makuti B, wananchi walionekana kujitokeza kwa kusuasua.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Baraza la Usuluhishi katika Kata ya Magomeni, Habiba Mondoma, alisema wanaamini baada ya mvua kumalizika wananchi wengi watajitokeza kujiandikisha.

Katika mitaa 16 iliyopo katika Kata ya Buyuni wilayani Ilala, mtaa wa Kigezi Juu uliopo katika Kata hiyo ya Buyuni, Saleh Salehe, alisema vituo vilifunguliwa mapema saa mbili asubuhi na watu walikuwa wamejitokeza kiasi.

"Sehemu nyingine ambako wananchi walikuwa wanajiandikisha ni katika ofisi za mtaa wa Nyegulu na Shule ya Msingi ya Nyegulu, Ofisi za Mtaa wa Tuliani.

Pia, Ofisi ya Mtaa wa Mgeule Juu, Ofisi za Serikali ya Mtaa wa Zavalana, Shule ya Msingi ya Zavala.

Mjumbe wa kamati ya siasa katika Kata hiyo ya Buyuni, Maliki Shemtandulo alisema hali bado si ya kuridhisha.

Waziri wa Ofisi ya Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza katika Mji wa Nyamanyere mkoani Rukwa katika ziara ya Rais John Magufuli, alisema uandikishwaji huo unatarajia kumalizika Oktoba 14. Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha ili wapate sifa ya kushiriki katika uchaguzi huo.

***Imeandaliwa na Agusta Njoji (Dodoma), Ashton Balaigwa (Morogoro) na Hamisi Nasiri (Mtwara)**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

KUITW A SHAURINI MD AI WA
(MGA/63)
Mahakama ya mwanzo ya UJIJI Wilaya ya KIGOMA
SHAURI LA MAD AI NO. 28 LA MW AKA 2019

Mdai: ES TER J. BU YO GERA
Mdaiwa: L UDO VICK JOHN BOSC O
Kwa: LU DO VICK JOHN BOSCO WA DA R ES SA LAAM

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba


Mdaiwa unadaiwa na mdai madai ya talaka.
Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 15 mwezi wa 10 mwaka 2019 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku hiyo iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea wito wa kuitwa shaurini mahakama hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 27/09/2019.

115455002

### VYETI VIMEPOTEA



**GERALDI CONRADI MATABARO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0769/0113/2015 kilichotolewa na MALAGARASI SEKONDARI mwaka 2015. Cheti cha Chuo chenye namba NS0769/0113/2015 kilichotolewa na KIBONDO SCHOOL OF NURSING mwaka 2018.
Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **KIG/KIB/RB/258970/2019.**

115453802

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 73 OF 2019

In the matter of the Estate of the late KEPHA JABU NDAGA of Mkonze within Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOSEPH NKAMBI NDAGA

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the …26… Day of …9….. 2019.
Dated at Dodoma this …5TH…. day of September, 2019.

115454602

IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 77 OF 2019

In the matter of the Estate of the late ENELESI KALOMBA
AND
In the matter of Application for letters of Administration by SALOCK MUSESE

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased's estate are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of petition for letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections (if any) to the grant should be filled on or before Day of 23rd October, 2019.

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 30th This day of September, 2019.

115454702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

FRANK ERNEST WILLIAM anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.445 DGG aina ya FUSO.

Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya Polisi: KAH/RB/TR/789/2019.

115454302

### KUPOTEA KWA CHETI



**Cosmas Nestory** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne kilichotolewa kwa mtahiniwa namba **S.2211/0053/2010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Mwilamvya.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi KAG/BUK/RB/257413/2019.

115454202

Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0767 223 311
Nipashe

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# SALAH ATAKUWA FITI KUIVAA MAN UNITED

**LIVERPOOL, England**

NYOTA wa Liverpool Mohamed Salah, ana matumaini makubwa ya kuwakabili Manchester United, kufuatia taarifa za jeraha lake kuleta ahueni kwa mashabiki.

Salah aliumia Jumamosi, wakati wa mchezo dhidi ya Leicester City, baada ya kuchezewa rafu na kiungo Hamza Choudhury, kitu ambacho kiliwashtua mashabiki wa Liverpool ambao wanahitaji kumwona akiendelea kuzichachafya ngome za timu pinzani msimu huu.

Majibu ya vipimo alivyofanyiwa mshambuliaji huyo, yameeleza kuwa hakuumia sana kama ilivyofikiriwa, na kwamba aliteguka kifundo cha mguu kwa kiasi kidogo.

Hata hivyo, mpaka sasa haijatangazwa ni lini Salah atarejea uwanjani, ila kinachoelezwa ni kwamba hatakuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu, na huenda akawa sehemu ya kikosi kitakachoikabili Manchester United.

Choudhury alionyeshwa kadi ya njano kutokana na rafu aliyomchezea Salah, huku Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akiamini kwamba lilikuwa ni tukio ambalo lilipaswa mchezaji huyo kupewa adhabu kali zaidi.

"Rafu za aina kama ile kwangu mimi, sitaki kumzungumzia huyo mchezaji tena, ila ilipaswa kuwa kadi nyekundu," alisema Klopp.

"Ilikuwa hatari sana. Kuna hatari nyingi, lakini hii ni moja ya hatari hizo. Sio kwamba nilitaka mchezaji atolewe kwa kadi nyekundu, la isipokuwa yalikuwa makosa ya makusudi yaliyolenga kuumiza."

Baada ya kupisha michezo ya kimataifa, majogoo wa Jiji, "Liverpool" watakua wageni wa Manchester United pale Old Trafford, Oktoba 20, mwaka huu.

## DELPH AONDOLEWA KIKOSI CHA ENGLAND

**LONDON, England**

KIUNGO wa klabu ya Everton, Fabian Delph ameondolewa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England, kilichoanza maandalizi ya kujiwinda na michezo ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Ulaya (Euro 2020) dhidi ya Jamhuri ya Czech na Bulgaria.

Delph mwenye umri wa miaka 29, alipatwa na majeraha ya nyama za paja akiwa katika mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Burnley, ambao walikubali kufungwa bao 1-0, Jumamosi.

Taarifa iliyotolewa na Chama cha Soka England (FA), imeeleza: "Hakuna nafasi ya mchezaji atakayeongezwa kuchukua nafasi ya Delph katika kipindi hiki."

Kocha Mkuu wa England Gareth Southgate ataendelea kukiandaa kikosi chake, ambacho kimesaliwa na wachezaji 24.

Viungo Dele Alli wa Tottenham na Jesse Lingard wa Manchester United ni sehemu ya wachezaji walioachwa wakati kocha huyo akitangaza kikosi juma lililopita.

England inayoongoza msimamo wa Kundi A, baada ya kupata ushindi mara nne, itacheza dhidi ya Jamhuri ya Czech kesho, Ijumaa kabla ya kupambana na Bulgaria siku tatu baadaye.




## HOWARD ASTAAFU SOKA

**COLORADO, Marekani**

GOLIKIPA wa zamani wa Klabu za Manchester United na Everton, Tim Howard, ametangaza kustaafu soka, baada ya kucheza mchezo wake wa mwisho akiwa na Colorado Rapids ya Marekani.

Howard mwenye umri wa miaka 40, Januari alisema mwishoni mwa msimu wa Ligi Kuu ya Marekani (MLS) atastaafu kucheza soka, na kweli ametimiza ahadi yake akiwa na Colorado Rapids.

Mlinda mlango huyo kutoka nchini Marekani ametundika daluga huku akiweka historia ya kucheza michezo 339 ya Ligi Kuu ya England akiwa na Man Utd, kutwaa ubingwa wa Kombe la FA mara moja, na ubingwa wa Kombe la Ligi (kwa sasa linajulikana kama Carrabao Cup) mara tatu.

Akiwa na timu ya Taifa ya Marekani, Howard alicheza michezo 121, na ameshiriki fainali mbili za Kombe la Dunia (2010 na 2014). Alitangaza kustaafu kuitumikia timu ya Taifa ya Marekani mwaka 2017.

Alisajiliwa na Everton kwa mkopo mwaka 2006 akitokea Man Utd, na mwaka mmoja baadaye alisajiliwa moja kwa moja na klabu hiyo ya Goodison Park. Aliitumikia klabu hiyo katika michezo 413 ya michuano yote kwa kipindi cha miaka kumi.

Kwa sasa Howard anashilikia rekodi ya kuwa mlinda mlango aliyeokoa michomo mingi katika fainali za Kombe la Dunia - alifanya hivyo katika mchezo dhidi ya Ubelgiji kwa kuokoa michomo 15 mwaka 2014.

Hata hivyo, upande wa klabu, Howard hakustaafu kwa furaha, kufuatia klabu yake Colorado Rapids kupoteza dhidi ya LA FC kwa kufungwa mabao 3-1.



## HABARI MICHEZO

**LONDON, England**

DANI Ceballos amesema 'kufufuka' kwa Gareth Bale na James Rodriguez pale Real Madrid hakumfanyi ajutie kuondoka kwa 'Los Blancos' hao na kutua Arsenal.

Bale alionekana majaliwa yake hayajulikani pale Real Madrid na alionekana kuelekea Klabu ya Jiangsu Suning ya nchini China kulikopewa baraka na kocha, Zinedine Zidane, kabla ya mpango kuo kusitishwa dakika za mwisho.

Majaliwa ya James pia yalikuwa hayajulikani baada ya kurejea kwa miamba hao akitokea kucheza kwa mkopo wa miaka miwili kule Bayern Munich, lakini alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Napoli na Atletico Madrid, ila usajili huo haukufanikiwa.

Wachezaji hao wote wawili sasa ni kama 'wamefufuka' kwani wote wamekuwa chaguo la kwanza kwenye mechi nane za Ligi Kuu za Madrid ikiwa imekaa kileleni mwa msimamowa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, ikiwa na pointi mbili zaidi ya wapinzani wao, Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, Ceballos aliamua kuondoka pale Santiago Barnabeu na kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England.

Ceballos amecheza mechi 11 katika mashindano yote kwa Arsenal hadi sasa na sasa anasema alikuwa hafurahii maisha pale Madrid.

"Madrid ndio ni pazuri. Ndio, walikuwa na majeruhi wengi, lakini sihuzuniki kwa kutokuwa pale," alisema akiwaambia waandishi wa habari akiwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania.

"Nina furaha kubwa hapa Arsenal, nimecheza mechi 11, ambapo nimeonyesha ubora wangu na sasa nipo pale nilipotaka kuwapo."




# CEBALLOS
## HAJUTII KUSEPA MADRID

## AC Milan yamfukuza kocha Giampaolo

**MILAN, Italia**

MARCO Giampaolo amefukuzwa kama kocha mkuu wa klabu ya AC Milan baada ya kuiongoza katika mechi saba.

Rossoneri wamekuwa na mwanzo mbaya kwenye Ligi Kuu ya Italia msimu huu na hata ushindi wa 2-1 dhidi ya Genoa Jumamosi haukutosha kuishawishi bodi ya klabu hiyo kumbakiza Giampaolo.

**Baada ya kuchukua na fasi ya Gennaro Gattuso pale kwenye dimba la San Siro, Giampaolo alipewa jukumu la kuijenga Milan iliyomaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Serie A msimu uliopita, lakini iliianza vibaya kwa kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Udinese.**

Baadaye ikapata ushindi dhidi ya Brescia na Hellas Verona, lakini ikafungwa 2-0 na Inter na pia aikachapwa na Torino na Fiorentina.

Katika taarifa fupi iliyotolewa Jumanne na klabu hiyo ilieleza: "AC Milan inatangaza kuachana na Marco Giampaolo kutoka katika nafasi yake kama kocha wa kikosi cha kwanza.

"Klabu inashukuru kwa ushirikiano mzuri kwa kwa kipindi chote ilichokaa na Marco na inamtakia kila la heri."

Kocha wa zamani wa Inter, Stefano Pioli anatarajiwa kutajwa kama mrithi wa Giampaolo.

Pioli amekuwa hana timu tangu alipojiuzulu kama kocha wa Fiorentina, Aprili mwaka huu.

## Sanamu ya Ibrahimovic yazinduliwa Sweden

**MALMO, Sweden**

SANAMU ya mshambuliaji wa zamani Manchester United, Zlatan Ibrahimovic iliyojengwa katika mji wa nyumbani kwake nchini Sweden, imezinduliwa rasmi.

Sanamu hiyo ya shaba ambayo imepewa baraka na Chama cha Soka cha Sweden, ilizinduliwa mbele ya maelfu ya mashabiki nje ya Uwanja wa Klabu ya Malmo, juzi Jumanne.

"Bila kujali wapi umetoka, wapi ulipo, bila kujali unaonekanaje, sanamu hii ni ishara kwamba kila kitu kinawezekana," alisema Ibrahimovic.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alifunga mabao 62 katika mechi 116 alizoichezea Sweden kati ya mwaka 2001 na 2016.

Sanamu hiyo imebuniwa na msanii wa michoro wa Sweden, Peter Linde, na ina urefu wa futi nane na uzito wa kilo 500.

Ibrahimovic alianza soka katika klabu ya nyumbani kwake ya Malmo kabla ya kujiunga na Ajax, baadaye Juventus halafu Inter Milan, akacheza Barcelona, pia AC Milan, Paris St-Germain na Man United.

Aliondoka United na kwenda nchini Marekani ambako anacheza katika Ligi Kuu ya nchi hiyo, MLS, akiitumikia LA Galaxy tangu mwaka 2018.

Nahodha wa zamani wa England, David Beckham, nyota wa Ureno na Juventus, Cristiano Ronaldo na mshambuliaji wa Misri na Liverpool, Mohamed Salah pia nao wamejengewa sanamu za heshima nchini kwao.

Pia kuna sanamu nyingine ya Ibrahimovic katika makumbusho ya Grevin jijini Paris nchini Ufaransa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BALE AKASIRIKA, ATAKA KUONDOKA REAL MADRID

●●●Inaelezwa kwa sasa anapenda gofu zaidi kuliko soka, na ni kweli kwamba...

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Gareth Bale ana "hasira" na "amechoshwa" na miamba hiyo ya Hispania na sasa anataka kuondoka klabuni hapo, kwa mujibu wa mtangazaji wa BBC Radio 5 Live, Mhispania Guillem Balague.

Bale alijiandaa kujiunga na Klabu ya Ligi Kuu China, Jiangsu Suning kwa mkataba wa miaka mitatu majira ya joto, akiripotiwa kuwa angeingiza pauni milioni moja kwa wiki, lakini Real ilifuta dili hilo kwa sababu ilihitaji kulipwa ada ya uhamisho.

Julai, mwaka huu, Kocha wa Real, Zinedine Zidane, alisema "tunatumai ataondoka mapema", maoni ambayo wakala wa Bale, Jonathan Barnett alijibu: "Zidane ni fedheha, hajaonyesha heshima kwa mchezaji ambaye amefanya makubwa kwa Real Madrid."

Bale ametwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ubingwa La Liga mara moja, Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na Uefa Super Cup mara tatu pamoja Kombe la Klabu Bingwa Dunia katika kipindi chake hapo Real, huku akifunga zaidi ya mabao 100.

Baada ya mpango wake wa kutua China kuvunjika, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Wales mwenye umri wa miaka 30, alipotezea kwenda kujiandaa na msimu mpya jijini Munich, Ujerumani - ikieleweka kwamba hakuwa vizuri kiakili kuweza kucheza.

Alirudi kikosi Real msimu huu, akifunga mara mbili katika mechi saba wakati wakikwea kileleni mwa La Liga.

Lakini wiki iliyopita aliachwa katika kikosi kilichocheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Club Bruges, kabla ya kurejea kikosini wakati wakishinda 4-2 dhidi ya Granada Jumamosi.

"Gareth Bale amechoka," alisema Balague. "Hawezi kufanya hivyo tena. Wakati ambao alianza kusimama nje, akijua kuwa kadiri anavyocheza mechi atakuwa fiti, ghafla alilazimika kutazama jukwaani mchezo dhidi ya Bruges. Hakuna mtu ajuaye kwa nini.

"Ana hasira, amechanganyikiwa. Wakati Zidane aliporudi klabuni hapo, aliamua kwamba hamtaki Bale, bila yeyote kupewa sababu sahihi.

"Bale aliambiwa kwamba Zidane, na ambaye wanamahusiano ya kitaaluma, amefanya uamuzi usio sahihi na anamwandalia safari ya kuondoka.

"Wakala wake, Jonathan Barnett, alijipanga kumtafutia sehemu mbadala, lakini Bale alipenda kwa vyovyote vile kubaki klabuni hapo.

"Kitu ambacho nyota huyo wa Wales hakuelewa kabisa ni kwa nini milango ilifunguliwa kwake, na kisha hawakumruhusu tena kuondoka. Madrid ilikubali kutohitaji ada ya uhamisho kwa klabu hiyo ya China, Jiangsu Suning, lakini kisha walibadilika kwa sababu waliamiani klabu nyingine ya China ilikuwa tayari kulipa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kumnunua James Rodriguez, tetesi ambazo zilishia kuwa uongo.

"Bale amecheza vizuri katika wiki za hivi karibuni - sehemu ya sababu ikiwa ni kwamba ana hasira, na kwamba alitaka kujibu namna kocha alivyomtenda, na hatimaye ameasi katika hali yake.

"Inaelezwa kwamba anapenda gofu zaidi kuliko soka, na ni kweli kwamba haishi taaluma kwa nguvu ya wengine, ama ndani au nje ya uwanja.

"Anauliza tu kupata dakika uwanjani ili kuwa tayari kuonyesha ubora wake na kuwa tayari kuifungia mabao timu, kitu ambacho anakikosa.

"Kuachwa nje katika mechi dhidi ya Bruges ni vigumu kuelewa, kwa mara ya kwanza tangu atue Real Madrid majira ya joto 2013, mchezaji huyo raia wa Wales sasa anataka kuondoka. Anahisi kwamba si haki kwa kile kinachofanywa kwake."

## KWA UFUPI

**KOULIBALY, RICE LULU UTD**

Manchester United inazingatia uwezekano wa kumfuata kiungo wa West Ham na England, Declan Rice, 20, na beki wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 28, bila kujaji mustakabali wa baadaye wa Ole Gunnar Solskjaer. ***(Goal)***

**MOURINHO AVIZIA DILI SPURS**

Jose Mourinho anafuatilia upepo unavyokwenda Tottenham wakati akitazama kurejea kazini baada ya kutimuliwa na Manchester United mwaka huu 2019. ***(Mail)***

**GUARDIOLA ATANGAZA MAZITO**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema 'atajiweka kando' kama mambo hayatakwenda kama alivyopanga wakati huu wakiwa pointi nane nyuma ya vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool kwenye mbio za ligi hiyo. ***(Sun)***

**SOLSKJAER MGUU NJE NDANI**

Manchester United bado inataka kumpa muda zaidi Ole Gunnar Solskjaer ili kuweza kubadili mambo klabuni hapo licha ya kuanza vibaya msimu, lakini kwa mujibu wa taarifa zingine kocha huyo atatimuliwa kama atapoteza mechi dhidi ya Norwich mwishoni mwa mwezi. (Telegraph/Sun)

**SPURS KUPUKUTISHA LUNDO**

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino anapanga kumuuza kiungo Muingereza Eric Dier, 25, Mdenmark Christian Eriksen, 27, beki Muivory Coast Serge Aurier, 26, Kiungo Mkenya Kenyan Victor Wanyama, 28, na beki Muingereza Danny Rose wote hao watawekwa sokoni hapo Januari baada ya kikosi hicho kuanza vibaya msimu huu. ***(Times)***

**MOYES AITAMANI EVERTON**

David Moyes amefungua milango ya kurudi kuinoa klabu yake ya zamani, Everton, wakati huu kocha Marco Silva presha ya kutimuliwa ikiongezeka baada ya klabu hiyo kuwa katika ukanda wa kushuka daraja. ***(Mirror)***

**BATSHUAYI ATAKIWA PALACE**

Crystal Palace itapaswa kulipa pauni milioni 22 ili kuipata saini ya mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Michy Batshuayi, 26, ambaye alitumia nusu msimu uliopita akiichezea Selhurst Park kwa mkopo. ***(Express)***

**CEBALLOS AIFURAHIA ARSENAL**

KIUNGO wa Arsenal, Dani Ceballos, 23, amesema alifanya uamuzi sahihi wa kujiunga na 'Gunners' hao kwa mkopo akitokea Real Madrid baada ya kurejesha nafasi yake katika kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania. ***(Goal)***

**NAGELSMANN ANUKIA UNITED**

Manchester United inamtazama Kocho kinda wa RB Leipzig, Mjerumani Julian Nagelsmann, 32, kama kocha wao ajaye hapo Old Trafford. ***(Mail)***

**DYBALA AZIKANA UTD, SPURS**

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala, 25, amesema kamwe hakuwahi kutaka kuondoka Juventus majira haya ya joto licha ya kuhusishwa na kujiunga na Manchester United pamoja na Tottenham. ***(Tuttosport - in Italian)***

**PHILLIPS ATAKA KAZI SUNDERLAND**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Sunderland, Kevin Phillips anataka kupewa majukumu ya kukiongoza kikosi hicho cha Uwanja wa Light baada ya Jack Ross kutimuliwa. ***(Star)***

**DEMBELE AVUTIA VIGOGO**

Borussia Dortmund imejiunga katika mbio moja na Arsenal, Juventus na Paris St-Germain kuwania saini ya winga wa Celtic, Karamoko Dembele, 16. ***(Bild - in German)***

HABARI MICHEZO

# MCHENGA MABINGWA TENA SPRITE BBALL KINGS 2019

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya upinzani mkali kutanda katika fainali tatu zilizopigwa jijini Dar es Salaam, hatimaye timu ya mpira wa kikapu ya Mchenga Bball Stars, imeendeleza ubabe kwa kutwaa ubingwa wa mashindano ya Sprite Bball Kings 2019, hii ikiwa ni mara ya tatu mfululizo.

Mchenga imetwaa ubingwa baada ya kufanikiwa kushinda mechi ya tatu ya fainali dhidi ya Tamaduni, iliyochezwa juzi katika Uwanja wa Don Bosco Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, Mchenga Bball Stars ilishinda kwa vikapu 115 dhidi ya 109 vya Tamaduni, na hivyo kufanikiwa kutetea ubingwa huo ambao timu hiyo inaushikilia kuanzia mwaka 2017.

Kwa kubeba ubingwa huo, Mchenga Bball Stars imejinyakulia kitita cha Sh. milioni 10 za Kitanzania, huku mshindi wa pili ambaye ni Tamaduni akijinyakulia kitita cha Sh. milioni tatu. Katika fainali ya mchezo wa kwanza iliochezwa Ijumaa iliyopita, kwenye viwanja vya Don Bosco, Mchenga Bball Stars ilivutwa shati na kupata ushindi mwembamba wa vikapu 122 dhidi ya 121 vya Tamaduni.

Baada ya hapo ikafuata fainali ya mchezo wa pili iliofanyika Jumapili kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa, Mchenga Bball Stars ikaongeza kasi zaidi na kuibuka na vikapu 104 dhidi ya 89 vya Tamaduni.

Msemaji wa mchezo huo, Goza Chuma alisema, fainali ya mchezo wa tatu iliyofanyika juzi kwenye Uwanja wa Don Bosco, Tamaduni ilijiuliza tena na kujikuta ikipata kichapo cha vikapu 115 kwa 109.

"Mchenga imetwaa ubingwa kwa mara nyingine baada ya kufanikiwa kushinda kwenye fainali zote tatu dhidi ya Tamaduni, kwa hiyo hao ndio mabingwa wa Sprite Bball Kings 2019," alisema Goza.

Goza alisema, michuano hiyo ya Sprite Bball Kings 2019, ambayo ilihitimishwa rasmi juzi, iliandaliwa na East Africa TV na East Africa Radio kwa udhamini wa kinywaji cha Sprite.




Mabingwa wa mpira wa kikapu, timu ya Mchenga Bball Stars wakiwa na mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 baada ya kutwaa ubingwa wa Sprite BBall Kings 2019 juzi, hii ikiwa ni mara ya tatu mfululizo kubeba taji hilo. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# COCA-COLA yajitosa matembezi ya hisani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Coca-Cola Kwanza imesema inaendelea kudhamini matembezi ya kilomita tano yenye lengo la kukusanya zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wenye kusumbuliwa na saratani ya matiti hapa nchini.

Matembezi hayo yamepangwa kufanyika Jumatatu kwenye viwanja vya The Green (zamani Uwanja wa Farasi).

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Masoko na Biashara wa Coca-Cola Kwanza, Wahida Mbaraka, alisema kampuni yake inaona fahari kutumia sehemu ya faida yake kudhamini matembezi hayo ya hisani ili kusaidia kuboresha maisha ya wanawake hapa nchini.

Wahida alisema wanaona fahari kushiriki kwa mara ya nne mfululizo kudhamini mashindano hayo ambayo yanaandaliwa na Asasi ya Saratani Tanzania (TBCF), na ambayo yanatarajia kushirikisha zaidi ya watu 2,500 kutoka sehemu mbalimbali.

"Tunapenda kuwaambia pia, mgeni rasmi katika mbio hizo atakuwa Mkurugenzi Mkazi wa Coca-Cola, chapa ya Afrika Mashariki, John Ulanga, siku hizi saratani ya matiti si tishio kwa wanawake peke yao bali hata kwa wanaume vilevile. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba wanaume kujitokeza kupima ili kuona kama wana dalili za saratani ya matiti au la," alisema Wahida.

Naye Mratibu wa programu wa TBCF, Kisa Mwakatobe, alisema watatumia matembezi hayo ya hisani kama sehemu ya mazoezi ya mwili, pia kutoa elimu kwa jamii kuhusu saratani ya matiti na haki zinazohusiana na matibabu.

Mwakatobe alisema upo umuhimu wa kupima afya mara kwa mara kwa sababu ugonjwa huo ukigundulika katika hatua za awali unaweza kutibiwa kirahisi.

# Timu 24 kuwania ubingwa U-13

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya timu 24 zinatarajiwa kuchuana katika mashindano ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 13 (U-13), ambayo yanatarajiwa kufanyika Novemba 2, mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam.

Mashindano hayo ambayo yana baraka za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), yanatarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Gymkhana jijini na lengo la michuano hiyo ni kukuza vipaji vya wachezaji chipukizi.

**Akizungumza jijini jana, Meneja wa Kampuni ya Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, George Nyanda, alisema kuwa wanaamini mashindano hayo yatazalisha nyota mbalimbali ambao watakuja kuzitumikia klabu za Ligi Kuu Bara na Timu ya Taifa (Taifa Stars).**

Nyanda alisema kuwa ili timu iweze kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali, ni vizuri wachezaji chipukizi wakasaidiwa kutimiza ndoto zao kwa kupewa misingi iliyo bora.

"Tunasijisikia furaha kuwa sehemu ya mashindano haya ya vijana wa umri chini ya miaka 13, hii ni njia sahihi ya kukuza vipaji," alisema kwa kifupi Nyanda ambaye kampuni yake pia inadhamini Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatoa wachezaji wengi katika kikosi cha Stars.

Naye Meneja wa Matukio wa Kampuni ya Toyota Tanzania, Nadah Dhiyebi, alisema kuwa mashindano hayo yatasaidia kuwapa uzoefu wachezaji hao chipukizi ambao baadaye watapeperusha bendera ya nchi katika michuano mbalimbali ya kimataifa.

# MKUDE KUENDELEA KUULA TAIFA STARS

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU kukiwa na taarifa kuwa uongozi wa Simba umemfungia kwa muda kiungo wake, Jonas Mkude, kutokana na kosa la utovu wa nidhamu, Kocha Msaidizi wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Mgunda, amesema kwamba adhabu hiyo hawaitambui.

Mkude na kiungo wa kimataifa wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Clatous Chama, wanadaiwa kusimamishwa kwa muda usiojulikana baada ya kubainika walichelewa kuamka na hivyo kushindwa kusafiri na kikosi cha timu hiyo kwenda mikoa ya Kanda ya Ziwa (Kagera na Mara).

Hata hivyo, hakuna taarifa rasmi zilizotolewa na uongozi wa Simba, lakini imefahamika kwamba nyota hao wawili walishapeleka utetezi wao kuhusiana na makosa yanayowakabili.

Mgunda aliliambia gazeti hili kuwa Mkude anaendelea vema na mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa kuwafuata Rwanda kwa ajili ya mchezo wa kirafiki wa kimataifa unayotarajiwa kuchezwa Oktoba 14, mwaka huu jijini Kigali.

Kocha huyo alisema adhabu hiyo ya klabu yao hawaitambui, na wanachoangalia ni mwenendo wake ndani ya kikosi hicho.

"Sisi hatuna taarifa hizo za kufungiwa, kwa upande wetu hakuna kosa ambalo amefanya, yupo hapa kambini kwa wakati, anafanya mazoezi kikamilifu pamoja na wenzake, hatuwezi kuyaingilia yaliyopo kati yake na klabu yake," Mgunda alisema.

Kikosi cha Stars kinatarajiwa kuondoka nchini Jumamosi na kinatarajiwa kutumia mchezo huo ili kujiandaa na mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Sudan itakayochezwa Oktoba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa El Merreikh Omdurman.



Bale akasirika, ataka kuondoka Madrid

HABARI UK 30

'MSUVA MABAO'...




Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva akishangilia na wenzake baada ya kuifungia bao pekee timu yake ya Difaa Hassan El-Jadidi wakati ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji, FAR Rabat katika mchezo wa hatua ya 16-Bora ya Kombe la Morocco uliopigwa Uwanja wa Manispaa ya Kenitra juzi. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA: TUTAWASHANGAZA CAF

## Nahodha, Zahera wamwaga cheche droo ya mechi ya mchujo ikipangwa huku wakijigamba...

**Na Somoe Ng'itu**

TUTAWASHANGAZA! Nahodha msaidizi wa Yanga, Juma Abdul, amesema wamejipanga kupeperusha vema bendera ya Tanzania kuelekea katika hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga, ambao ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano hayo ya kimataifa, walitarajia kuwafahamu wapinzani wao jana usiku, baada ya kufanyika kwa droo ya michuano hiyo huko jijini Cairo, Misri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Abdul, alisema wanafahamu mechi zote za hatua hiyo ya makundi ni ngumu na zenye ushindani, lakini wamejiandaa kupambana ili kuhakikisha wanasonga mbele.

Abdul alisema wanafahamu wanapofanya vizuri, wanajiweka katika nafasi ya "kuvuna" fedha za Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ambazo wakizipata, zitawasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali klabuni kwao.

"Tunaweza kufika mbali na kuwashangaza wengi, katika mpira lolote linaweza kutokea, tunajua ni hatua ngumu, lakini kama tukiwa makini, tuna nafasi ya kusonga mbele, kikubwa ni kuendelea kujipanga," alisema beki huyo ambaye amerejea katika kikosi cha kwanza.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga Mkongomani Mwinyi Zahera, amesema kuwa anaendelea kurekebisha mapungufu aliyoyaona katika mechi zilizopita ili waweze kupata matokeo mazuri katika mashindano hayo ya kimataifa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Bado timu haichezi vizuri, tulianza ligi kwa kupoteza, tukapata pointi moja, na tukaifunga Coastal Union, bado tunahitaji kuwa imara ili kukabiliana na ushindani, tunaelekea sehemu ngumu zaidi, katika Ligi ya Tanzania na Kombe la Shirikisho Afrika," Zahera alisema.

Aliongeza kuwa anaamini wachezaji wake ambao ni majeruhi, watakuwa wamepona na kuanza kuitumikia timu baada ya mechi za ligi zitakapoanza tena.

Yanga ambayo iliong'olewa na Zesco katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ina jumla ya pointi nne baada ya kucheza mechi tatu za Ligi Kuu Bara huku watani zao Simba wenye pointi 12 kileleni mwa ligi hiyo, wakiwa wameshuka dimbani mara nne.

# Stars kundi la kifo kufuzu Afcon 2021

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars imepangwa kundi linaloonekana kuwa la kifo [gumu] kuwania tiketi ya kufuzu michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 nchini Cameroon.

Katika droo iliyopangwa usiku wa kuamkia jana Makao Makuu ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf), jijini Cairo nchini Misri, Stars imeangukia Kundi J pamoja na Tunisia, Libya na Equatorial Guinea.

Kwa upande wa majirani wa Stars, Uganda wapo Kundi B pamoja na Burkina Faso na Malawi na mshindi kati ya Sudan Kusini na Shelisheli zitakazomenyana katika mechi ya mchujo, wakati Kenya wapo Kundi G pamoja na Misri, Togo na Comoro.

Ethiopia wapo Kundi K pamoja na Ivory Coast, Niger na Madagascar, Rwanda huku Kundi F likiundwa na Cameroon, Cape Verde na Msumbiji, Burundi wao wapo Kundi E pamoja na Morocco, Mauritania na Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) na Sudan wapo Kundi C pamoja na Ghana, Afrika Kusini na mshindi kati ya Mauritius na Sao Tome & Principe.

Kundi A linaundwa na Mali, Guinea, Namibia na mshindi kati ya Liberia na Chad, Kundi D likiwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Gabon, Angola na mshindi kati ya Djibouti na Gambia, mabingwa watetezi, Algeria wapo Kundi H pamoja na Zambia, Zimbabwe na Botswana.

Washindi wa pili wa fainali zilizopita, Senegal wapo Kundi I pamoja na Congo, Guinea-Bissau na Eswatini na washindi wa tatu wa fainali za mwaka huu, Nigeria wapo Kundi L pamoja na Benin, Sierra Leone na Lesotho.

Mechi za makundi zitaanza kupigwa Novemba 11, mwaka huu, hadi Novemba 17 mwakani na washindi wawili wa kila kundi watafuzu fainali hizo zitakazofanyika nchini Cameroon ambayo imefuzu moja kwa moja kutokana na kuwa mwenyeji licha ya kushirikishwa hatua ya makundi na matokeo ya kundi lao yataamua tu mustakabali wa washiriki wengine kwenye kundi hilo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >